Hii ndiyo siri kuu ya Mungu ambayo imefichwa tangu zama zote zilizopita, na bado imefichwa kwa wote isipokuwa kundi maalum—watakatifu, au waumini waliojiweka wakfu. Lakini nini maana ya "Kristo ndani yenu?" Tumejifunza kwamba Yesu alitiwa mafuta kwa Roho mtakatifu (*Mdo. 10:38*), na hivyo tunamtambua kuwa ndiye Kristo—mpakwa-mafuta—kwa maana neno **Kristo** linamaanisha **mpakwa-mafuta**. Na Mtume Yohana anasema kwamba *upako* ambao *sisi* (waumini waliojiweka wakfu) tumeupokea *unakaa ndani yetu*. (*1 Yohana 2:27*) Hivyo watakatifu wa zama hizi za Injili ni kundi lililotiwa mafuta—likiwa limetiwa mafuta kuwa wafalme na makuhani kwa Mungu (*2 Kor. 1:21; 1 Petro 2:9*); na pamoja na Yesu, kiongozi na Bwana wao, wanaunda Mpakwa-mafuta wa Yehova—yaani, **Kristo.**

Kwa kupatana na fundisho hili la Yohana, kwamba sisi pia **tumetiwa mafuta,** Paulo anatuhakikishia kwamba siri hii iliyofichwa katika zama zilizopita, lakini ambayo sasa imefunuliwa kwa watakatifu, ni kwamba **Kristo** (Mpakwa-mafuta) "si kiungo kimoja, bali ni viungo vingi," kama vile ambavyo mwili wa mwanadamu ni mmoja, na una viungo vingi; lakini kama viungo

vyote vya mwili, vikiwa vingi, ni mwili mmoja, vivyo hivyo ndivyo alivyo Mpakwa-mafuta—Kristo. (*1 Kor. 12:12-28*) Yesu ametiwa mafuta kuwa Kichwa au Bwana juu ya Kanisa, ambalo ni mwili wake (au bibi-arusi wake, kama inavyoelezwa katika mfano mwingine—*Efe. 5:25-30*), na kwa umoja wao wanaunda **"Uzao" ulioahidiwa**—Mkombozi Mkuu: *"Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi." Gal. 3:29*

Mtume analionya Kanisa kwa makini juu ya madai yoyote ya kujikweza., akisema juu ya Yesu kwamba "*Mungu ameweka vitu vyote chini ya miguu yake, akamtoa awe kichwa juu ya vitu vyote kwa Kanisa, ambalo ndilo mwili wake," "ili kwamba awe mtangulizi katika yote..*" (*Efe. 1:22; Kol. 1:18*) Hata hivyo, chini ya mfano wa mwili wa mwanadamu, anaonyesha kwa uzuri na kwa nguvu uhusiano wetu wa karibu. Umoja huohuo Yesu pia aliufundisha, akisema, "*Mimi ndimi mzabibu, ninyi ni matawi*." *Yohana 15:5*

Umoja wetu na Bwana Yesu, kama viungo vya Kristo, kundi lililotiwa mafuta, unaonyeshwa vizuri na mfano wa piramidi.

Jiwe la kilele ni piramidi kamilifu. Mawe mengine yanaweza kujengwa chini yake, na, kama yanapatana na mistari yote bainifu ya jiwe la kilele, umati wote utakuwa piramidi kamilifu. Jinsi gani hili linaonyesha kwa uzuri msimamo wetu kama viungo vya "Uzao"—"Kristo." Tukiwa tumeunganishwa na Kichwa chetu na tukiwa katika uwiano mkamilifu naye, sisi, kama mawe yaliyo hai, tu wakamilifu; tukiwa tumetengwa naye, sisi si kitu.



Yesu, aliye mkamilifu, ameinuliwa juu sana, na sasa tunajitoa kwake ili tuweze kuumbwa na kufanywa kulingana na mfano wake, na ili tuweze kujengwa kama jengo la Mungu. Katika jengo la kawaida hakuna jiwe kuu la pembeni; lakini katika jengo letu kuna jiwe moja kuu la pembeni, "jiwe la kilele," kama il-ivyoandikwa: *"Tazama, naweka Sayuni jiwe kuu la pembeni, teule, lenye heshima"* – *"ambalo mkimwendea, jiwe lililo hai... ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya kiroho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za kiroho*[*]*, zinazokubalika na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo."* (*1 Petro 2:4-6*) Na punde sana, tunatumaini, muungano kati ya Yesu, "Kichwa," na "Kanisa, ambalo ni mwili wake," utakamilika.

Na, wapendwa wangu, ni lazima tuvumilie mapigo mengi na kung'arishwa sana—ni lazima tupitie mabadiliko mengi, na

[*] *Hati ya Sinai inaondoa neno za kiroho kabla ya neno dhabihu.*

kufananishwa sana na mfano wake, chini ya uongozi wa Mjenzi Mkuu; na ili kuwa na uwezo na ubunifu wa mjenzi ukidhihirishwa ndani yetu, tutahitaji kuona kwamba hatuna mapenzi yetu wenyewe yaliyopotoka ya kupinga au kuzuia utimilifu wa Mapenzi yake ndani yetu; ni lazima tuwe kama watoto wachanga na wanyenyekevu—" "*Naam, ninyi nyote jifungeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana; kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema. Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake;*" (*1 Petro 5:5,6*), kama alivyomkweza Kichwa chetu na Mtangulizi wetu. *Filip. 2:8,9*

Huu kwa kweli ni ujumbe wa ajabu, na, tunapoliendea Neno la Mungu kuuliza kuhusu mwito wetu mkuu, tunawakuta manabii wote wakitangaza kwa ufasaha neema [upendeleo au baraka] iliyotujia (*1 Petro 1:10*); huku mifano, na mafumbo, na maneno yaliyokuwa ya siri hadi sasa, yakianza kung'aa, yakiangaza nuru yake kwenye "njia nyembamba" ambayo kundi lililotiwa mafuta [Kristo] linaitwa kuikimbilia kwa ajili ya tuzo iliyofunuliwa sasa. Hii ilikuwa kweli ni siri ambayo haikuwahi kufikiriwa hapo awali—kwamba Mungu anakusudia kumwinua si tu mkombozi, bali mkombozi anayeundwa na viungo vingi. Huu ndib o **"mwito wa mkuu"** ambao waumini waliojiweka wakfu wa zama za Injili wamepata fursa ya kuufikia. Yesu hakujaribu kuufunua kwa wanafunzi walipokuwa watu wa asili, bali alingoja hadi Pentekoste walipotiwa mafuta—wakazaliwa katika asili mpya. Kutokana na maelezo ya Paulo tunajua kwamba ni "viumbe vipya" pekee wanaoweza sasa kuuthamini au kuuelewa mwito huu wa juu. Anasema:

> *"Lakini twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa [mpango], ambayo Mungu aliiazimu tangu milele kwa utukufu wetu; ambayo hakuna hata mmoja wa wakuu [viongozi] wa dunia hii aliyeijua;... kama ilivyoandikwa, 'Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, ndiyo Mungu aliyowaandalia wampendao'; lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho wake." 1 Kor. 2:6-14*

Katika waraka wake kwa Wagalatia, Paulo anafunua siri yote, na anaonyesha jinsi agano la Abrahamu litakavyotimizwa. Anaonyesha kwamba Sheria waliyopewa Israeli haikuingilia agano la asili (*Gal. 3:15-18*), na kwamba uzao wa Ibrahimu utakaobariki mataifa yote ni ***Kristo***. (Mstari wa 16) Kisha, akiendeleza wazo lililogusiwa tayari, kwamba Kristo anajumuisha wote waliotiwa mafuta kwa Roho, anasema: "*Kwa maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo;... na kama ninyi ni wa Kristo, basi, NINYI [pamoja na Yesu] uzao wa Ibrahimu, na warithi, sawasawa na ahadi*" iliyotolewa kwa Ibrahimu. (Mstari wa 27,29) Akifuata hoja hiyohiyo, anaonyesha (*Gal. 4*) kwamba Ibrahimu alikuwa mfano wa Yehova, Sara mfano wa agano au ahadi, na Isaka mfano wa Kristo (kichwa na mwili); na kisha anaongeza, "Sisi, ndugu, kama Isaka, tu watoto wa ahadi." (Mstari wa 28) Hivyo, mpango wa Mungu ulifichwa katika alama za mfano hadi Zama za Injili zilipoanza kumdhihirisha Kristo..

Kulikuwa na umuhimu wa kuifanya siri hii iendelee kufichwa, la sivyo isingefichwa hivyo. Ilikuwa ni muhimu, kwa sababu kuufunua mpango wote kwa wanadamu kungekuwa ni kuuharibu. Kama wanadamu wangejua, wasingemsulubisha Bwana wa utukufu wala Kanisa ambalo ni mwili wake. (*1 Kor. 2:8*) Si tu kwamba kifo cha Kristo, kama bei ya ukombozi wa mwanadamu, kingeingiliwa, kama mpango haungekuwa umefichwa kama siri kwa ulimwengu, bali pia jaribu la imani la Kanisa, kama washiriki katika mateso ya Kristo, lingezuiwa pia; kwa maana "Ulimwengu haututambui [kama warithi-pamoja naye] kwa sababu [kwa sababu hiyohiyo] haukumtambua yeye." *1 Yohana 3:1*

Si tu kwamba mpango wa Mungu, na Kristo ambaye ndiye mfano halisi wa mpango huo, ni siri kuu kwa ulimwengu, bali pia njia ya pekee ambayo kundi hili dogo linaitwa kuitembea inawaweka washiriki wake alama kama "**watu wa pekee**." Ilikuwa ni siri kwa ulimwengu kwamba mtu mwenye uwezo

mkubwa kama Yesu wa Nazareti angetumia muda na kipaji chake kama alivyofanya, ambapo, kama angeelekeza mawazo yake kwenye siasa, sheria, biashara au dini maarufu, angeweza kuwa mkuu na mwenye kuheshimiwa. Kwa maoni ya watu, alipoteza maisha yake kipumbavu, nao wakasema, "Ana pepo, tena ana wazimu." Maisha yake na mafundisho yake vilikuwa siri kwao. Hawakuweza kumwelewa.

Mitume na wenzao vivyo hivyo walikuwa siri ulimwenguni, kwa kuacha matarajio yao ya kibiashara, n.k., ili kuhubiri msamaha wa dhambi kupitia kifo cha Yesu aliyedharauliwa na kusulubishwa. Paulo aliacha cheo cha juu na ushawishi wa kijamii ili kufanya kazi kwa mikono yake, na kumhubiri Kristo, na taji isiyoonekana kwa waumini wote watakaoenenda katika nyayo zake. Hili lilikuwa la siri kiasi kwamba wengine walisema, "*Paulo, umerukwa na akili; kusoma sana kumekufanya uwe na wazimu*." Na wote wanaomfuata Bwana kwa namna hiyo, kama Paulo, wanahesabiwa kuwa wajinga kwa ajili ya Kristo.

Lakini mpango wa Mungu hautafichwa daima katika siri: mapambazuko ya Siku ya Milenia yanaleta nuru kamili zaidi ya Mungu kwa wanadamu, na "kumjua BWANA kutaifunika dunia yote." Jua la Haki, litakalochomoza likiwa na uponyaji katika mbawa zake, likiondoa giza la ujinga, ni Kristo katika utukufu wa Milenia—si Kichwa peke yake, bali pia viungo vya mwili wake; kwa maana imeandikwa: Tukiteseka pamoja naye, tutatukuzwa pamoja naye pia. *"risto atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu. "*; na *"Ndipo wenye haki watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao." Rum. 8:17; 2 Tim. 2:11,12; Kol. 3:4; Mt. 13:43*

Basi, kwa wote isipokuwa wale waliozaliwa(Walio pokea mbegu/kutungwa) kwa nia mpya, kwa kuipokea '**nia ya Kristo**,' ahadi tunazoziamini, na matumaini tunayoyathamini, huonekana kama njozi, na mambo yasiyowezekana kabisa kupokelewa au kuitendea kazi. Katika zama zijazo, Mungu atakapomimina "roho yake juu ya wote wenye mwili," kama

ambavyo katika zama hizi anaimimina juu ya "watumishi wake na wajakazi wake," ndipo kwa kweli wote wataelewa na kuthamini ahadi zinazoshikiliwa sasa na "kundi dogo"; nao watafurahia utii na kuinuliwa kwa Kanisa, wakisema, *"Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu; kwa kuwa arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari."* (*Ufu. 19:7*) Watafurahia kutukuzwa kwa Kanisa, ambalo kupitia kwake baraka zitakuwa zikiwatiririkia; na ingawa watatambua kwamba "ahadi zilizo kuu mno, na za thamani" walizorithi Wapakwa-mafuta (kichwa na mwili) si kwa ajili yao, bali zimetimizwa juu yetu, watabarikiwa na somo lililoonyeshwa katika Kanisa; na huku wakikimbilia baraka *zitakazotolewa kwao wakati huo*, watafaidika na mfano wa Kanisa, na kumtukuza Mungu kwa niaba yake. Lakini maarifa haya hayataleta tamaa; kwa maana chini ya utaratibu mpya wa mambo, wito wao wa kufikia asili kamilifu ya kibinadamu utawatosheleza kikamilifu, na utaonekana kuwa wa kutamanika zaidi kwao kuliko mabadiliko ya asili.

Ndipo "siri" itakuwa imekwisha; kwa maana ulimwengu utakuwa umekuja kuona kwamba ilikuwa ni roho ya Mungu ndani ya Kristo, na roho ya Kristo ndani yetu—Mungu aliyedhihirishwa katika mwili—ambayo hadi sasa walikuwa wameielewa vibaya. Ndipo wataona kwamba hatukuwa na wazimu, wala wajinga; bali kwamba tulichagua sehemu iliyo bora tulipokimbilia utajiri, heshima na taji, visivyoonekana na wao, lakini vya milele.

Kwa upande wa wakati, siri ya Mungu itakamilika katika kipindi cha kupigwa kwa tarumbeta ya saba [ya mfano]. (*Ufu. 10:7*) Hili linahusu siri katika maana zote mbili inazotumika: siri au sehemu zilizofichika za *mpango* wa Mungu zitatangazwa na zitaonekana wazi; na pia "siri ya Mungu," yaani Kanisa, mfano halisi wa mpango huo. Zote mbili zitakuwa zimekamilika wakati huo. Mpango wa siri, uliofichika, utakuwa umetafuta idadi kamili, na kamilifu ya viungo vya mwili wa Kristo, na hivyo, MWILI WA KRISTO, utakuwa umekamilika. Mpango huo utakoma kuwa

siri, kwa sababu hakutakuwa na lengo lingine la kuendeleza usiri wake. Ukuu wa siri, iliyofichwa kwa muda mrefu, na iliyofichika katika ahadi, mifano na mafumbo, na neema ya ajabu waliyopewa wale walioitwa kwenye ushirika wa siri hii (*Efe. 3:9*), vinatufanya tufikiri kwamba kazi itakayofuata kukamilika kwake, ambayo kwa miaka elfu sita Yehova amewaweka wanadamu katika matarajio na tumaini, ni lazima iwe kazi kubwa mno, kazi kuu, inayostahili maandalizi makuu kama hayo. Ni nini tusichoweza kutarajia katika baraka juu ya ulimwengu, pazia la siri litakapoondolewa na mvua za baraka kushuka! Hiki ndicho ambacho viumbe vyote vinaugua na kuwa na utungu pamoja hadi sasa, **vikisubiri** kukamilika kwa siri hii—kwa ajili ya kudhihirishwa kwa Wana wa Mungu, "Uzao" ulioahidiwa, ambao ndani yake wote watabarikiwa. *Rum. 8:19,21,22*

Toleo la Siku ya Bwana

"Nakutolea Wewe: Kila pigo la moyo, yote ni Yako; Kila kifungo changu cha kibinadamu; Kila furaha na kila maumivu; Kila tendo la nia au fikra— Mungu wangu Mbarikiwa! Kila tumaini na kila hofu; Kila tabasamu na kila chozi; Kila wimbo na tenzi, 'Laudamus Te.'

"Yatwae yote, Bwana wangu Mbarikiwa, Yafunge kwa kamba Yako ya siri; Jitukuze Wewe mwenyewe ndani yangu, Wewe Unayeabudiwa! Yazidishe kwa Neno Lako; Imarisha, bariki, ongeza, Bwana wangu Wa upendo mkamilifu! Wewe wa Kwanza na wa Mwisho!"

SOMO LA VI

KURUDI KWA BWANA WETU – KUSUDI LAKE, KUFANYWA UPYA KWA VITU VYOTE

KURUDI KWA BWANA WETU MARA YA PILI: NI YEYE MWENYEWE NA NI KABLA YA MILENIA – UHUSIANO WAKE NA KUJA KWAKE MARA YA KWANZA – UCHAGUZI WA KANISA NA KUONGOLEWA KWA ULIMWENGU – UCHAGUZI NA NEEMA – WAFUNGWA WA TUMAINI – USHUHUDA WA KIUNABII KUHUSIANA NA KUFANYWA UPYA – KURUDI KWA BWANA WETU: TUMAINI DHAHIRI LA KANISA NA ULIMWENGU.

KWAMBA Bwana wetu alikusudia wanafunzi wake waelewe kwamba kwa kusudi fulani, kwa namna fulani, na wakati fulani, atakuja tena, tunadhania, ni jambo linalokubaliwa na kuaminiwa na wote wanaoyafahamu Maandiko. Ni kweli, Yesu alisema, *"Na tazama, mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari"* (**Mathayo 28:20**), na kwa Roho yake na kwa Neno lake amekuwa pamoja na Kanisa daima, akiliongoza, akielekeza, akilifariji na kuwategemeza watakatifu wake, na kuwachangamsha katikati ya mateso yao yote. Lakini ingawa Kanisa limekuwa na ufahamu uliobarikiwa wa Bwana kuzijua njia zake zote na utunzaji na upendo wake wa daima, bado linatamani kurudi kwake binafsi alikoahidi; kwa maana, aliposema, *"Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi muwepo"* (**Yohana 14:3**), bila shaka alikuwa anazungumzia kuja kwake mara ya pili yeye **binafsi**.

Wengine hudhani alikuwa anamaanisha kushuka kwa Roho mtakatifu Siku ya Pentekoste; wengine, kuangamizwa kwa Yerusalemu, na kadhalika. Lakini, inavyoonekana watu hawa wanapuuza ukweli kwamba katika kitabu cha mwisho cha Biblia, kilichoandikwa takriban miaka sitini baada ya Pentekoste, na miaka ishirini na sita baada ya kuangamizwa kwa Yerusalemu, yeye aliyekuwa amekufa na sasa yu hai anazungumzia tukio hilo kama jambo ambalo bado liko mbeleni, akisema: *"Tazama, naja upesi, na thawabu yangu i pamoja nami."* Na Yohana aliyeongozwa

na Roho anajibu, *"Amina; na uje, Bwana Yesu."* —**Ufunuo 22:12, 20**

Idadi kubwa ya watu hufikiri kwamba wenye dhambi wanapoongoka hiyo ni sehemu ya kuja kwa Kristo, na kwamba ataendelea kuja hivyo mpaka ulimwengu wote utakapoongoka. Kisha, wanasema, atakuwa amekuja kikamilifu.

Ni dhahiri watu hawa wanasahau ushuhuda wa Maandiko juu ya jambo hili, unaoeleza kinyume cha matarajio yao: kwamba wakati wa kuja kwa Bwana wetu mara ya pili, ulimwengu utakuwa bado uko mbali sana na kumgeukia Mungu; *"Siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari. Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe... wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu"* (**2 Timotheo 3:1-4**); kwamba *"Lakini watu waovu na wadanganyifu wataendelea, na kuzidi kuwa waovu, wakidanganya na kudanganyika."* (**Mstari wa 13**) Wanasahau onyo maalumu la Bwana kwa kundi lake dogo: *"Basi, jiangalieni, mioyo yenu isije ikalemewa na ulafi, na ulevi, na masumbufu ya maisha haya; siku ile ikawajia ghafula, kama mtego unasavyo; kwa kuwa ndivyo itakavyowajia watu wote wakaao juu ya uso wa dunia nzima."* (**Luka 21:34, 35**) Tena, tunaweza kuwa na hakika kwamba inaposemwa, *"Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma; na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake,"* (**Ufunuo 1:7**), hakuna rejeleo linalofanywa kwa uongofu wa wenye dhambi. Je, watu wote huomboleza kwa sababu ya uongofu wa wenye dhambi? Kinyume chake, ikiwa kifungu hiki kinarejelea, kama karibu wote wanavyokubali, kuwapo kwa Kristo duniani, kinafundisha kwamba si wote duniani watakaopenda kuonekana kwake, kama ambavyo kwa hakika wangefanya ikiwa wote wangeongoka.

Wengine wanatarajia kuja halisi na uwepo wa Bwana, lakini wanaweka muda wa tukio hilo mbali sana, wakidai kwamba kupitia jitihada za Kanisa katika hali yake ya sasa, lazima ulimwengu umgeukie Mungu, na hivyo Zama za Milenia zianzishwe. Wanadai kwamba dunia itakapokuwa imeongoka, Shetani amefungwa, maarifa ya Bwana yameijaza dunia yote, na mataifa

hayajifunzi vita tena, hapo ndipo kazi ya Kanisa katika hali yake ya sasa itakapokuwa imekwisha. Pia wanadai kwamba, Kanisa litakapokuwa limetimiza jukumu hili kubwa na gumu, ndipo Bwana atakuja ili kuhitimisha mambo ya duniani, **kuwapa thawabu zao** waamini, na kuwahukumu wenye dhambi.

Baadhi ya maandiko, yakichukuliwa bila muktadha, yanaonekana kuunga mkono maoni haya; lakini Neno la Mungu na mpango wake vinapotazamwa kwa ujumla, maandiko hayo yote yataonekana kuunga mkono maoni kinyume, yaani: kwamba Kristo anakuja kabla ya uongofu wa ulimwengu, na anatawala kwa kusudi la kuuongoa ulimwengu; kwamba Kanisa sasa linajaribiwa, na kwamba thawabu walioahidiwa washindi ni kwamba baada ya kutukuzwa watashiriki pamoja na Bwana Yesu katika utawala huo, ambao ndio njia ya Mungu aliyoiteua kwa ajili ya kuubariki ulimwengu na kusababisha kumjua Bwana kumfikie kila kiumbe. Hizo ndizo ahadi maalum za Bwana: *"Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi."* (**Ufunuo 3:21**) *"Nao wakawa hai, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu."* **—Ufunuo 20:4**

Kuna maandiko mawili yanayotegemewa zaidi na wale wanaodai kwamba Bwana hatakuja mpaka baada ya Milenia, ambayo tungependa kuyaangazia hapa.

Moja ni, *"Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja."* (**Mathayo 24:14**)

Wanadai andiko hili linarejelea uongofu wa ulimwengu kabla ya mwisho wa Zama za Injili. Lakini **kutoa ushuhuda** kwa ulimwengu hakumaanishi uongofu wa ulimwengu. Andiko hili halisemi chochote kuhusu jinsi ushuhuda huo utakavyopokelewa. Ushuhuda huu umeshatolewa. Mnamo mwaka 1861, ripoti za Vyama vya Biblia zilionyesha kuwa Injili ilikuwa imechapishwa katika kila lugha ya dunia, ingawa si mamilioni yote ya wakazi wa dunia walikuwa wameipokea. La, hata nusu ya wale

watu bilioni moja na milioni mia sita walio hai hawajawahi kulisikia jina la Yesu. Japokuwa hivyo, sharti la andiko hilo limetimizwa: injili imehubiriwa katika ulimwengu wote kuwa ushuhuda—**kwa kila taifa**.

Mtume (**Matendo 15:14**) anatuambia kwamba **kusudi kuu** la Injili katika zama hizi za sasa ni **"kuchagua watu"** kwa ajili ya jina la Kristo—Kanisa linaloshinda, ambalo, wakati wa kurudi kwake mara ya pili, litaunganishwa naye na kulipokea jina lake. Kutoa ushuhuda kwa ulimwengu katika zama hizi ni kusudi la pili.

Andiko lingine ni, *"Uketi mkono wangu wa kuume, Hata niwafanyapo adui zako Kuwa chini ya miguu yako."* (**Zaburi 110:1**) Wazo lisilo wazi na la ujumla kuhusu andiko hili linaonekana kuwa ni kwamba Kristo anakaa kwenye kiti cha enzi cha kimwili mahali fulani mbinguni mpaka kazi ya kuvitiisha vitu vyote itakapokamilishwa kwa ajili yake kupitia Kanisa, na kwamba ndipo anakuja kutawala. Hili ni wazo potofu. Kiti cha enzi cha Mungu kinachorejelewa si cha kimwili, bali kinarejelea mamlaka na utawala wake mkuu; na Bwana Yesu ameinuliwa kushiriki katika utawala huo. Paulo anatangaza, *"Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno [Yesu], akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina."* Amempa **mamlaka** juu ya kila mamlaka nyingine, akimfuata Baba. Ikiwa Kristo anakaa kwenye kiti cha enzi cha kimwili mpaka adui zake wafanywe kuwa chini ya miguu yake [wote watiishwe], basi bila shaka hawezi kuja mpaka vitu vyote vitakapotishwa. Lakini ikiwa "mkono wa kuume" katika andiko hili haurejelei eneo maalum na kiti, bali, kama tunavyodai, unarejelea nguvu, mamlaka, na utawala, inafuata kwamba andiko linalozingatiwa halingepingana kwa vyovyote na maandiko mengine yanayofundisha kwamba anakuja *"kuvitiisha vitu vyote viwe chini yake"* (**Wafilipi 3:21**), kwa nguvu ya mamlaka aliyopewa. Kwa mfano: Tunasema Mfalme William yuko kwenye kiti cha enzi cha Ujerumani, lakini hatumaanishi kile kiti halisi cha kifalme, na kwa hakika ni mara chache sana anakikalia. Tunaposema yuko kwenye kiti cha enzi, tunamaanisha anatawala Ujerumani. Mkono wa kuume

humaanisha nafasi kuu, cheo cha juu cha heshima au upendeleo, karibu na mtawala mkuu. Hivyo, Mwanamfalme Bismarck aliinuliwa au kuketishwa kwenye mkono wa kuume wa mamlaka, na Mfalme wa Ujerumani; na Yusufu alikuwa kwenye mkono wa kuume wa Farao katika ufalme wa Misri—si kihalisi, bali kulingana na lugha ya picha iliyozoeleka. Maneno ya Yesu kwa Kayafa yanakubaliana na wazo hili: *"Tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni."* (**Mathayo 26:64**) Atakuwa mkono wa kuume wakati anapokuja, na atabaki mkono wa kuume wakati wa Zama za Milenia, na milele.

Uchunguzi zaidi wa mipango iliyofunuliwa ya Mungu utatoa mtazamo mpana zaidi wa kusudi la **kuja kwa Kristo mara ya kwanza** na **kurudi kwake mara ya pili**; na tunapaswa kukumbuka kwamba matukio yote mawili yanahusiana kama sehemu za mpango mmoja. Kazi maalum ya kuja kwake mara ya kwanza ilikuwa **kuwakomboa** wanadamu; na ile ya kurudi kwake mara ya pili ni **kurejesha**, na kubariki, na kuwaweka huru waliokombolewa. Baada ya kutoa maisha yake kuwa fidia kwa ajili ya wote, Mwokozi wetu alipaa juu ili kuiwasilisha dhabihu hiyo kwa Baba, na hivyo kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu wa mwanadamu. Anakawia na kumruhusu "mkuu wa ulimwengu huu" aendeleze utawala wa uovu, hadi baada ya kuchaguliwa kwa "Bibi-arusi, Mke wa Mwana-Kondoo," ambaye, ili ahesabiwe kuwa **anastahili** heshima hiyo, lazima ashinde mvuto wa ulimwengu huu mbovu wa sasa. Ndipo kazi ya kuwapa ulimwengu wa wanadamu baraka kuu walizohakikishiwa kwa dhabihu yake itakapopaswa kuanza, naye atakuja kuzibariki jamaa zote za dunia.

Ni kweli, kazi ya kurejesha na kubariki ingeweza kuanza mara moja, wakati bei ya fidia ilipolipwa na Mkombozi, na hapo kuja kwa Masihi kungekuwa tukio moja tu, utawala na baraka vikianza mara moja, kama mitume walivyotarajia mwanzoni. (**Matendo 1:6**) Lakini Mungu alikuwa ametangulia *"kutuwekea*

sisi [Kanisa la Kikristo] jambo lililo bora zaidi" (**Waebrania 11:40**); kwa hiyo ni kwa faida yetu kwamba utawala wa Kristo umetenganishwa na mateso ya Kichwa kwa karne hizi kumi na tisa.

Kipindi hiki kati ya kuja kwake mara ya kwanza na ya pili—yaani, kati ya kutolewa kwa fidia kwa ajili ya wote na kutolewa kwa baraka kwa wote—kimekusudiwa kwa ajili ya jaribio na uteuzi wa Kanisa, ambalo ni mwili wa Kristo. Kama isingekuwa hivyo, kuja kwake kungekuwa ni mara moja tu, na kazi itakayofanyika katika kipindi cha uwepo wake wa pili, katika Utawala wa Miaka Elfu (Milenia), ingefuata mara moja baada ya ufufuo wa Yesu.

Au, badala ya kusema kazi ya kuja kwa mara ya pili ingefuata mara moja ile ya kwanza, tuseme hivi: kama Yehova asingekusudia kufanya uteuzi wa "kundi dogo," yaani, "mwili wa Kristo," basi kuja kwa Kristo mara ya kwanza kusingetokea wakati ule kulipotokea. Badala yake, kungetokea wakati wa kuja kwake mara ya pili, na hivyo kuja kwake kungekuwa ni mara moja tu. Kwa maana ni wazi kwamba Mungu amepanga kuruhusu uovu kwa miaka elfu sita, na pia amepanga kwamba kusafishwa na kurejeshwa kwa vitu vyote kutimizwe katika kipindi cha miaka elfu ya saba.

Kwa kuona hivi, kuja kwa Yesu, kama dhabihu na fidia kwa ajili ya wenye dhambi, kulitokea mapema kabla ya wakati wa kubariki na kurejesha kwa muda wa kutosha tu kuruhusu uchaguzi wa "kundi dogo" lake la "warithio-pamoja." Hili litawapa wengine maelezo kuhusu kuchelewa kunakoonekana kwa upande wa Mungu katika kutoa baraka zilizoahidiwa, na zilizoandaliwa, katika fidia. Baraka zitakuja kwa wakati ufaao, kama ilivyopangwa mwanzoni, ingawa, kwa kusudi tukufu, bei ilitolewa mapema zaidi kuliko ambavyo wanadamu wangetarajia.

Mtume anatuarifu kwamba Yesu amekuwa hayupo duniani—yuko mbinguni—katika kipindi chote cha kati tangu kupaa kwake hadi mwanzo wa nyakati za kufanywa upya vitu vyote,

au Zama za Milenia—*"ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni **hata** nyakati za kufanywa upya vitu vyote,"* n.k. (**Matendo 3:21**) Kwa kuwa Maandiko yanafundisha hivi kwamba kusudi la kurudi kwa Bwana wetu mara ya pili ni kufanywa upya kwa vitu vyote, na kwamba wakati wa kuonekana kwake mataifa yatakuwa mbali na kuongoka kiasi cha kuwa na hasira (*"Na mataifa walikasirika"*—**Ufunuo 11:18**) na katika upinzani, ni lazima ikubalike kwamba aidha Kanisa litashindwa kutimiza utume wake, na kwamba mpango wa Mungu utakuwa umetatizwa, au sivyo, kama tunavyodai na tumeonyesha, kwamba uongofu wa ulimwengu katika zama hizi za sasa haukutarajiwa kutoka kwa Kanisa, bali utume wake umekuwa ni kuhubiri Injili ulimwenguni kote **kama ushuhuda**, na kujiandaa chini ya uongozi wa Mungu kwa ajili ya kazi yake kuu ya wakati ujao. Mungu bado hajatimiza hata kidogo uwezo wake wote kwa ajili ya uongofu wa ulimwengu. La, zaidi ya hayo: **bado hajawahi hata kujaribu** kuuongoa ulimwengu.

Huu unaweza kuonekana kama usemi wa ajabu kwa wengine, lakini watu kama hao na watafakari kwamba ikiwa Mungu amejaribu kazi kama hiyo ameshindwa vibaya; kwa maana, kama tulivyoona, ni sehemu ndogo tu ya mabilioni ya watu duniani ambayo imewahi kusikia kwa akili timamu kuhusu **jina pekee** ambalo kwa hilo wanapaswa kuokolewa. Tumesema kwa msisitizo tu maoni na mafundisho ya baadhi ya madhehebu makuu—Wabatisti, Wapresbiteri na wengine—yaani, kwamba Mungu anachagua au kuteua kutoka ulimwenguni "kundi dogo," Kanisa. Wanaamini kwamba Mungu hatafanya zaidi ya kulichagua Kanisa hili, wakati sisi tunapata Maandiko yakifundisha hatua zaidi katika mpango wa Mungu—**KUFANYWA UPYA** kwa ajili ya ulimwengu, kutakakotimizwa kupitia Kanisa teule, litakapokamilishwa na kutukuzwa. "Kundi dogo," washindi, wa Zama hizi za Injili, ni mwili tu wa **"Uzao"** ambao ndani yake au kupitia kwake jamaa zote za dunia zitabarikiwa.

Wale wanaodai kwamba Yehova amekuwa akijaribu kwa miaka elfu sita kuuongoa ulimwengu, na akishindwa wakati wote, ni lazima waone ni vigumu kupatanisha maoni hayo na uhakikisho wa Biblia kwamba makusudi yote ya Mungu yatatimizwa, na kwamba Neno lake halitamrudia bure, bali litafanikiwa katika **lile alilolituma**. (*"Ndivyo litakavyokuwa neno langu, litokalo katika kinywa changu; halitanirudia bure, bali litatimiza mapenzi yangu, nalo litafanikiwa katika mambo yale niliyolituma."* —**Isaya 55:11**) Ukweli kwamba ulimwengu bado haujaongoka, na kwamba kumjua Bwana bado hakujaijaza dunia, ni uthibitisho kwamba bado **halijatumwa** kwenye utume huo.

Hii inatufikisha kwenye mitazamo miwili ambayo imewagawa Wakristo kwa karne nyingi, yaani, **Uchaguzi** na **Neema ya Bure**. Kwamba mafundisho yote haya mawili, licha ya kuonekana kwake kupingana, yana uthibitisho wa Kimaandiko, hakuna mwanafunzi wa Biblia atakayeweza kukanusha. Ukweli huu unapaswa kutuongoza mara moja kudhania kwamba kwa namna fulani yote mawili ni lazima yawe ya kweli; lakini hayawezi kupatanishwa kwa njia yoyote isipokuwa kwa kuzingatia sheria ya mbinguni, **utaratibu**, na *"kulitumia kwa halali neno la kweli"* juu ya somo hili.

Utaratibu huu, kama unavyowakilishwa katika mpango wa nyakati, ukizingatiwa, utatuonyesha wazi kwamba ingawa Uchaguzi umekuwa ukiendelea katika zama hizi za sasa na zilizopita, kile ambacho kwa njia ya utofautishaji kinaitwa Neema ya Bure ni maandalizi ya Mungu yenye neema kwa ajili ya ulimwengu kwa ujumla wakati wa Zama za Milenia. Ikiwa sifa bainifu za vipindi na nyakati zilizoainishwa katika sura iliyotangulia zitakumbukwa, na vifungu vyote vinavyohusiana na Uchaguzi na Neema ya Bure vikachunguzwa na kuwekwa mahali pake, itagundulika kwamba vyote vinavyohusu Uchaguzi vinatumika kwa zama za sasa na zilizopita, wakati vile vinavyofundisha Neema ya Bure vinatumika kikamilifu kwa zama zijazo.

Hata hivyo, Uchaguzi, kama unavyofundishwa katika Biblia, si ule ulazimishaji wa kiholela, au itikadi ya majaliwa, ambayo kwa kawaida huaminiwa na kufundishwa na watetezi wake, bali ni uteuzi kulingana na kufaa na uwezo wa kukabiliana na lengo ambalo Mungu analikusudia, katika kipindi alichokipanga kwa kusudi hilo.

Fundisho la Neema ya Bure, linalotetewa na Waarmenia, pia ni onyesho kuu zaidi la fadhili tele za Mungu kuliko vile watetezi wake wenye bidii walivyowahi kufundisha. Neema au fadhili za Mungu katika Kristo daima ni za bure, kwa maana ya kwamba hazistahiliwi; lakini tangu anguko la mwanadamu katika dhambi, hadi wakati huu, baadhi ya fadhili za Mungu zimekuwa zikielekezwa kwa watu maalum, mataifa na makundi, wakati katika zama zijazo ulimwengu wote utaalikwa kushiriki fadhili zitakazotolewa wakati huo, kwa masharti yatakayojulishwa kwa wote, *"naye anayetaka, na ayatwae maji ya uzima bure."* **—Ufunuo 22:17**

Tukitazama nyuma, tunaona Mungu alivyomchagua Ibrahimu na uzao wake. Wao ndio walikuwa njia ambayo ingemleta yule Mzao wa ahadi, ili azibariki familia zote za dunia.. (*"Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi."* **—Wagalatia 3:29**) Tunaona pia kuchaguliwa kwa taifa la Israeli kutoka miongoni mwa mataifa yote, kama taifa ambalo, kwa njia ya mfano, Mungu alionyesha jinsi kazi kuu kwa ajili ya ulimwengu itakavyotimizwa—kukombolewa kwao kutoka Misri, Kanaani yao, maagano yao, sheria zao, dhabihu zao za dhambi, kwa ajili ya kufutwa kwa hatia na kunyunyiziwa kwa watu, na ukuhani wao kwa ajili ya utimilifu wa yote haya, vikiwa ni uwakilishi mdogo na wa kivuli wa ukuhani halisi na dhabihu halisi kwa ajili ya kutakaswa kwa ulimwengu wa wanadamu. Mungu, akizungumza na watu, alisema, *"Ni ninyi tu niliowajua katika jamaa zote za dunia."* (**Amosi 3:2**) Watu hawa pekee ndio waliotambuliwa mpaka Kristo alipokuja; naam, na hata baadaye, kwa maana huduma yake ilikuwa kwao tu, na

hakuwaruhusu wanafunzi wake waende kwa wengine—akisema, alipowatuma, *"Msiende katika njia ya Mataifa, wala msiingie katika mji wo wote wa Wasamaria."* Kwa nini, Bwana? Kwa sababu, anaeleza, *"Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli."* (**Mathayo 10:5, 6; 15:24**)

Muda wake wote aliutoa kwa ajili yao hadi kifo chake, na hapo ndipo ilipofanyika kazi yake ya kwanza kwa ajili ya ulimwengu, onyesho la kwanza la neema yake ya bure na iliyojaa tele, ambayo katika 'wakati wake' hakika itakuwa baraka kwa wote.

Hii, zawadi kuu zaidi ya Mungu, haikuwa na kikomo kwa taifa au kundi. Haikuwa kwa ajili ya Israeli pekee, bali kwa ajili ya ulimwengu wote; *"kwa maana Yesu Kristo, kwa neema ya Mungu, alionja mauti kwa ajili ya kila mtu."* —**Waebrania 2:9**

Na sasa pia, katika Zama za Injili, aina fulani ya uchaguzi inatumika. Baadhi ya sehemu za ulimwengu zimependelewa zaidi na Injili (ambayo ni ya bure kwa wote waisikiao) kuliko nyingine. Hebu tazama ramani ya ulimwengu na uone jinsi sehemu ndogo tu ilivyoangazwa au kubarikiwa kwa kiwango chochote kinachoonekana na Injili ya Kristo. Jilinganishe wewe, na fursa na maarifa yako, na mamilioni walio katika giza la kipagani leo, ambao hawajawahi kusikia wito, na kwa hivyo hawakuitwa. Wakati kundi lililoitwa (walioitwa kuwa wana wa Mungu, warithi wa Mungu, na warithi-pamoja na Yesu Kristo Bwana wetu—ambao wamefanya wito na uteule wao kuwa thabiti) litakapokamilika, ndipo mpango wa Mungu kwa ajili ya wokovu wa **ulimwengu** utakuwa ndio unaanza.

Hadi hapo **Uzao** utakapokuwa umechaguliwa, kukukuzwa, na kuinuliwa mamlakani, ndipo utakapomponda kichwa nyoka. *"Naye Mungu wa amani atamseta Shetani chini ya miguu yenu upesi. Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na iwe pamoja nanyi."* (**Warumi 16:20; Mwanzo 3:15**) Zama za Injili humwandaa yule bikira safi, yaani, **Kanisa la waaminifu**, kwa ajili ya Bwana Harusi ajaye. Na mwishoni mwa zama hizo, atakapokuwa amefanywa

"tayari"(**Ufunuo 19:7**), Bwana-arusi huja, na wale walio tayari huingia pamoja naye arusini—Adamu wa pili na Hawa wa pili wanakuwa mmoja, na ndipo kazi tukufu ya kufanya upya vitu vyote huanza. Katika kipindi kijacho, mbingu mpya na nchi mpya, Kanisa halitakuwa tena bikira aliyechumbiwa, bali Bibi-arusi; na ndipo *"Roho na Bibi-arusi wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, Njoo! Naye mwenye kiu na aje; na yeye anayetaka, na ayatwae maji ya uzima bure."* **—Ufunuo 22:17**

Zama za Injili, badala ya kuhitimisha utume wa Kanisa, ni maandalizi tu muhimu kwa ajili ya kazi kuu ya wakati ujao. Kwa ajili ya baraka hii iliyoahidiwa na inayokuja, viumbe vyote vinaomboleza na kuteseka pamoja hadi sasa, vikitazamia **kufunuliwa** kwa wana wa Mungu. (*"Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaugua pamoja, navyo vina utungu pamoja hata sasa... kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu."* **—Warumi 8:22, 19**) Na ni ukweli uliobarikiwa kwamba neema ya bure kwa kipimo kamili kabisa, si tu kwa walio hai bali pia kwa wale waliokufa, imeandaliwa katika mpango wa Baba yetu kama fursa iliyobarikiwa ya zama zijazo.

Wengine wanaoweza kuona baadhi ya baraka zinazopatikana wakati wa kurudi kwa Kristo mara ya pili, na wanaothamini kwa kiasi fulani ukweli ni kwamba Bwana anakuja kutoa baraka kuu iliyonunuliwa kwa kifo chake, wanashindwa kuliona pendekezo hili la mwisho, yaani: kwamba wale walio makaburini wana maslahi sawa katika utawala huo mtukufu wa Masihi kama wale ambao wakati huo watakuwa wamepungukiwa kidogo na utumwa wa uharibifu—kifo. Lakini kama vile ambavyo Yesu alikufa kwa ajili ya **wote**, ni hakika kwamba wote lazima wapate baraka na fursa alizozinunua kwa damu yake ya thamani. Kwa hiyo, tunapaswa kutarajia baraka katika Zama za Milenia juu ya wote walio makaburini mwao na vilevile juu ya wale wasio makaburini; na tutapata uthibitisho wa kutosha wa hili, tunapoangalia zaidi katika ushuhuda wa Bwana juu ya somo hili. Ni kwa sababu ya mpango wa Mungu wa kuwaachilia huru ndiyo

maana wale walio kaburini wanaitwa **"wafungwa wenye matumaini."**

Inakadiriwa kwamba wanadamu wapatao bilioni mia moja na arobaini na tatu wameishi duniani katika miaka elfu sita tangu kuumbwa kwa Adamu. Kati ya hao, makadirio ya juu kabisa ambayo yanaweza kufanywa kwa busara yangekuwa kwamba chini ya bilioni moja ndio waliokuwa watakatifu wa Mungu. Makadirio haya mapana yanaacha jumla kuu ya watu bilioni mia moja na arobaini na mbili (142,000,000,000) ambao walishuka katika mauti bila imani na tumaini katika *jina pekee* tulilopewa chini ya mbingu, wala kati ya wanadamu, ambalo litupasa kuokolewa kwalo. Hakika, sehemu kubwa sana ya watu hawa hawakuwahi kumjua wala kusikia habari za Yesu, na hawakuweza kumwamini yeye ambaye hawajapata kusikia habari zake.

Tunauliza, umati huu mkubwa, ambao takwimu haziwezi kuupa picha kamili, umepatwa na nini? Hali yao ikoje, na itakuwaje? Je, Mungu hakuwafanyia maandalizi hawa, ambao ni lazima alikuwa ameona mbele hali na mazingira yao? Au je, tangu kuwekwa kwa misingi ya ulimwengu, aliwaandalia maandalizi ya kinyama na yasiyo na huruma ya mateso yao yasiyo na tumaini na ya milele, kama watoto wake wengi wanavyodai? Au je, bado amewawekea akiba, katika urefu na kina na upana wa mpango wake, fursa kwa wote kupata maarifa ya **jina hilo pekee**, na, kwa kutii masharti, kufurahia uzima wa milele?

Kwa maswali haya, ambayo kila Mkristo mwenye kufikiri hujiuliza, na kutamani kuona yakijibiwa kwa kweli, na kwa kupatana na tabia ya Yehova, huja majibu ya aina mbalimbali:

Wasiomwamini Mungu hujibu:

> *Wamekufa milele. Hakuna maisha baada ya kifo. Hawataishi tena kamwe.*

Ukalvini unajibu,

Hawakuchaguliwa kuokolewa. Mungu aliwaamuru na kuwachagua tangu awali wapotee – waende kuzimu – na wako huko sasa, wakigaagaa kwa maumivu makali, ambako watabaki milele, bila tumaini.

Uarmenia unajibu,

Tunaamini kwamba Mungu huwasamehe wengi wao kwa sababu ya kutojua. Wale waliofanya vema kadiri ya ufahamu wao watakuwa na hakika ya kuwa sehemu ya "Kanisa la wazaliwa wa kwanza," hata kama hawakuwahi kusikia habari za Yesu.

Kwenye mtazamo huu wa mwisho, Wakristo wengi wa madhehebu yote hukubaliana (licha ya kauli za imani za baadhi yao kusema kinyume), kutokana na hisia kwamba mtazamo mwingine wowote haungeweza kupatanishwa na haki kwa upande wa Mungu.

Lakini je, Maandiko yanaunga mkono mtazamo huu wa mwisho? Je, yanafundisha kwamba kutojua ni msingi wa wokovu? La; msingi pekee wa wokovu unaotajwa katika Maandiko ni **imani** katika Kristo kama Mkombozi na Bwana wetu. *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, **kwa njia ya imani**."* (**Waefeso 2:8**) Kuhesabiwa haki kwa imani ndiyo kanuni ya msingi ya mfumo mzima wa Ukristo. Walipoulizwa, Nifanye nini nipate kuokoka? Mitume walijibu, Mwamini Bwana Yesu Kristo. *"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana **hapana jina jingine** chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo."* (**Matendo 4:12**); na *"kwa kuwa kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka."* **—Warumi 10:13**

Lakini Paulo anatoa hoja kwamba mtu lazima aisikie injili kabla ya kuamini, akisema, *"Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia?"* **—Warumi 10:14**

Wengine wanadai kwamba Paulo anafundisha kuwa **kutojua** kutawaokoa watu, anaposema kwamba *"Mataifa wasio na sheria, wayatendapo kwa tabia zao yaliyo ya sheria, wao wasio na sheria wamekuwa sheria kwa nafsi zao."* (**Warumi 2:14**) Wanahitimisha kutokana na hili kwamba sheria ambayo dhamiri zao huwapa

inatosha kuwahesabia haki. Lakini watu kama hao wanamwelewa Paulo vibaya. Hoja yake ni kwamba ulimwengu wote una hatia mbele za Mungu (**Warumi 3:19**); kwamba Mataifa, ambao hawakuwa na sheria iliyoandikwa, **walihukumiwa**, si kuhesabiwa haki, na nuru ya dhamiri, ambayo, iwe iliwatetea au kuwashtaki, ilithibitisha kwamba walipungukiwa na ukamilifu na hawakustahili uzima, kama vile Wayahudi waliokuwa na sheria iliyoandikwa **walivyohukumiwa** nayo; *"kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria."* (**Warumi 3:20**) Sheria aliyopewa Myahudi ilifunua udhaifu wake, na ilikusudiwa kumwonyesha kwamba hakuwa na uwezo wa kujihesabia haki mbele za Mungu; *"kwa sababu hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele zake [Mungu] kwa matendo ya sheria."* Sheria iliyoandikwa **iliwahukumu** Wayahudi, na Mataifa yalikuwa na nuru ya kutosha ya dhamiri **kuwahukumu**; na hivyo kila kinywa kinafungwa kisiweze kudai haki ya uzima, na ulimwengu wote unasimama ukiwa na hatia mbele za Mungu.

Tukikumbuka kauli ya Yakobo (**2:10**), kwamba yeyote atakayeishika sheria yote, isipokuwa akajikwaa katika neno moja, ana hatia, na hawezi kudai baraka yoyote iliyoahidiwa na Agano la Sheria, tunatambua kwamba kwa kweli *"hakuna mwenye haki, hata mmoja."* (**Warumi 3:10**) Na hivyo Maandiko hufunga kila mlango wa tumaini isipokuwa mmoja, yakionyesha kwamba hakuna hata mmoja kati ya waliohukumiwa anayeweza kupata uzima wa milele kwa matendo ya kustahili, na kwamba ni bure vivyo hivyo kutetea **kutojua** kama msingi wa wokovu. Kutojua hakuwezi kumpa mtu yeyote **thawabu** ya imani na utii.

Wakristo wengi, wasiopenda kuamini kwamba mamilioni mengi ya watoto wachanga wasio na hatia na wapagani watapotea milele (ambalo wamefundishwa linamaanisha kupelekwa mahali pa mateso ya milele na yasiyo na tumaini), wanasisitiza, licha ya kauli hizi za Biblia, kwamba Mungu hatawahukumu wasiojua. Tunavutiwa na ukarimu wa mioyo yao na uthamini wao kwa wema wa Mungu, lakini tunawasihi wasiwe na haraka ya

kuzitupilia mbali au kuzipuuza kauli za Biblia. Mungu ana baraka kwa wote, kwa njia iliyo bora zaidi kuliko kupitia kutojua.

Lakini je, watu hawa wanatenda kulingana na imani yao wanayoitangaza? La: ingawa wanakiri kuamini kwamba wasiojua wataokolewa kwa sababu ya kutojua kwao, wanaendelea kuwatuma wamisionari kwa wapagani kwa gharama ya maelfu ya maisha ya thamani na mamilioni ya pesa. Ikiwa wote, au hata nusu yao, wangeokolewa kupitia kutojua, ni kuwatendea madhara ya wazi kuwatuma wamisionari kuwafundisha habari za Kristo; kwa maana ni mmoja tu kati ya elfu anayeamini, wamisionari wanapowaendea. Ikiwa wazo hili ni sahihi, ingekuwa bora zaidi kuwaacha wabaki katika kutojua; kwa maana hapo idadi kubwa zaidi wangeokolewa.

Tukiendelea na hoja hiyo hiyo, je, hatuwezi kusema kwamba kama Mungu angewaacha **wanadamu wote** katika kutojua, **wote** wangeokolewa? Ikiwa ni hivyo, kuja na kifo cha Yesu havikuwa na maana, kuhubiri na mateso ya mitume na watakatifu vilikuwa bure, na ile inayoitwa injili, badala ya kuwa habari njema, ni habari mbaya sana. Kupelekwa kwa wamisionari kwa wapagani na wale wanaoamini mtazamo wa Kikalvini au wa itikadi ya majaliwa kuhusu uchaguzi, kwamba hatima ya milele ya kila mtu iliamuliwa bila kubadilika kabla ya yeye kuwepo, ni upuuzi na jambo lisilo na mantiki kabisaa.

Lakini Biblia, ambayo imejaa roho ya umisionari, haifundishi kwamba kuna njia kadhaa za wokovu—njia moja kwa imani, nyingine kwa matendo, na nyingine kwa kutojua. Wala haifundishi fundisho linalomvunjia Mungu heshima la itikadi ya majaliwa. Ingawa inaonyesha kila mlango mwingine wa tumaini ukiwa umefungwa dhidi ya jamii ya wanadamu, inaufungua wazi mlango ule mmoja, pekee, na kutangaza kwamba yeyote anayetaka anaweza kuingia katika uzima; na inaonyesha kwamba wote ambao sasa hawaoni au hawathamini fursa iliyobarikiwa ya kuingia, watafumbuliwa macho kwa wakati ufaao ili

waelewe na kuthamini kikamilifu. **Njia pekee**, ambayo kwayo yeyote na wote wa jamii iliyohukumiwa wanaweza kumjia Mungu, si kwa matendo ya kustahili, wala kwa kutojua, bali kwa imani katika damu ya thamani ya Kristo, iondoayo dhambi ya ulimwengu. (**1 Petro 1:19; Yohana 1:29**) Hii ndiyo Injili, habari njema ya furaha kuu, "**itakayokuwa** kwa WATU WOTE."

Tuseme sasa tunayaangalia mambo haya kama vile Mungu anavyotuambia, na tumwachie yeye mwenyewe jukumu la kuitakasa tabia yake. Hebu tuulize, Watu bilioni mia moja arobaini na mbili wamepatwa na nini?

Chochote kiwe kilichowapata, tunaweza kuwa na hakika kwamba sasa hawako katika hali ya mateso; kwa sababu, si tu kwamba Maandiko yanafundisha kuwa thawabu kamili haitolewi kwa Kanisa mpaka Kristo atakapokuja, atakapomlipa kila mtu (*"Kwa sababu Mwana wa Adamu atakuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika zake; ndipo atakapomlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake."* —**Mathayo 16:27**), lakini pia kwamba wasio haki watapokea adhabu yao wakati huo pia. Hali yao ya sasa iwe yoyote, haiwezi kuwa thawabu yao kamili; kwa maana Petro anasema, *"basi, Bwana ajua kuwaokoa watauwa na majaribu, na kuwaweka wasio haki katika hali ya adhabu hata siku ya hukumu;."* (**2 Petro 2:9**); na atafanya hivyo.

Ni wazo linalohuzunisha kwelikweli, hasa kwa mtu mwenye upendo, kufikiria kwamba wanadamu wenzetu wengi wanaweza kupotea kwa kukosa tu maarifa ya wokovu. Halafu, pia, kuna maandiko mengi ambayo inaonekana haiwezekani kuyapatanisha na yote haya. Hebu tuone: Kwa mtazamo wa wakati uliopita na wa sasa kama fursa pekee, tukiweka kando tumaini lote la kufanywa upya kwa vitu katika zama zijazo, tutaelewaje kauli hizi, *"Mungu ni upendo,"* na *"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee"?* (**1 Yohana 4:8; Yohana 3:16**) Je, haitaonekana kwamba ikiwa Mungu aliupenda ulimwengu sana angeweza kufanya

maandalizi, si tu kwamba waaminio waokolewe, bali pia kwamba wote wapate kusikia ili waweze kuamini?

Tena, tunaposoma, *"Kulikuwako Nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu, akija katika ulimwengu."* (**Yohana 1:9**), uchunguzi wetu unasema, Si kweli; si kila mtu ameangaziwa; hatuwezi kuona kwamba Bwana wetu amewaangazia zaidi ya wachache kati ya mabilioni ya watu duniani. Hata katika siku hii yenye nuru kiasi, mamilioni ya wapagani hawaonyeshi dalili za kuangaziwa huko; wala Wasodoma, wala umati wa wengine katika zama zilizopita.

Tunasoma kwamba Yesu Kristo, kwa neema ya Mungu, alionja mauti *"kwa ajili ya kila mtu."* (**Waebrania 2:9**) Lakini ikiwa alionja mauti kwa ajili ya watu bilioni mia moja arobaini na tatu, na kwa sababu yoyote ile dhabihu hiyo ikawa na matokeo kwa bilioni moja tu, je, ukombozi huo haukuwa umeshindwa kwa kiasi kikubwa? Na katika hali hiyo, je, kauli ya Mtume si pana mno? Tunaposoma tena, *"Tazama, nawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa WATU WOTE"* (**Luka 2:10**), na, tukitazama pembeni yetu, tunaona kwamba imekuwa habari njema kwa "kundi dogo" tu, na si kwa watu wote, tungelazimika kujiuliza kama malaika hawakuzidisha wema na upana wa ujumbe wao, na kutia chumvi umuhimu wa kazi itakayotimizwa na Masihi waliyemtanganza.

Kauli nyingine ni, *"Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu; ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote."* (**1 Timotheo 2:5, 6**) Ukombozi kwa ajili ya wote? Basi kwa nini wote waliohusika wasipate faida kutokana na kifo cha Kristo? Kwa nini **wote** wasifikie ujuzi wa kweli, ili waweze kuamini?

Bila ufunguo, jinsi gani kauli hizi zinaonekana kuwa giza na zisizopatana; lakini tunapopata ufunguo wa mpango wa Mungu, maandiko haya yote yanatangaza kwa sauti moja, "Mungu ni upendo." Ufunguo huu unapatikana katika sehemu ya mwisho ya andiko lililotajwa mwisho—*"ambaye alijitoa mwenyewe kuwa*

ukombozi kwa ajili ya wote, ***utakaoshuhudiwa kwa majira yake****"* [au, **kwa wakati ufaao**].

Mungu ana wakati ufaao kwa kila kitu. Angeweza kuwashuhudia hawa katika maisha yao ya zamani; lakini kwa kuwa hakufanya hivyo, inathibitisha kwamba wakati wao ufaao ni lazima uwe wa wakati ujao. Kwa wale watakaokuwa sehemu ya Kanisa, bibi-arusi wa Kristo, na kushiriki heshima za ufalme, wakati wa sasa ndio "wakati ufaao" wa kusikia; na yeyote aliye na sikio la kusikia sasa, na asikie na kutii, naye atabarikiwa ipasavyo. Ingawa Yesu alilipa fidia yetu kabla hatujazaliwa, haukuwa "wakati wetu ufaao" kusikia habari zake kwa miaka mingi baadaye, na ni kuithamini tu ndiko kulikoleta wajibu; na huu, ulikuwa kwa kadiri ya uwezo na uthamini wetu tu. Kanuni hiyo hiyo inatumika kwa wote: katika wakati ufaao wa Mungu itashuhudiwa kwa wote, na wote watapata fursa ya kuamini na kubarikiwa nayo.

Maoni yaliyoenea ni kwamba kifo kinamaliza kipindi chote cha majaribio; lakini hakuna andiko linalofundisha hivyo; na yote yaliyo hapo juu, na maandiko mengine mengi zaidi, yangekuwa hayana maana, au mabaya zaidi, kama kifo kingemaliza tumaini lote kwa umati wa watu wasiojua ulimwenguni. Andiko moja linalotajwa kuthibitisha mtazamo huu unaoshikiliwa na wengi ni, *"Paangukapo ule mti, papo hapo utalala."* (**Mhubiri 11:3**) Ikiwa hili lina uhusiano wowote na mustakabali wa mwanadamu, linaonyesha kwamba hali yake yoyote anapoingia kaburini, hakuna mabadiliko yanayotokea mpaka aamshwe kutoka humo. Na hili ndilo fundisho linalofanana la maandiko yote yanayohusu somo hili, kama litakavyoonyeshwa katika sura zinazofuata.

Kwa kuwa Mungu hapendekezi kuwaokoa watu kwa sababu ya kutojua, bali *"hutaka* ***watu wote*** *waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli"* (**1 Timotheo 2:4**); na kwa kuwa umati wa wanadamu umekufa katika kutojua; na kwa kuwa *"hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima, huko kuzimu [kaburini]"* (**Mhubiri 9:10**);

kwa hiyo Mungu ameandaa kuamshwa kwa wafu, ili wapate maarifa, imani na wokovu. Kwa hiyo mpango wake ni, kwamba *"kama katika Adamu wote wanakufa, vivyo hivyo katika Kristo wote watahuishwa. Lakini kila mmoja kwa utaratibu wake"* —Kanisa la Injili, Bibi-arusi, mwili wa Kristo, kwanza; baadaye, wakati wa Zama za Milenia, wote watakaokuwa wake katika ile miaka elfu ya **kuwapo** kwake (tafsiri isiyo sahihi **kuja**), wakati ufaao wa Bwana kwa wote kumjua yeye, tangu aliye mdogo hata aliye mkuu. **—1 Wakorintho 15:22**

Kama kifo kilivyoingia kwa Adamu wa kwanza, ndivyo uzima unavyokuja kwa Kristo, Adamu wa pili. Kila kitu ambacho wanadamu walipoteza kwa kuwa katika Adamu wa kwanza kitarejeshwa kwa wale wanaoamini katika Adamu wa pili. Watakapoamshwa, wakiwa na faida ya uzoefu dhidi ya uovu, ambao Adamu hakuwa nao, wale watakaoupokea ukombozi kwa shukrani kama zawadi ya Mungu wanaweza kuendelea kuishi milele kwa sharti la asili la utii. Utii mkamilifu utahitajika, na uwezo mkamilifu wa kutii utatolewa, chini ya utawala wa haki wa Mfalme wa Amani. Huu ndio wokovu unaotolewa kwa ulimwengu.

Hebu sasa tuchunguze andiko lingine ambalo kwa ujumla hupuuzwa isipokuwa na Wauniversalisti; kwa maana, ingawa sisi si Wauniversalisti, tunadai haki ya kutumia, na kuamini, na kufurahia, kila ushuhuda wa Neno la Mungu. Linasomeka hivi, *"kwa maana twamtumaini Mungu aliye hai, aliye Mwokozi wa **watu wote**, hasa wa **waaminio**."* (**1 Timotheo 4:10**) Mungu atawaokoa watu wote, lakini hatawaokoa "kikamilifu" isipokuwa wale wanaomjia kupitia Kristo. Wokovu wa Mungu kwa watu wote si wa aina itakayopingana na hiari yao, au uhuru wao wa kuchagua, kuwapa uzima kinyume na matakwa yao: *"Nimekuwekea mbele yako uzima na mauti... **chagua** uzima, ili uwe hai."*

Simeoni alitofautisha aina hizi mbili za wokovu, akisema, *"Macho yangu yameuona wokovu wako,... Nuru ya kuwaangazia Mataifa, Na kuwa utukufu wa watu wako Israeli [Waisraeli wa kweli]."*

Hili linapatana na tangazo la Mtume, kwamba ukweli kuwa Yesu Kristo, Mpatanishi, alijitoa mwenyewe kuwa fidia kwa ajili ya wote **utashuhudiwa kwa wote** KWA WAKATI UFAAO. Hili ndilo litakalowajia watu wote, bila kujali imani au matakwa yao. **Habari hizi njema** za Mwokozi zitakuwa kwa **watu wote** (**Luka 2:10, 11**), lakini wokovu maalum kutoka katika dhambi na mauti utawajia tu **watu wake** (**Mathayo 1:21**)—wale wanaomwamini—kwa maana tunasoma kwamba hasira ya Mungu inaendelea kukaa juu ya asiyeamini. —**Yohana 3:36**

Tunaona, basi, kwamba wokovu wa jumla, utakaomjia kila mtu, unajumuisha nuru kutoka kwa nuru ya kweli, na fursa ya kuchagua uzima; na, kwa kuwa idadi kubwa ya jamii ya wanadamu iko kaburini, itakuwa muhimu kuwatoa makaburini ili kuwashuhudia habari njema za Mwokozi; pia kwamba wokovu maalum ambao waamini sasa wanafurahia kwa tumaini (**Warumi 8:24**), na ambao uhalisi wake utafunuliwa, katika Zama za Milenia, pia kwa wale "watakaoamini siku hiyo," ni **kufunguliwa kabisa** kutoka katika utumwa wa dhambi, na uharibifu wa mauti, na kuingia katika uhuru mtukufu wa watoto wa Mungu. Lakini kufikia baraka hizi zote kutategemea utii wa moyo wote kwa sheria za Ufalme wa Kristo—kasi ya kufikia ukamilifu ikionyesha kiwango cha upendo kwa Mfalme na kwa sheria yake ya upendo. Ikiwa yeyote, aliyeangazwa na Kweli, na kuletwa kwenye ujuzi wa upendo wa Mungu, na kurejeshwa (iwe kihalisi au kwa kuhesabiwa) kwenye ukamilifu wa kibinadamu, atakuwa "mwoga," na "kusitasita" (**Waebrania 10:38, 39**), yeye, pamoja na wasioamini (**Ufunuo 21:8**), wataangamizwa kutoka miongoni mwa watu. (**Matendo 3:23**) Hii ndiyo mauti ya pili.

Hivyo tunaona kwamba maandiko yote haya yaliyokuwa magumu hapo awali yanaelezwa na kauli—*"ushuhuda utakaotolewa kwa wakati wake."* **Kwa wakati ufaao**, nuru hiyo ya kweli itamwangazia kila mtu ambaye amekuja ulimwenguni. **Kwa wakati ufaao**, *"itakuwa habari njema ya furaha kuu kwa watu wote."* Na hakuna njia nyingine ya kutumia maandiko haya bila

kuyapotosha. Paulo anaendeleza hoja hii kwa msisitizo katika **Warumi 5:18, 19**. Anatoa hoja kwamba, kama watu wote walivyohukumiwa kifo kwa sababu ya kosa la Adamu, vivyo hivyo, haki ya Kristo, na utii wake hata mauti, vimekuwa msingi wa kuhesabiwa haki; na kwamba, kama wote walivyopoteza uzima katika Adamu wa kwanza, vivyo hivyo wote, bila kujali makosa ya kibinafsi, wanaweza kupokea uzima kwa kumkubali Adamu wa pili.

Petro anatuambia kwamba urejesho huu (kufanywa upya kwa vitu) umenenwa kwa vinywa vya manabii wote watakatifu. (**Matendo 3:19-21**) Wote wanafundisha hivyo. Ezekieli anasema kuhusu bonde la mifupa mikavu,

> *"Mifupa hii ni nyumba yote ya Israeli." Na Mungu anaiambia Israeli, "Kisha akaniambia, Mwanadamu, mifupa hii ni nyumba yote ya Israeli; tazama, wao husema, Mifupa yetu imekauka, matumaini yetu yametupotea; tumekatiliwa mbali kabisa. Basi tabiri, uwaambie, Bwana MUNGU asema hivi; Tazama, nitafunua makaburi yenu, na kuwapandisha kutoka katika makaburi yenu, enyi watu wangu, nami nitawaingizeni katika nchi ya Israeli. Nanyi mtajua ya kuwa mimi ndimi Bwana, nitakapoyafunua makaburi yenu, na kuwatoa ninyi katika makaburi yenu, enyi watu wangu. Nami nitatia roho yangu ndani yenu, nanyi mtaishi, nami nitawawekeni katika nchi yenu, nanyi mtajua ya kuwa mimi, Bwana, nimesema hayo, na kuyatimiza, asema Bwana. ."* ***– Ezekieli 37:11-14***

Na maneno ya Paulo yanakubaliana na hili (**Warumi 11:25, 26**) — *"kwa maana upofu umewapata Israeli kwa sehemu, mpaka utimilifu wa Mataifa [kundi teule, bibi-arusi wa Kristo] uwasili. Na hivyo Israeli wote wataokoka,"* au kurudishwa kutoka katika hali yao ya kutupwa; kwa maana *"Mungu hakuwasukumia mbali watu wake aliowajua tokea awali."* (**Mstari wa 2**) Walitupwa kutoka katika upendeleo wake wakati bibi-arusi wa Kristo alipokuwa anachaguliwa, lakini watarejeshwa kazi hiyo itakapokamilika. (**Mstari wa 28-33**) Manabii wamejawa na kauli za jinsi Mungu atakavyowapanda tena, nao hawatang'olewa tena.

> *"Maana, asema Bwana, Mungu wa Israeli,... Nitawakazia macho yangu kwa wema, nami nitawarudisha tena katika nchi hii; nami nitawajenga, wala sitawabomoa; nitawapanda, wala sitawang'oa. Nami nitawapa moyo wanijue, ya kuwa mimi ndimi Bwana; nao watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao; maana watanirudia kwa moyo wao wote." (**Yeremia 24:5-7; 31:28; Yeremia 32:40-42; 33:6-16**)*

Haya hayawezi kurejelea tu kurudishwa kutoka katika utumwa wa zamani huko Babeli, Shamu, n.k., kwa maana tangu wakati huo wameng'olewa tena.

Zaidi ya hayo, Bwana anasema, "*Siku zile, hawatasema tena, Baba za watu wamekula zabibu kali, na meno ya watoto wao yametiwa ganzi. Bali kila mtu [anayekufa] atakufa kwa sababu ya uovu wake mwenyewe.*" (**Yeremia 31:29, 30**) Hali si hii kwa sasa. Kwa sasa kila mmoja hafi kwa ajili ya dhambi yake mwenyewe, bali kwa ajili ya dhambi ya Adamu—"*Katika Adamu wote wanakufa*." Yeye alikula zabibu mbichi ya dhambi, na baba zetu waliendelea kuzila, wakirithisha magonjwa zaidi na taabu kwa watoto wao, na hivyo kuharakisha adhabu ya kifo. Siku ambayo *"kila mtu [anayekufa] atakufa kwa ajili ya dhambi yake mwenyewe,"* pekee, ni siku ya **Milenia au ya Urejesho**.

Ingawa unabii na ahadi nyingi za baraka za wakati ujao zaonekana kuwahusu Israeli pekee, ni lazima ikumbukwe kwamba walikuwa watu wa mfano, na kwa hiyo ahadi walizopewa, ingawa wakati mwingine zinawahusu wao hasa, kwa ujumla pia zina maana pana zaidi kwa ulimwengu wote wa wanadamu ambao taifa hilo liliuwakilisha. Wakati Israeli kama taifa ilikuwa mfano wa ulimwengu wote, ukuhani wake ulikuwa mfano wa "kundi dogo" teule, kichwa na mwili wa Kristo, "Ukuhani wa Kifalme"; na dhabihu, utakaso na upatanisho uliofanywa kwa ajili ya Israeli ulikuwa mfano wa "dhabihu zilizo bora," utakaso kamili zaidi na upatanisho halisi *"kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote,"* ambao wao ni sehemu yake.

Na si hivyo tu, bali Mungu anayataja kwa majina mataifa mengine na kuahidi urejesho wao. Kama mfano wenye nguvu tunawataja Wasodoma. Hakika, ikiwa tutapata urejesho wa Wasodoma ukifundishwa waziwazi, tunaweza kuridhika na ukweli wa fundisho hili tukufu la Urejesho kwa ajili ya wanadamu wote, lililonenwa kwa vinywa vya manabii wote watakatifu. Na kwa nini Wasodoma wasipate fursa ya kufikia ukamilifu na uzima wa milele kama Israeli, au kama yeyote kati yetu? Kweli, hawakuwa wenye haki, lakini wala Israeli haikuwa, wala sisi tunaosikia injili sasa. *"Hakuna mwenye haki, hata mmoja,"* ukiacha haki ya kuhesabiwa ya Kristo, aliyekufa kwa ajili ya wote. Maneno ya Bwana wetu mwenyewe yanatuambia kwamba ingawa Mungu alimwaga moto kutoka mbinguni na kuwaangamiza wote kwa sababu ya uovu wao, bado Wasodoma hawakuwa wenye dhambi wakubwa machoni pake kama walivyokuwa Wayahudi, waliokuwa na maarifa zaidi. (**Mwanzo 19:24; Luka 17:29**) Aliwaambia Wayahudi wa Kapernaumu, *"maana kama miujiza iliyofanyika kwako ingefanyika Sodoma, ungalikuwapo mji huo hata leo."* **—Mathayo 11:23**

Hivyo Bwana wetu anafundisha kwamba Wasodoma hawakupata fursa kamili; na anawahakikishia fursa hiyo anapoongeza (**mstari wa 24**), *"Walakini nawaambia, itakuwa rahisi nchi ya Sodoma kustahimili katika siku ya hukumu, kuliko wewe."* Tabia ya Siku ya Hukumu na kazi yake itaonyeshwa katika kurasa zinazofuata. Hapa tunaelekeza tu mawazo kwenye ukweli kwamba itakuwa wakati **unaoweza kustahimilika** kwa Kapernaumu, na bado **unaoweza kustahimilika zaidi** kwa Sodoma; kwa sababu, ingawa hakuna kati yao aliyekuwa bado amepata maarifa **kamili**, wala baraka zote zilizokusudiwa kuja kupitia "Uzao," bado Kapernaumu ilikuwa imetenda dhambi dhidi ya nuru kubwa zaidi.

Na kama Kapernaumu na Israeli wote watakumbukwa na kubarikiwa chini ya "Agano Jipya," lililotiwa muhuri kwa damu ya Yesu, kwa nini Wasodoma nao wasibarikiwe miongoni mwa

"jamaa zote za dunia"? Hakika watabarikiwa. Na ikumbukwe kwamba kwa kuwa Mungu *"alimwagia moto kutoka mbinguni na **kuwaangamiza wote**"* karne nyingi kabla ya siku za Yesu, urejesho wao unapozungumzwa, unamaanisha kuamshwa kwao, yaani, kutoka kwao kaburini.

Hebu sasa tuchunguze unabii wa **Ezekieli 16:48-63**. Usome kwa makini. Hapa Mungu anazungumza kuhusu Israeli, na kumlinganisha na jirani yake, Samaria, na pia na Wasodoma, ambao anasema hivi kuwahusu: *"Naliwaondoa nilipoona vema."* Wala Yesu wala Nabii hawatoi maelezo yoyote kuhusu kukosekana kwa usawa kunakoonekana katika matendo ya Mungu kwa kumwangamiza Sodoma na kuwaruhusu wengine wenye hatia kubwa kuliko Sodoma waendelee bila kuadhibiwa. Hilo lote litawekwa wazi wakati, kwa **"wakati ufaao**," makusudi yake makuu yatakapofunuliwa. Nabii anaeleza tu kwamba Mungu **"aliona vema**" kufanya hivyo, na Yesu anaongeza kuwa itakuwa rahisi zaidi kwao kustahimili katika siku ya hukumu kuliko wengine wenye hatia kubwa zaidi. Lakini kwa dhana kwamba kifo kinamaliza kipindi chote cha majaribio, na kwamba baada ya hapo hakuna anayeweza kupata fursa ya kufikia ujuzi wa kweli na kuutii, tunaweza kuuliza, Kwa nini Mungu aliona vema kuwaondoa watu hawa bila kuwapa nafasi ya wokovu kupitia ujuzi wa jina pekee ambalo kwalo wanaweza kuokolewa? Jibu ni, kwa sababu bado haukuwa **wakati wao ufaao**. Kwa "wakati ufaao" wataamshwa kutoka katika mauti na kuletwa kwenye ujuzi wa kweli, na hivyo kubarikiwa pamoja na jamaa zote za dunia, na "Uzao" ulioahidiwa. Hapo ndipo watakapokuwa kwenye jaribio la kupata uzima wa milele.

Kwa wazo hili, na si kwa lingine, tunaweza kuelewa matendo ya Mungu wa upendo kwa Waamaleki na mataifa mengine ambayo hakuwaruhusu tu bali aliwaamuru Israeli wawaangamize, akisema, *"asi sasa enda ukawapige Amaleki, na kuviharibu kabisa vitu vyote walivyo navyo, wala msiwaachilie; bali waueni, mwanamume na mwanamke, mtoto naye anyonyaye, ng'ombe na kondoo, ngamia na*

punda." (**1 Samweli 15:3**) Uharibifu huu wa maisha unaoonekana kuwa wa kizembe unaonekana kutopatana na tabia ya upendo anayopewa Mungu, na fundisho la Yesu, "*Wapendeni adui zenu*," n.k., hadi tunapokuja kutambua utaratibu uliopangwa wa mpango wa Mungu, "wakati ufaao" wa kutimizwa kwa kila sehemu yake, na ukweli kwamba kila mwanachama wa jamii ya wanadamu ana nafasi ndani yake.

Sasa tunaweza kuona kwamba Waamaleki hao, Wasodoma na wengine waliwekwa kama mifano ya ghadhabu ya haki ya Mungu, na ya azimio lake la kuwaangamiza kabisa na hatimaye watenda maovu: mifano ambayo haitakuwa na manufaa kwa wengine tu, bali pia kwao wenyewe, siku yao ya hukumu au jaribio itakapofika. Watu hao ingekuwa sawa tu kufa kwa njia hiyo kama kwa magonjwa na tauni. Haikuwa na maana kubwa kwao, kwani walikuwa wanajifunza tu kuujua uovu, ili watakapokuwa kwenye jaribio, kwa wakati ufaao, waweze kujifunza haki, na kuwa na uwezo wa kutofautisha na kuchagua mema na kuwa na uzima.

Lakini hebu tuchunguze unabii huo zaidi. Baada ya kumlinganisha Israeli na Sodoma na Samaria, na kutamka Israeli kuwa ndiye mwenye lawama zaidi (**Ezekieli 16:48-54**), Bwana anasema, *"Nitakapowarudisha tena wafungwa wao, yaani, wafungwa wa Sodoma na binti zake, na wafungwa wa Samaria na binti zake, ndipo nitakapowarudisha wafungwa wako waliofungwa kati yao."* Utumwa unaorejelewa hapa hauwezi kuwa mwingine isipokuwa utumwa wao katika mauti; kwa maana waliotajwa walikuwa wamekufa wakati huo. Katika mauti wote ni wafungwa; na Kristo anakuja kufungua milango ya kaburi, na kuwaweka huru wafungwa. (**Isaya 61:1; Zekaria 9:11**) Katika mstari wa 55 hili linaitwa *"kurudia hali yao ya kwanza"*—yaani, urejesho.

Wengine, ambao wako tayari kabisa kuipokea rehema ya Mungu kupitia Kristo katika msamaha wa makosa na udhaifu wao wenyewe chini ya nuru na maarifa makubwa zaidi, hawawezi kuwazia fadhili hiyo hiyo ikiwahusu wengine chini ya Agano

Jipya; ingawa wanaonekana kuikubali kauli ya Mtume kwamba Yesu Kristo, kwa fadhili ya Mungu, alionja mauti kwa ajili ya kila mtu. Baadhi ya hawa wanapendekeza kwamba ni lazima, katika unabii huu, Bwana anazungumza kwa dhihaka na Wayahudi, akimaanisha kwamba angekuwa radhi kuwarudisha Wasodoma kama wao, lakini hakuwa na nia ya kumrejesha yeyote kati yao. Lakini hebu tuone jinsi mistari inayofuata inavyopatana na wazo hili. Bwana anasema,

> *"Pamoja na hayo, **mimi nitalikumbuka** agano langu nawe, katika siku za ujana wako, **nami nitafanya** nawe agano la milele. **Ndipo, utakapozikumbuka** njia zako, na kutaabika, utakapowapokea dada zako... **Nami nitalifanya** imara agano langu nawe; nawe utajua ya kuwa mimi ndimi Bwana; upate kukumbuka, na kufadhaika, usifunue kinywa chako tena, kwa sababu ya aibu yako; **nitakapokupatanisha** kwa yote uliyoyatenda, ASEMA BWANA MUNGU."*

Ahadi inapotiwa saini hivi na Yehova Mkuu, wote waliotia muhuri wao kwamba Mungu ni kweli wanaweza kufurahia uhakika wake kwa ujasiri; hasa wale wanaotambua kwamba baraka hizi za Agano Jipya zimethibitishwa na Mungu katika Kristo, ambaye damu yake ya thamani inalitia muhuri agano hilo.

Kwa hili Paulo anaongeza ushuhuda wake, akisema,

> *"Na hivyo Israeli wote [walio hai na waliokufa] wataokoka [wataponywa upofu], kama ilivyoandikwa, 'Atatoka katika Sayuni Mwokozi, Na kumwondolea Yakobo ubaya wake. Na hili ndilo agano langu nao, Nitakapowaondolea dhambi zao.'... Wao ni wapendwa kwa ajili ya baba zao; kwa maana karama za Mungu na wito wake si vya kujutia." – **Warumi 11:26-29***

Hatupaswi kushangaa kwamba Wayahudi, Wasodoma, Wasamaria, na wanadamu wote, wataona aibu na kufedheheka **Mungu atakapodhihirisha** utajiri wa fadhila zake katika 'wakati wake ufaao". Naam, wengi wa wale ambao sasa ni watoto wa Mungu watafadhaika na kushangaa watakapoona jinsi Mungu **aliupenda** ULIMWENGU, na jinsi mawazo na mipango yake ilivyokuwa juu yao.

Watu wa Kikristo kwa ujumla huamini kwamba baraka za Mungu zote ni kwa ajili ya Kanisa teule pekee, lakini sasa tunaanza kuona kwamba mpango wa Mungu ni mpana kuliko tulivyodhania, na kwamba ingawa ametoa kwa Kanisa *"ahadi kubwa mno, za thamani,"* pia amefanya maandalizi tele kwa ajili ya ulimwengu alioupenda kiasi cha kuukomboa. Wayahudi walifanya kosa linalofanana sana walipodhani kwamba ahadi zote za Mungu zilikuwa kwao na kwa ajili yao pekee; lakini "*wakati ufaao*" ulipofika na Mataifa yakapendelewa, mabaki ya Israeli, ambao mioyo yao ilikuwa mikubwa kiasi cha kufurahia ushahidi huu mpana wa neema ya Mungu, walishiriki katika fadhila hiyo iliyoongezeka, huku wengine wakipofushwa na chuki na mapokeo ya wanadamu. Wale wa Kanisa wanaoiona sasa nuru inayopambazuka ya Zama za Milenia, pamoja na fursa zake za neema kwa ulimwengu wote, na wajihadhari wasije wakakutwa wakiipinga nuru inayoendelea, na hivyo kwa muda wakapofushwa wasione utukufu na baraka zake.

Jinsi gani mpango huu mtukufu wa Mungu wa kuwachagua wachache sasa, ili kuwabariki wengi baadaye, ulivyo tofauti na upotoshaji wa kweli hizi, kama unavyowakilishwa na mitazamo miwili inayopingana—Ukalvini na Uarmenia. Ule wa kwanza unakana fundisho la Biblia la Neema ya Bure na unalipotosha vibaya fundisho tukufu la Uchaguzi; ule wa pili unakana fundisho la Uchaguzi na unashindwa kuuelewa utimilifu uliobarikiwa wa Neema ya Bure ya Mungu.

Ukalvini unasema:

> *Mungu ni mwenye hekima yote; alijua mwisho tangu mwanzo; na kwa kuwa makusudi yake yote yatatimizwa, hangeweza kamwe kuwa alikusudia kuwaokoa wengine isipokuwa wachache tu, yaani, Kanisa. Hawa aliwachagua na kuwaamuru tangu awali waokolewe milele; wengine wote waliagizwa na kuchaguliwa vivyo hivyo kwenda kwenye mateso ya milele; kwa maana "Mungu anayajua matendo yake yote tangu mwanzo wa ulimwengu."*

Mtazamo huu una sifa zake nzuri. Unatambua ujuzi wa Mungu wa yote. Hii ingekuwa taswira yetu ya Mungu **mkuu**, isipokuwa kwamba sifa mbili muhimu za ukuu zinakosekana, yaani, upendo na haki, ambazo hakuna hata moja inayoonyeshwa kwa kuleta ulimwenguni watu bilioni mia moja arobaini na mbili ya viumbe waliohukumiwa kuteswa milele kabla ya kuzaliwa, na kudhihakiwa kwa maungamo ya upendo wake. Kwa kuwa Mungu ni upendo, na haki ndio msingi wa kiti chake cha enzi, tabia yake haiwezi kuwa hivyo.**Uarmenia** unasema:

> *Ndiyo, Mungu ni upendo; na katika kuleta wanadamu ulimwenguni hakuwakusudia madhara – bali mema tu. Lakini Shetani alifanikiwa kuwajaribu wanadamu wa kwanza, na hivyo dhambi ikaingia ulimwenguni, na mauti kwa njia ya dhambi. Na tangu wakati huo, Mungu amekuwa akifanya kila awezalo kumkomboa mwanadamu kutoka kwa adui yake, hata kumtoa Mwanawe. Na ingawa sasa, miaka elfu sita baadaye, injili imewafikia idadi ndogo sana ya wanadamu, bado tunatumaini na kuamini kwamba ndani ya miaka elfu sita ijayo, kupitia juhudi na ukarimu wa kanisa, Mungu atakuwa amerekebisha uovu ulioletwa na Shetani kiasi kwamba wote watakao kuwa hai wakati huo angalau wapate kujua upendo wake, na kuwa na fursa ya kuamini na kuokolewa.*

Wakati mtazamo huu unamwonyesha Mungu kama kiumbe aliyejaa mipango ya upendo na wema kwa ajili ya viumbe vyake, unadokeza kwamba anakosa uwezo na maarifa ya mbeleni ya kutosha kutimiza mipango yake ya wema: kwamba ana upungufu wa hekima na nguvu. Kutokana na mtazamo huu, ingeonekana kwamba wakati Mungu alipokuwa akijishughulisha na kupanga na kubuni kwa ajili ya wema wa watoto wake wapya, Shetani aliingia kimya kimya na kwa pigo moja la ubingwa akavuruga mipango yote ya Mungu kiasi kwamba, hata kwa kutumia nguvu zake zote, ni lazima Mungu atumie miaka elfu kumi na mbili kurejesha haki, hata kwa kiwango ambacho mabaki ya jamii ya wanadamu watakaoendelea kuishi watapata fursa ya kuchagua mema kwa urahisi kama wanavyochagua mabaya. Lakini watu bilioni mia moja arobaini na mbili ya miaka elfu sita iliyopita, na wengine wengi kama hao wa miaka elfu sita

ijayo, kulingana na mtazamo huu, wamepotea milele yote, licha ya upendo wa Mungu kwao, kwa sababu Shetani aliingilia mipango yake. Hivyo Shetani angeingiza maelfu katika mateso ya milele kwa kila mmoja ambaye Mungu anamwokoa kwenda kwenye utukufu.

Mtazamo huu ni lazima uinue mawazo ya watu kuhusu hekima na nguvu za Shetani, na ushushe tathmini yao ya sifa hizi kwa Mungu, ambaye Mtunga-zaburi kinyume chake anatangaza kwamba, *"Kwa kuwa yeye aliamuru, vikawa; na alivyoamuru, vilisimama imara."* Lakini la: Mungu hakushtukizwa wala kushindwa na adui; wala Shetani kwa namna yoyote hajavuruga mipango yake. Mungu ndiye, na daima amekuwa, bwana kamili wa hali hiyo, na mwishowe itaonekana kwamba yote yamekuwa yakifanya kazi pamoja kutimiza makusudi yake.

Wakati mafundisho ya uchaguzi na neema ya bure, kama yanavyofundishwa na Ukalvini na Uarmenia, hayawezi kamwe kupatanishwa yenyewe kwa yenyewe, na mantiki, au na Biblia, bado mafundisho haya mawili matukufu ya Biblia yanapatana kikamilifu na ni mazuri, yanapotazamwa kutoka kwa mtazamo wa mpango wa zama.

Tukiona, basi, kwamba sehemu nyingi kubwa na tukufu za mpango wa Mungu wa wokovu wa mwanadamu kutoka katika dhambi na mauti ziko katika wakati ujao, na kwamba kurudi kwa Bwana wetu Yesu mara ya pili ndiyo hatua ya kwanza iliyokusudiwa katika utimilifu wa baraka hizo zilizoahidiwa kwa muda mrefu na kutarajiwa kwa muda mrefu, je, hatupaswi kutamani kwa bidii zaidi wakati wa kurudi kwake mara ya pili kuliko Myahudi asiye na habari nyingi alivyotazamia na kutamani kuja kwake mara ya kwanza? Tukiona kwamba wakati wa uovu, udhalimu na mauti utakomeshwa na mamlaka ya nguvu atakayotumia wakati huo, na kwamba haki, kweli na amani zitakuwa za ulimwengu wote, ni nani asiyefurahi kuiona siku yake? Na ni nani ambaye sasa anateseka pamoja na Kristo, akitiwa moyo na ahadi ya thamani kwamba *"kama tukiteseka pamoja naye,*

tutatawala pamoja naye," hatainua kichwa chake na kufurahi kwa kila ushahidi wa kukaribia kwa Bwana, akijua kwa hilo kwamba ukombozi wetu na kutukuzwa kwetu pamoja naye kunakaribia? Hakika wote wanaounga mkono utume wake wa kubariki na roho yake ya upendo watasalimu kila ushahidi wa kuja kwake kama kukaribia kwa *"furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote."*

SOMO LA VII

KURUHUSIWA KWA UOVU NA UHUSIANO WAKE NA MPANGO WA MUNGU

KWA NINI UOVU ULIRUHUSIWA — HAKI NA UOVU KAMA KANUNI — HISIA YA MAADILI — MUNGU ALIRUHUSU UOVU, NA ATAUGEUZA ULETE WEMA — MUNGU SIYE MWANZILISHI WA DHAMBI — KUJARIBIWA KWA ADAMU HAKUKUWA MZAHA — KISHAWISHI CHAKE KILIKUWA KIKALI — ALITENDA DHAMBI KWA KUSUDI — ADHABU YA DHAMBI SIYO DHALIMU, WALA SI KALI MNO — HEKIMA, UPENDO NA HAKI ZIKIDHIHIRISHWA KATIKA KUWAHUKUMU WOTE NDANI YA ADAMU — SHERIA YA MUNGU IMEENEA POTE.

UOVU ni kile kinacholeta huzuni; kitu chochote ambacho, moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja, husababisha mateso ya aina yoyote—*Webster*. Kwa hiyo, somo hili, si tu kwamba linachunguza magonjwa ya wanadamu, huzuni, maumivu, udhaifu na kifo, bali linarudi nyuma ya yote haya kuzingatia chanzo chake cha msingi—**dhambi**—na suluhisho lake. Kwa kuwa dhambi ndiyo chanzo cha uovu, kuiondoa ndiyo njia pekee ya kuponya ugonjwa huu kabisa.

Labda, hakuna ugumu unaojitokeza mara kwa mara zaidi kwa akili inayochunguza kuliko maswali haya, Kwa nini Mungu aliruhusu utawala wa sasa wa uovu? Kwa nini alimruhusu Shetani awaletee majaribu wazazi wetu wa kwanza, baada ya kuwaumba wakiwa wakamilifu na wanyofu? Au kwa nini aliruhusu mti uliokatazwa uwe na nafasi kati ya miti mizuri? Licha ya majaribio yote ya kuliepuka, swali hili litajitokeza lenyewe—Je, Mungu hangeweza kuzuia uwezekano wote wa anguko la mwanadamu?

Bila shaka, ugumu huu unatokana na kushindwa kuuelewa mpango wa Mungu. Mungu angeweza kuzuia kuingia kwa dhambi, lakini ukweli kwamba hakufanya hivyo unapaswa kuwa uthibitisho wa kutosha kwetu kwamba kuruhusiwa kwake kwa sasa kumekusudiwa hatimaye kuleta wema mkubwa zaidi. Mipango ya Mungu, inapotazamwa katika ukamilifu wake, itathibitisha hekima ya njia aliyoifuata. Wengine huuliza, Je, Mungu, ambaye kwake mambo yote

yanawezekana, hangeweza kuingilia kati kwa wakati ili kuzuia utimilifu kamili wa mpango wa Shetani? Bila shaka angeweza; lakini kuingilia kati huko kungezuia utimilifu wa makusudi yake mwenyewe. Kusudi lake lilikuwa kudhihirisha ukamilifu, ukuu na mamlaka ya haki ya sheria yake, na kuwathibitishia wanadamu na malaika matokeo mabaya yanayotokana na kuivunja. Mbali na hilo, kwa asili yake, baadhi ya mambo hayawezekani hata kwa Mungu, kama Maandiko yanavyosema. *"Haiwezekani kwa Mungu kusema uongo."* (**Waebrania 6:18**) *"Hawezi kujikana mwenyewe."* (**2 Timotheo 2:13**) Hawezi kutenda kosa, na kwa hiyo hakuweza kuchagua mpango wowote isipokuwa ule wenye hekima na bora zaidi wa kuwaingiza viumbe vyake katika uzima, hata kama macho yetu yenye kuona karibu yangeshindwa kwa muda kutambua chemchemi zilizofichika za hekima isiyo na kikomo.

Maandiko yanatangaza kwamba vitu vyote viliumbwa kwa ajili ya furaha ya Bwana (**Ufunuo 4:11**)—bila shaka, kwa ajili ya furaha ya kugawa baraka zake, na ya kutumia sifa za nafsi yake tukufu. Na ingawa, katika utendaji wa mipango yake ya wema, anaruhusu uovu na watenda maovu kwa muda wawe na sehemu muhimu, lakini si kwa ajili ya uovu wenyewe, wala kwa sababu yeye anashirikiana na dhambi; kwa maana anatangaza kwamba yeye *"si Mungu apendezwaye na ubaya."* (**Zaburi 5:4**) Ingawa anaupinga uovu kwa kila namna, Mungu **anaruhusu** (yaani, hazuii) uovu kwa muda, kwa sababu hekima yake inaona njia ambayo kwayo unaweza kufanywa kuwa somo la kudumu na la thamani kwa viumbe vyake.

Ni ukweli unaojidhihirisha kwamba kwa kila kanuni ya haki kuna kanuni inayopingana nayo isiyo ya haki; kwa mfano, ukweli na uongo, upendo na chuki, haki na udhalimu. Tunatofautisha kanuni hizi zinazopingana kama **za haki** na **zisizo za haki**, kwa matokeo yake zinapotumika. Kanuni ambayo matokeo yake, inapokuwa inatenda, ni ya manufaa na huleta **utaratibu**, upatano na furaha, tunaiita **kanuni ya haki**; na ile inayopingana nayo, ambayo huleta mfarakano, huzuni

na uharibifu, tunaiita **kanuni uovu**. Matokeo ya kanuni hizi katika utendaji tunayaita **mema** na **mabaya**; na kiumbe mwenye akili, anayeweza kutofautisha kanuni ya haki na ile potofu, na kwa hiari anaongozwa na mojawapo, tunamwita **mwema** au **mwenye dhambi**.

Uwezo huu wa kupambanua kati ya lililo jema na lililo baya ndio unaoitwa **utambuzi wa kimaadili**, au **dhamiri**. Ni kupitia utambuzi huu wa kimaadili, ambao Mungu amempa mwanadamu, ndipo tunaweza kupima matendo ya Mungu na kutambua kuwa yeye ni mwema. Huu ndio utambuzi ambao Mungu daima huulenga ili kuthibitisha uadilifu na haki yake; na kwa kutumia utambuzi huohuo, Adamu aliweza kupambanua dhambi, au ukosefu wa haki, kuwa ni uovu, hata kabla ya kujua matokeo yake yote.

Viumbe wengine wa Mungu wasio wanadamu hawajajaliwa utambuzi huu wa kimaadili. Kwa mfano, mbwa ana akili kiasi, lakini si kwa kiwango hiki, ingawa anaweza kujifunza kwamba matendo fulani huleta kibali na thawabu kutoka kwa bwana wake, na mengine huleta kutokubaliwa. Anaweza kuiba au kuua, lakini hawezi kuitwa mwenye dhambi; au anaweza kulinda mali na maisha, lakini hawezi kuitwa mwema—kwa sababu haelewi uhalisia wa kimaadili wa matendo yake.

Mungu angeweza kumwumba mwanadamu akiwa hana uwezo wa kutofautisha kati ya mema na mabaya, au akiwa na uwezo wa kutambua na kutenda mema tu; lakini kumfanya hivyo ingekuwa ni kumfanya kuwa mashine hai tu, na hakika si sura ya kiakili ya Muumba wake. Au angeweza kumwumba mtu mkamilifu na mwenye hiari, kama alivyofanya, na kumlinda dhidi ya majaribu ya Shetani. Katika hali hiyo, uzoefu wa mwanadamu ungekuwa wa mema pekee, na angeendelea kuwa katika hatari ya kupokea mapendekezo ya uovu kutoka nje, au tamaa kutoka ndani, jambo ambalo lingefanya mustakabali wa milele usiwe na uhakika, na mlipuko wa uasi na fujo

ungeweza kuwa uwezekano daima; mbali na hilo, mema yasingeweza kamwe kuthaminiwa sana isipokuwa kwa kulinganishwa na uovu.

Mwanzoni, Mungu aliwafahamisha viumbe wake kuhusu wema kwa kuwazungushia wema huo katika bustani ya Edeni; na baadaye, kama adhabu kwa uasi wao, akawapa funzo kali kuhusu uovu.

Baada ya kuwafukuza kutoka Edeni na kuwanyima ushirika naye, Mungu aliwaruhusu wapitie magonjwa, maumivu na mauti, ili kwa njia hiyo wajue uovu milele na watambue jinsi dhambi isivyofaa na ilivyo mbaya kupita kiasi.

Kwa kulinganisha matokeo, walikuja kuthamini na kupima vizuri yote mawili; *"Kisha Bwana Mungu akasema, Basi, huyu mtu amekuwa kama mmoja wetu, kwa kujua mema na mabaya."* (**Mwanzo 3:22**) Katika hili vizazi vyao vinashiriki, isipokuwa kwamba wao kwanza wanapata ujuzi wao wa uovu, na hawawezi kutambua kikamilifu mema ni nini mpaka watakapoyapata katika Milenia, kama matokeo ya ukombozi wao na yeye ambaye wakati huo atakuwa Mwamuzi na Mfalme wao.

Ule utambuzi wa kimaadili, yaani, uwezo wa kupambanua kati ya jema na baya, pamoja na uhuru wa kuutumia, vilikuwa ni sifa muhimu zilizomfanya Adamu awe mfano wa Mungu. Sheria ya kutofautisha jema na baya ilikuwa imeandikwa katika maumbile yake. Ilikuwa ni sehemu ya asili yake, sawa na jinsi ilivyo sehemu ya asili ya Mungu.

Lakini tusisahau kwamba mfano huu wa Mungu, yaani, asili ya mwanadamu iliyokuwa na sheria ndani yake tangu mwanzo, umepoteza uhalisia wake kwa kiasi kikubwa kutokana na athari ya dhambi inayofuta na kudhalilisha. Kwa hiyo, hali ya sasa si sawa na ilivyokuwa kwa yule mwanadamu wa kwanza. Uwezo wa kupenda unamaanisha pia uwezo wa kuchukia; hivyo, tunaweza kusema kwamba Muumba hakuweza kumfanya mwanadamu kwa mfano wake, akiwa na uwezo

wa kupenda na kutenda mema, bila kumpa uwezo sawia wa kuchukia na kutenda mabaya. Huu uhuru wa kuchagua, unaoitwa **utashi binafsi**, ni sehemu ya kipawa cha asili cha mwanadamu; na uhuru huu, pamoja na vipawa vyake kamili vya kiakili na kimaadili, ndivyo vilivyomfanya awe mfano wa Muumba wake. Leo, baada ya miaka elfu sita ya uharibifu, sehemu kubwa ya ule mfano wa asili imefutwa na dhambi. Matokeo yake, hatuko huru, kwa kuwa tumefungwa, kwa kiwango kikubwa au kidogo, na dhambi na matokeo yake. Hivyo, sasa ni rahisi zaidi na inakubalika zaidi kwa jamii iliyoanguka kutenda dhambi kuliko kutenda haki.

Kwamba Mungu angeweza kumpa Adamu picha ya wazi ya matokeo mengi mabaya ya dhambi kiasi cha kumzuia asiitende, hatuna haja ya kutilia shaka, lakini tunaamini kwamba Mungu aliona mbele kuwa uzoefu halisi wa uovu ungekuwa somo la uhakika na la kudumu zaidi la kumsaidia mwanadamu milele; na kwa sababu hiyo Mungu hakuzuia bali alimruhusu mwanadamu afanye uchaguzi wake, na ahisi matokeo ya uovu. Kama fursa ya kutenda dhambi isingewahi kuruhusiwa, mwanadamu asingeweza kuipinga. Matokeo yake, kusingekuwa na wema wala sifa yoyote katika matendo yake mema. Mungu anawatafuta wale watakaomwabudu katika roho na kweli. Anataka utii unaotokana na ufahamu na utashi, badala ya utumishi usio na maarifa na unaofanywa kama mashine.

Tayari alikuwa na vyombo visivyo na uhai vilivyokuwa vinatimiza mapenzi yake kama mashine. Lakini kusudi lake lilikuwa kuumba kiumbe mtukufu zaidi: kiumbe mwenye akili kwa mfano wake mwenyewe, ambaye angekuwa bwana wa dunia. Uaminifu na uadilifu wa kiumbe huyo ungejengwa juu ya uelewa wake wa kina wa kutofautisha kati ya jema na baya.

Kanuni za mema na mabaya, kama **kanuni**, zimekuwepo daima, na ni lazima ziwepo daima; na viumbe wote wakamilifu, wenye akili, kwa mfano wa Mungu ni lazima wawe huru kuchagua mojawapo, ingawa

kanuni ya haki **pekee** ndiyo itaendelea kutumika milele. Maandiko Matakatifu yanatueleza kuwa uovu utakapokuwa umeruhusiwa kwa muda uliopangwa kutimiza kusudi la Mungu, basi utendaji wake utakoma kabisa. Tena, yanasema kwamba wale wote watakaoendelea kujisalimisha kwa udhibiti wa uovu watakoma kuwepo milele. (1 Wakorintho 15:25,26; Waebrania 2:14) Ni matendo mema na wale wayatendao tu ndio watakaodumu milele.

Lakini swali linajirudia kwa namna nyingine: Je, mwanadamu hangeweza kufahamishwa juu ya uovu kwa njia nyingine isipokuwa kwa uzoefu? Kuna njia nne za kujua mambo, nazo ni, kwa maarifa ya moja kwa moja (**intuition**), kwa **kuchunguza**, kwa **uzoefu**, na kwa **habari** inayopokewa kupitia vyanzo vinavyokubalika kuwa vya kweli kabisa. Maarifa ya moja kwa moja yangekuwa ni ufahamu wa papo hapo, bila mchakato wa kufikiri, au uhitaji wa uthibitisho. Maarifa kama hayo ni ya Yehova pekee, chemchemi ya milele ya hekima na kweli yote, ambaye, kwa ulazima na katika asili yenyewe ya mambo, yuko juu ya viumbe vyake vyote. Kwa hiyo, maarifa ya mwanadamu ya mema na mabaya hayakuweza kuwa ya moja kwa moja. Maarifa ya mwanadamu yangeweza kuja kwa kuchunguza, lakini katika hali hiyo ingehitajika kuwepo na onyesho la uovu na matokeo yake ili mwanadamu achunguze. Hili lingemaanisha kuruhusiwa kwa uovu mahali fulani, miongoni mwa viumbe fulani, na kwa nini isiwe miongoni mwa wanadamu, na duniani, kama ilivyo kwa wengine mahali pengine?

Kwa nini mwanadamu asiwe ndiye mfano, na apate maarifa yake kwa uzoefu halisi? Ndivyo ilivyo: mwanadamu anapata uzoefu halisi, na anatoa mfano kwa wengine pia, akiwa *"amefanywa kuwa tamasha kwa malaika.""...hakika utakufa"* ndiyo tafsiri ya pembeni ya **Mwanzo 2:17**.

Adamu tayari alikuwa na maarifa ya uovu kwa njia ya habari, lakini hiyo haikutosha kumzuia asijaribu. Adamu na Hawa walimjua Mungu kama Muumba wao, na hivyo kama yule aliyekuwa na haki

ya kuwadhibiti na kuwaongoza; na Mungu alikuwa amesema kuhusu mti uliokatazwa, *"Siku utakapokula matunda ya mti huo, hakika utakufa."*

Kwa hiyo, walikuwa na maarifa ya kinadharia ya uovu, ingawa hawakuwa wamewahi kuona wala kupata uzoefu wa matokeo yake. Kwa hiyo, hawakuthamini mamlaka ya upendo ya Muumba wao na sheria yake yenye manufaa, wala hatari ambazo kwa hiyo alikusudia kuwalinda nazo. Kwa hiyo walishindwa na jaribu ambalo Mungu alilirusu kwa hekima, ambapo hekima yake ilikuwa imefuatilia manufaa yake ya mwisho.

Wachache wanathamini ukubwa wa jaribu ambalo wazazi wetu wa kwanza walianguka chini yake, wala haki ya Mungu katika kuweka adhabu kali kiasi hicho kwa kile kinachoonekana kwa wengi kuwa kosa dogo sana; lakini tafakari kidogo itaweka yote wazi. Maandiko yanasimulia hadithi rahisi ya jinsi mwanamke, aliye dhaifu zaidi, alivyodanganywa, na hivyo akawa mkosaji. Uzoefu na kufahamiana kwake na Mungu kulikuwa na mipaka zaidi kuliko kwa Adamu, kwa maana yeye aliumbwa kwanza, na Mungu alikuwa amewasiliana naye moja kwa moja kabla ya kuumbwa kwa Hawa, akimpa maarifa ya adhabu ya dhambi, wakati Hawa labda alipokea habari zake kutoka kwa Adamu. Baada ya kula tunda, yeye, akiwa ameweka imani katika upotoshaji wa udanganyifu wa Shetani, ni dhahiri hakutambua ukubwa wa kosa hilo, ingawa labda alikuwa na wasiwasi, na hofu kidogo kwamba mambo hayakuwa sawa. Lakini, ingawa alidanganywa, Paulo anasema alikuwa mkosaji—ingawa hakuwa na hatia kubwa kama vile angekosa dhidi ya nuru kubwa zaidi.

Adamu, tunaambiwa, tofauti na Hawa, hakudanganywa (**1 Timotheo 2:14**), kwa hiyo ni lazima awe alikosa akiwa na utambuzi kamili zaidi wa dhambi, na huku adhabu ikiwa mbele yake, akijua hakika kwamba lazima afe. Tunaweza kuona kwa urahisi ni jaribu gani lililomsukuma aingie bila kujali katika adhabu iliyotamkwa. Tukikumbuka kwamba

walikuwa viumbe wakamilifu, katika mfano wa kiakili na kiadili wa Muumba wao, kipengele cha kimungu cha upendo kilionyeshwa kwa umaarufu mkubwa na mtu mkamilifu kwa mwenza wake mpendwa, mwanamke mkamilifu.

Akitambua dhambi na kuhofia kifo cha Hawa, na hivyo kumpoteza (na hilo bila tumaini la kumrejesha, kwa maana hakuna tumaini kama hilo lililokuwa limetolewa), Adamu, kwa kukata tamaa, aliamua bila kujali kutokuishi bila yeye. Akiona maisha yake mwenyewe kuwa ya huzuni na yasiyo na thamani bila ushirika wake, alishiriki kwa makusudi kitendo chake cha uasi ili kushiriki adhabu ya kifo ambayo labda alidhani ilikuwa juu yake. Wote wawili *"walikuwa katika kosa,"* kama Mtume anavyoonyesha. (**Warumi 5:14; 1 Timotheo 2:14**) Lakini Adamu na Hawa walikuwa mmoja na si *"wawili"*; kwa hiyo Hawa alishiriki hukumu ambayo mwenendo wake ulisaidia kumletea Adamu. **—Warumi 5:12, 17-19.**

Mungu hakutazamia tu kwamba, baada ya kumpa mwanadamu uhuru wa kuchagua, angeikubali dhambi kwa sababu ya kukosa uthamini **kamili** wa dhambi na matokeo yake, bali pia aliona kwamba, baada ya kuifahamu, bado angeichagua, kwa sababu kufahamiana huko kungeharibu sana asili yake ya kiadili kiasi kwamba uovu hatua kwa hatua ungekuwa wa kupendeza na wa kutamanika zaidi kwake kuliko wema. Bado, Mungu alikusudia **kuruhusu uovu**, kwa sababu, akiwa amekwishaandaa suluhisho la kumwokoa mwanadamu kutoka katika matokeo yake, aliona kwamba matokeo yake yangekuwa ni kumwongoza, kupitia uzoefu, kwenye uthamini kamili wa "ubaya mwingi wa dhambi" na uzuri usio na kifani wa wema kwa kulinganisha—hivyo kumfundisha zaidi kumpenda na kumheshimu Muumba wake, ambaye ndiye chanzo na chemchemi ya wema wote, na kuepuka milele kile kilicholeta ole na taabu nyingi. Hivyo matokeo ya mwisho yatakuwa upendo mkuu zaidi kwa Mungu, na chuki kubwa zaidi kwa yote yanayopingana na mapenzi yake, na matokeo yake, kuimarishwa imara katika haki ya

milele kwa wote watakaofaidika na masomo ambayo Mungu anayafundisha sasa kupitia kuruhusiwa kwa dhambi na maovu yanayohusiana nayo.

Hata hivyo, tofauti kubwa inapaswa kuonekana kati ya ukweli usiopingika kwamba Mungu ameruhusu dhambi, na kosa zito la wengine linalomshtaki Mungu kuwa ndiye mwandishi na mchochezi wa dhambi. Mtazamo wa pili ni wa kukufuru na unapingana na ukweli uliowasilishwa katika Maandiko. Wale wanaoangukia katika kosa hili kwa ujumla hufanya hivyo katika jaribio la kutafuta mpango mwingine wa wokovu kuliko ule ambao Mungu ameuandaa kupitia **dhabihu** ya Kristo kama gharama yetu ya ukombozi. Ikiwa watafanikiwa kujishawishi wenyewe na wengine kwamba Mungu ndiye anayehusika na dhambi na uovu wote na uhalifu*,na kwamba mwanadamu kama chombo kisicho na hatia mikononi mwake alilazimishwa kuingia katika dhambi, basi wametengeneza njia kwa ajili ya nadharia kwamba si dhabihu kwa ajili ya dhambi zetu, wala rehema kwa namna yoyote, iliyohitajika, bali kwa urahisi na pekee **HAKI**.

Hivyo, pia, wanaweka msingi kwa sehemu nyingine ya nadharia yao potofu, yaani, **Universalisti**, wakidai kwamba kama Mungu

---

* *Maandiko mawili (Isa. 45:7 na Amo. 3:6) yanatumiwa kutetea nadharia hii, lakini ni kwa tafsiri potofu ya neno uovu katika maandiko yote mawili. Dhambi sikuzote ni uovu, lakini uovu si sikuzote ni dhambi. Tetemeko la ardhi, moto mkubwa, mafuriko au tauni vingekuwa ni janga, yaani uovu; lakini hakuna kati ya hayo yangekuwa ni dhambi. Neno uovu katika maandiko yaliyotajwa linamaanisha majanga. Neno hilo hilo la Kiebrania limetafsiriwa mateso katika Zab. 34:19; 107:39; Yer. 48:16; Zek. 1:15. Limetafsiriwa shida katika Zab. 27:5; 41:1; 88:3; 107:26; Yer. 51:2; Omb. 1:21. Limetafsiriwa majanga, misiba, na dhiki katika 1 Sam. 10:19; Zab. 10:6; 94:13; 141:5; Mhu. 7:14; Neh. 2:17. Na neno hilo hilo katika sehemu nyingi sana limetafsiriwa madhara, uharibifu, uchungu, kuumia, taabu, huzuni na sikitiko."*
"Katika Isa. 45:7 na Amo. 3:6 Bwana alitaka kuwakumbusha Israeli juu ya agano lake alilofanya nao kama taifa – kwamba ikiwa wangetii sheria zake angewabariki na kuwalinda dhidi ya majanga yaliyo ya kawaida kwa ulimwengu kwa ujumla; lakini kwamba ikiwa watamuacha ataleta majanga (uovu) juu yao kama mapigo ya kuwarudi. Tazama Kum. 28:1-14, 15-32; Law. 26:14-16; Yos. 23:6-11, 12-16."
"Majanga yalipowajia, hata hivyo, walielekea kuyaona kama ajali na si kama mapigo ya kuwarudi. Hivyo Mungu aliwatumia neno kupitia manabii, akiwakumbusha agano lao na kuwaambia kwamba majanga yao yalitoka kwake na kwa mapenzi yake kwa ajili ya kuwarekebisha. Ni upuuzi kutumia maandiko haya kuthibitisha kuwa Mungu ni mwanzilishi wa dhambi, kwa maana hayarejelei dhambi hata kidogo.

alivyosababisha dhambi na uovu na uhalifu wote katika wote, atasababisha pia ukombozi wa wanadamu wote kutoka katika dhambi na mauti. Na wakifikiri kwamba Mungu alitaka kusababisha dhambi, na kwamba hakuna aliyeweza kumpinga, ndivyo wanavyodai kwamba atakapotaka haki wote vivyo hivyo hawatakuwa na nguvu za kumpinga. Lakini katika mawazo yote kama hayo, sifa bora zaidi ya mwanadamu, uhuru wa kutaka au **kuchagua**, sifa ya kushangaza zaidi ya kufanana kwake na Muumba wake, inawekwa kando kabisa; na mwanadamu kinadharia anashushwa hadhi kuwa mashine tu inayotenda tu inapotendewa.

Kama ingekuwa hivi, mwanadamu, badala ya kuwa bwana wa dunia, angekuwa duni hata kuliko wadudu; kwa maana bila shaka wao wana utashi au uwezo wa kuchagua. Hata sisimizi mdogo amepewa uwezo wa kutaka ambao mwanadamu, ingawa kwa nguvu zake kubwa anaweza kuupinga na kuuvuruga, hawezi kuuharibu.

Ni kweli, Mungu ana uwezo wa kumlazimisha mwanadamu aingie katika dhambi au katika haki, lakini Neno lake linatangaza kwamba hana kusudi kama hilo. Hakuweza kumlazimisha mwanadamu aingie katika dhambi kwa sababu ileile ambayo *"hawezi kujikana mwenyewe."* Kitendo kama hicho kingekuwa kinyume na tabia yake ya haki, na kwa hiyo ni jambo lisilowezekana. Naye anatafuta ibada na upendo wa wale tu wanaomwabudu katika roho na kweli. Kwa ajili hiyo amempa mwanadamu uhuru wa **utashi** unaofanana na wake, na anatamani yeye **achague** haki. **Kumruhusu** mwanadamu ajichagulie mwenyewe kulisababisha anguko lake kutoka katika ushirika na upendeleo na baraka za kimungu, na kuingia katika mauti. Kwa uzoefu wake katika dhambi na mauti, mwanadamu anajifunza kwa vitendo kile ambacho Mungu alijitolea kumfundisha kwa nadharia, bila yeye kupata uzoefu wa dhambi na matokeo yake. Kujua kwa Mungu mambo kabla hayajatokea hakutumiki dhidi ya mwanadamu, kama kisingizio cha kumshusha hadhi na kumfanya awe kama kiumbe

anayetenda mithili ya mashine tu. Kinyume chake, Mungu hutumia maarifa yake hayo kwa faida ya mwanadamu.

Kwa kuwa Mungu alijua tangu mwanzo njia ambayo mwanadamu angeichukua ikiwa angeachwa huru ajichagulie, hakumzuia asionje dhambi na matokeo yake machungu. Badala yake, alianza mara moja kuandaa njia ya kumwokoa kutoka katika kosa lake la kwanza. Alifanya hivi kwa kumuandaa Mkombozi, Mwokozi mkuu, awezaye kuwaokoa kikamilifu wote watakaomrudia Mungu kupitia yeye. Kusudi la yote haya lilikuwa hili: mwanadamu awe na utashi binafsi na wakati huohuo awezeshwe kunufaika kutokana na kosa lake la kwanza la kutumia vibaya utashi huo kwa kutotii mapenzi ya Bwana. Ili kutimiza hili, Mungu hakuandaa tu fidia kwa ajili ya wote, bali pia amepanga kwamba maarifa ya fursa hii ya upatanisho naye yashuhudiwe kwa watu wote kwa wakati ufaao. *(1 Timotheo 2:3-6)*

Ukali wa adhabu haukuwa onyesho la chuki na uovu kwa upande wa Mungu, bali ulikuwa matokeo ya lazima na yasiyoepukika, ya mwisho ya uovu, ambayo Mungu alimruhusu mwanadamu ayaone na kuyahisi. Mungu anaweza kuendeleza uhai kwa muda wote aonao inafaa, hata dhidi ya nguvu ya uharibifu ya uovu halisi; lakini isingewezekana kwa Mungu kuendeleza uhai kama huo milele, kama vile isivyowezekana kwa Mungu kusema uongo. Yaani, **haiwezekani Kwa kanuni ya maadili**. Uhai kama huo ungeendelea tu kuwa chanzo cha huzuni zaidi kwake na kwa wengine; kwa hiyo, Mungu ni mwema mno asiweze kuendeleza uwepo usio na maana na wenye madhara kwake na kwa wengine, na, nguvu yake ya kuendeleza uhai ikiondolewa, uharibifu, matokeo ya asili ya uovu, ungefuata. Uhai ni fadhila, zawadi ya Mungu, na utaendelezwa milele kwa watiifu pekee.

Hakuna udhalimu uliofanywa kwa vizazi vya Adamu kwa kutowapa kila mmoja jaribio la kibinafsi. Yehova hakuwa na wajibu wowote wa kutuleta sisi katika uwepo; na, baada ya kutuleta katika uwepo,

hakuna sheria ya usawa au haki inayomlazimisha kuendeleza uwepo wetu milele, wala hata kutupa jaribio chini ya ahadi ya uzima wa milele kama tungelikuwa watiifu. Weka alama vizuri kwenye hoja hii. Uhai wa sasa, ambao tangu utotoni hadi kaburini ni mchakato wa kufa tu, bado ni neema, ni fadhila, hata kama kusingekuwa na maisha ya baadaye, licha ya maovu na masikitiko yake yote. Wengi huuthamini hivyo, isipokuwa wachache (wanaojiua) ambao ni wachache kulinganisha; na hawa mahakama zetu za sheria zimeamua mara kwa mara kuwa hawana akili timamu, la sivyo wasingejinyima baraka za sasa hivi. Mbali na hilo, mwenendo wa mtu mkamilifu, Adamu, unatuonyesha jinsi mwenendo wa watoto wake ungekuwa chini ya hali kama hizo.

"Hakika utakufa"—hii ni rejea ya pembeni katika Biblia ya King James. Wengi wamejijengea wazo potofu kwamba Mungu aliiweka jamii yetu kwenye jaribio la uzima na mbadala wake ukiwa ni **mateso ya milele**, ambapo hakuna kitu kama hicho kinachodokezwa katika adhabu hiyo.

Fadhila au baraka ya Mungu kwa watoto wake watiifu ni uzima—uzima endelevu—usiokuwa na maumivu, magonjwa na kila kipengele kingine cha uharibifu na kifo. Adamu alipewa baraka hii kwa kipimo kamili, lakini alionywa kwamba atanyang'anywa "zawadi" hii kama angeshindwa kumtii Mungu—"Siku utakapokula matunda ya mti huo, hakika utakufa." Hakujua chochote kuhusu **uhai** katika mateso, kama adhabu ya dhambi. Uzima wa milele haujaahidiwa popote kwa yeyote isipokuwa watiifu. Uzima ni zawadi ya Mungu, na mauti, kinyume cha uzima, ndiyo adhabu anayoiamuru.

Mateso ya milele hayadokezwi popote katika Maandiko ya Agano la Kale, na ni kauli chache tu katika Agano Jipya zinazoweza kupotoshwa maana ili zionekane kana kwamba zinafundisha hivyo; na hizi zinapatikana aidha miongoni mwa ishara za kitabu cha Ufunuo, au miongoni mwa mifano na maneno ya fumbo ya Bwana

wetu, ambayo **hayakueleweka** na watu walioyasikia (**Luka 8:10**), na ambayo yanaonekana kueleweka vibaya zaidi leo. *"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti."* (**Warumi 6:23**) *"Nafsi itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa."* **—Ezekieli 18:4**

Wengi wamefikiri kuwa Mungu hakuwa mwenye haki kwa kuruhusu hukumu ya Adamu iwaguse vizazi vyake vyote, badala ya kumpa kila mmoja nafasi na jaribio la maisha ya milele sawa na lile alilofurahia Adamu. Lakini, watasema nini watu kama hao, ikiwa sasa itaonyeshwa kwamba fursa na jaribio la ulimwengu kwa ajili ya uzima litakuwa lenye neema zaidi kuliko la Adamu? Na zaidi ya hayo, hii itatokea **kwa sababu** Mungu alitumia mpango huu wa kuruhusu uzao wa Adamu kushiriki adhabu yake kwa njia ya kawaida? Tunaamini kuwa ndivyo ilivyo, na tutajitahidi kulieleza jambo hili kwa uwazi.

Mungu anatuhakikishia kwamba kama vile hukumu **ilivyowajia wote katika** Adamu, ndivyo amepanga kichwa kipya, baba au mtoauhai mpya kwa ajili ya jamii ya wanadamu, ambaye wote wanaweza kuhamishiwa kwake kwa imani na utii; na kwamba kama wote **katika** Adamu walivyoshiriki laana ya mauti, ndivyo wote **katika** Kristo watakavyoshiriki baraka ya urejesho; Kanisa likiwa la kipekee. (**Warumi 5:12, 18, 19**) Kwa kuona hivi, kifo cha Yesu, asiye na waa, asiye na dhambi, kilikuwa malipo kamili mbele za Mungu kwa ajili ya dhambi ya Adamu. Kama vile mtu mmoja alivyotenda dhambi, na wote waliokuwa ndani yake wakashiriki laana yake, adhabu yake, ndivyo Yesu, akiwa amelipa adhabu ya mkosaji huyo mmoja, alimnunua si Adamu tu, bali na vizazi vyake vyote—wanadamu wote—ambao kwa urithi walishiriki udhaifu na dhambi zake na adhabu ya haya—mauti. Bwana wetu, *"**mwanadamu** Kristo Yesu,"* yeye mwenyewe asiye na dosari, aliyekubaliwa, na akiwa na uzao au jamii kamilifu ndani yake, ambayo haijazaliwa, vivyo hivyo isiyo na doa la dhambi, alitoa **vyote** alivyo navyo vya maisha ya kibinadamu na haki yake kama **bei**

kamili ya ukombozi kwa ajili ya Adamu na jamii au uzao uliokuwa ndani yake ulipohukumiwa.

Baada ya kununua kikamilifu maisha ya Adamu na jamii yake, Kristo anajitolea kuwafanya wana kuwa uzao wake, watoto wake, wote wa jamii ya Adamu watakaokubali masharti ya Agano lake Jipya na hivyo kwa imani na utii kuingia katika familia ya Mungu na kupokea uzima wa milele. Hivyo Mkombozi *"ataona **uzao wake** [wengi wa uzao wa Adamu watakaokubali **kufanywa wana**, kwa masharti yake] na kuongeza siku zake [ufufuo kwenda kwenye daraja la juu kuliko la kibinadamu, akipewa na Baba kama thawabu ya utii wake],"* na yote kwa njia isiyotarajiwa kabisa; kwa kujitoa muhanga maisha yake na uzao wake. Na ndivyo ilivyoandikwa: *"Kama wote wanakufa katika Adamu, **vivyo hivyo** wote katika Kristo watahuishwa."* —Tafsiri iliyosahihishwa, **1 Wakorintho 15:22**

Jeraha tulilolipata kupitia anguko la Adamu (hatukutendewa dhuluma) litafidiwa na kuzidi kwa fadhila kupitia Kristo, kwa neema ya Mungu; na wote, mapema au baadaye (kwa "wakati ufaao" wa Mungu) watapata fursa kamili ya kurejeshwa kwenye hadhi ileile aliyoifurahia Adamu kabla ya kutenda dhambi. Wale wasiopokea maarifa kamili na, kwa imani, furaha ya fadhila hii ya Mungu kwa wakati huu (na hao ndio walio wengi zaidi, wakiwemo watoto na wapagani) bila shaka watapata fursa hizi katika zama zijazo, au "ulimwengu ujao," kipindi au zama zitakazofuata hizi za sasa. Kwa kusudi hili, *"wote walio makaburini...watatoka."* Kila mmoja (iwe katika zama hizi au zijazo) anapofahamu kikamilifu bei ya ukombozi iliyotolewa na Bwana wetu Yesu, na fursa zake zinazofuata, anahesabiwa kuwa yuko kwenye jaribio, kama Adamu alivyokuwa; na utii huleta uzima wa kudumu, na uasi huleta mauti ya kudumu—**"mauti ya pili."** Hata hivyo, utii mkamilifu, bila kuwa na uwezo mkamilifu wa kuutoa, hautakiwi kwa yeyote. Chini ya Agano la Neema, washiriki wa Kanisa wakati wa Zama za Injili wamehesabiwa haki ya Kristo kwa imani, ili kufidia upungufu wao usioweza kuepukika kupitia

udhaifu wa mwili. Neema ya Mungu pia itatenda kazi kwa ajili ya "yeyote atakaye" wa ulimwengu wakati wa Zama za Milenia. Hadi ukamilifu wa kimwili utakapofikiwa (ambayo itakuwa **fursa** ya wote kabla ya mwisho wa Zama za Milenia) ndipo ukamilifu kamili wa ki-adili utakapotarajiwa. Jaribio hilo jipya, matokeo ya ukombozi na Agano Jipya, litatofautiana na jaribio la Edeni, kwa kuwa ndani yake matendo ya kila mmoja yataathiri mustakabali wake mwenyewe tu.

Lakini je, hii haitakuwa ni kuwapa baadhi ya jamii ya wanadamu **nafasi ya pili** ya kupata uzima wa milele? Tunajibu—**Nafasi ya kwanza** ya uzima wa milele ilipotea kwa ajili yake mwenyewe na kwa ajili ya jamii yake yote, "ambao bado walikuwa katika viuno vyake," kwa uasi wa baba Adamu. Chini ya jaribio hilo la asili "hukumu ili-wajia watu wote"; na mpango wa Mungu ulikuwa kwamba kupitia dhabihu ya ukombozi ya Kristo, Adamu, na **wote** waliopoteza uzima katika kushindwa kwake, wapewe fursa ya kumrudia Mungu kwa imani katika Mkombozi, baada ya kuonja ubaya mwingi wa dhambi na kuhisi uzito wa adhabu ya dhambi. Ikiwa mtu yeyote atachagua kuiita hii "nafasi ya pili," na afanye hivyo: hakika itakuwa ni nafasi ya pili ya Adamu, na kwa namna fulani ni vivyo hivyo kwa jamii yote iliyokombolewa, lakini itakuwa ni fursa ya kwanza ya **kibinafsi** ya wazao wake, ambao, walipozaliwa, tayari walikuwa chini ya hukumu ya kifo. Iite upendavyo, ukweli unabaki uleule; yaani, wote wali-hukumiwa kifo kwa sababu ya uasi wa Adamu, na wote watafurahia (katika Zama za Milenia) **fursa kamili** ya kupata uzima wa milele chini ya masharti mazuri ya Agano Jipya. Hii, kama malaika walivyotangaza, ni "Habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote." Na, kama Mtume alivyotangaza, neema hii ya Mungu—kwamba Bwana wetu Yesu *"alijitoa mwenyewe kuwa **fidia kwa ajili ya wote"***—lazima "ishuhudiwe" kwa wote "kwa wakati ufaao." (**Warumi 5:17-19; 1 Timotheo 2:4-6**) Wanadamu, si Mungu, ndio wameweka kikomo cha nafasi hii ya kupata uzima kuwa katika Zama za Injili pekee. Mungu, kinyume chake, anatuambia kwamba Zama za

Injili ni kwa ajili tu ya uteuzi wa Kanisa, ukuhani wa kifalme, ambao kupitia kwao, katika zama zinazofuata, wengine wote wataletwa kwenye ujuzi sahihi wa kweli na kupewa fursa kamili ya kupata uzima wa milele chini ya Agano Jipya.

Hakuna udhalimu ndani ya Mungu; kwa hiyo *"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa **haki** hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."* (**1 Yohana 1:9**) Kama vile ambavyo angekuwa si wa haki kama angeturuhusu tuepuke adhabu iliyotamkwa kabla ya malipo kutolewa, ndivyo anavyotufahamisha hapa kwamba isingekuwa haki kama angetuzuia tusipate urejesho, kwa kuwa kwa mpango wake mwenyewe adhabu yetu imelipiwa kwa ajili yetu. Haki ileile isiyoyumba iliyomhukumu mwanadamu kifo hapo awali, sasa imeahidi kuwaachilia wote wanaoziungama dhambi zao na kuomba uzima kupitia Kristo. *"Ni nani atakayewashitaki wateule wa Mungu? Mungu ndiye mwenye kuwahesabia haki.Ni nani atakayewahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye aliyekufa; naam, na zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, naye yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea."* **—Warumi 8:33, 34**

Ukamilifu wa fidia ndiyo hoja yenye nguvu zaidi iwezekanavyo kwa ajili ya urejesho wa wanadamu wote watakaoikubali kwa

masharti yanayotolewa. (**Ufunuo 22:17**) Tabia yenyewe ya Mungu ya haki na heshima imeahidi hivyo; kila ahadi aliyoitoa inamaanisha hivyo; na kila dhabihu ya mfano ilielekeza kwenye dhabihu kuu na ya kutosha—*"Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye DHAMBI YA ULIMWENGU"*—ambaye ndiye *"upatanisho [malipo ya kuridhisha] kwa dhambi zetu [za Kanisa], wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote."* (**Yohana 1:29; 1 Yohana 2:2**) Kwa kuwa kifo ndiyo adhabu au mshahara wa dhambi, dhambi inapoondolewa mshahara huo lazima ukome kwa wakati ufaao. Mtazamo mwingine wowote ungekuwa usio na mantiki na usio wa haki.

Ukweli ni kwamba bado hakuna urejesho kamili kutoka katika **hasara ya Adamu** uliokamilishwa, ingawa karibu miaka elfu mbili imepita tangu Bwana wetu alipokufa, si hoja ya kupinga mpango wa **urejesho**. Hii ni sawa na kusema kuwa miaka elfu nne iliyopita kabla ya kifo chake ni uthibitisho kwamba Mungu hakuwa amepanga **ukombozi** kabla ya kuwekwa **misingi ya ulimwengu**.Zile nyakati zote mbili—yaani miaka elfu mbili tangu kifo cha Kristo na ile miaka elfu nne kabla ya kifo chake—zilikuwa ni **nyakati zilizowekwa** kwa ajili ya sehemu nyingine za kazi, kama maandalizi kuelekea **"nyakati za urejesho wa vitu vyote."**

Imani na Matendo Bado ni vya Lazima

Mtu yeyote asidhani kwa haraka kwamba katika mtazamo huu kuna chochote kinachopingana na fundisho la Maandiko kwamba imani kwa Mungu, toba kwa ajili ya dhambi na matengenezo ya tabia ni vya lazima kwa ajili ya wokovu. Suala hili litashughulikiwa kwa urefu zaidi baadaye, lakini sasa tunadokeza kwamba ni wachache tu ndio wamewahi kuwa na nuru ya kutosha kuleta imani kamili, toba na matengenezo. Wengine wamepofushwa kwa sehemu, na wengine kabisa, na mungu wa dunia hii, nao ni lazima waponywe upofu na pia mauti, ili wao, **kila mmoja kwa ajili yake mwenyewe**, waweze kupata nafasi **kamili** ya kuthibitisha, kwa utii au uasi, ustahili wao au

kutostahili kwao uzima wa milele. Kisha wale watakaojithibitisha kuwa hawastahili uzima watakufa tena—mauti ya pili—ambayo hakutakuwa na ukombozi kutoka kwayo, na hivyo hakutakuwa na ufufuo. Kifo kinachokuja kwa sababu ya dhambi ya Adamu, na kutokamilika kote kunakofuata, vitaondolewa kwa sababu ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu; lakini kifo kinachokuja kama matokeo ya uasi wa mtu binafsi, wa makusudi, ni cha mwisho. Dhambi hii haina msamaha kamwe, na adhabu yake, mauti ya pili, itakuwa ya **milele**—si kufa kwa milele, bali mauti ya milele—mauti isiyovunjwa na ufufuo.

Mshahara wa Dhambi ya Makusudi ni wa Hakika

Falsafa ya mpango wa ukombozi itashughulikiwa katika kitabu kijacho. Hapa tunaweka tu msingi wa ukweli kwamba ukombozi kupitia Kristo Yesu utakuwa na matokeo na fursa zenye kuenea mbali kama vile dhambi ya Adamu ilivyokuwa katika uharibifu na maangamizi yake—kwamba wote waliohukumiwa na kuteseka kwa sababu ya yule mmoja wanaweza kwa hakika, "*kwa wakati ufaao*," kuwekwa huru kutoka katika maovu yote hayo kwa sababu ya yule mwingine. Hata hivyo, hakuna anayeweza kuielewa hoja hii ya Kimaandiko asiyekubali kauli ya Maandiko kwamba mauti—yaani, kutoweka kwa uhai—**ndio mshahara wa dhambi**. Wale wanaofikiri kifo ni uzima katika mateso si tu kwamba wanapuuza maana ya maneno **mauti** na **uzima**, ambayo yanapingana, bali pia wanajiingiza katika upuuzi mara mbili. Ni upuuzi kudhani kwamba Mungu angeendeleza uwepo wa Adamu milele katika mateso kwa aina yoyote ya dhambi aliyoweza kuitenda, lakini hasa kwa kosa dogo la kula tunda lililokatazwa. Tena, ikiwa Bwana wetu Yesu aliwakomboa wanadamu, akafa badala yetu, akawa fidia yetu, akaingia katika mauti ili tuwekwe huru kutoka humo, je, si dhahiri kwamba mauti aliyokufa kwa ajili ya wasio haki yalikuwa ya aina ileile kama yale ambayo wanadamu wote walihukumiwa? Je, basi, anateseka mateso ya milele kwa ajili ya dhambi zetu?

Ikiwa sivyo, basi kwa hakika kama alivyokufa kwa ajili ya dhambi zetu, adhabu ya dhambi zetu ilikuwa ni mauti, na si uzima kwa maana au hali yoyote.

Lakini, cha ajabu, wakiona kwamba nadharia ya mateso ya milele haipatani na kauli kwamba *"Bwana ameweka juu yake uovu wetu sote,"* na kwamba Kristo *"alikufa kwa ajili ya dhambi zetu,"* na wakiona kwamba mojawapo ni lazima liachwe kwa kuwa halipatani, wengine wameshikilia wazo la mateso ya milele kiasi kwamba wanalishikilia kama tonge tamu, bila kujali Maandiko, na kwa makusudi wanakana kwamba Yesu alilipa bei ya fidia ya ulimwengu, ingawa ukweli huu unafundishwa katika kila ukurasa wa Biblia.

Je, Kutakuwa na Nafasi Duniani kwa Ajili ya Mamilioni Watakaofufuliwa?

Je, Urejesho Unawezekana?

Wengine wamedhania kwamba kama mabilioni ya wafu wangefufuliwa, kusingekuwa na nafasi kwa ajili yao duniani; na kwamba hata kama kungekuwa na nafasi, dunia isingeweza kuhimili idadi kubwa kiasi hicho ya watu. Wengine hata wanadai kwamba dunia ni kaburi moja kubwa, na kwamba kama wafu wote wangeamshwa, wangekanyagana kwa kukosa nafasi.

Hii ni hoja muhimu. Ingekuwa ajabu kama tungegundua kwamba ingawa Biblia inatangaza ufufuo kwa watu wote, bado, kwa vipimo halisi, wasingeweza kupata hata mahali pa kuweka mguu duniani! Sasa hebu tuone: fanya hesabu na utagundua hii ni hofu isiyo na msingi. Utagundua kwamba kuna nafasi tele kwa ajili ya "urejesho wa vitu vyote," kama "Mungu alivyonena kwa vinywa vya manabii wake wote watakatifu."

Tuchukulie kwamba imepita miaka elfu sita tangu kuumbwa kwa mwanadamu, na kwamba kuna watu Bilioni moja , milioni mianne (1,400,000,000) wanaoishi duniani sasa. Jamii yetu ilianza na watu wawili, lakini hebu tufanye makadirio ya ukarimu sana

na tuchukulie kwamba kulikuwa na watu wengi mwanzoni kama walivyo sasa; na, zaidi ya hayo, kwamba kamwe hakukuwa na idadi ndogo kuliko hiyo wakati wowote, ingawa kwa kweli gharika ilipunguza idadi ya watu hadi watu wanane. Tena, tuwe wakarimu, na tukadirie vizazi vitatu kwa kila karne, au miaka thelathini na tatu kwa kila kizazi, ingawa, kulingana na Mwanzo 5, kulikuwa na vizazi kumi na kimoja tu kutoka Adamu hadi gharika, kipindi cha miaka elfu moja mia sita hamsini na sita, au takriban miaka mia moja hamsini kwa kila kizazi. Sasa hebu tuone: miaka elfu sita ni karne sitini; vizazi vitatu kwa kila karne vitatupa vizazi mia moja themanini tangu Adamu; na watu milioni elfu moja mia nne kwa kila kizazi vitatupa jumla ya watu bilioni mia mbili hamsini na mbili (252,000,000,000) kama idadi kamili ya jamii yetu tangu uumbaji hadi sasa, kulingana na makadirio haya ya ukarimu, ambayo pengine ni zaidi ya mara mbili ya idadi halisi.

Tutapata wapi nafasi ya kutosha kwa umati huu mkubwa? Hebu tuipime ardhi, tuone. Jimbo la Texas, nchini Marekani, lina eneo la maili za mraba laki mbili thelathini na saba elfu (237,000). Kuna futi za mraba milioni ishirini na saba, mia nane sabini na nane, mia nne (27,878,400) katika maili moja, na, kwa hiyo, kuna futi za mraba trilioni sita, bilioni mia sita na saba, milioni mia moja themanini, na mia nane elfu (6,607,180,800,000) katika jimbo la Texas. Tukiruhusu futi za mraba kumi kama eneo linalofunikwa na kila mwili wa marehemu, tunaona kwamba Texas, kama makaburi, kwa kiwango hiki ingeweza kuhifadhi miili bilioni mia sita sitini, milioni mia saba kumi na nane, na elfu themanini (660,718,080,000), au karibu mara tatu ya makadirio yetu yaliyotiwa chumvi ya idadi ya watu waliowahi kuishi duniani.

Mtu aliyesimama anachukua takriban futi za mraba moja na theluthi mbili za nafasi. Kwa kiwango hiki idadi ya sasa ya watu duniani (watu bilioni moja na milioni mia nne) wangeweza kusimama katika eneo la maili za mraba themanini na sita—eneo dogo sana kuliko la jiji la London au Philadelphia. Na kisiwa cha

Ireland (eneo, maili za mraba elfu thelathini na mbili) kingetoa nafasi ya kusimama kwa zaidi ya mara mbili ya idadi ya watu waliowahi kuishi duniani, hata kwa makadirio yetu yaliyotiwa chumvi.

Basi, hakuna ugumu sana katika kujibu pingamizi hili. Na tunapokumbuka unabii wa Isaya (**35:1-6**), kwamba nchi itatoa mazao yake; kwamba jangwa litafurahi na kuchanua kama waridi; kwamba katika nyika maji yatabubujika, na vijito jangwani, tunaona kwamba Mungu anaonyesha kuwa ameona mbele mahitaji yote ya mpango wake, na ataandaa kwa wingi mahitaji ya viumbe vyake kwa njia itakayoonekana kuwa ya asili sana.

Urejesho Dhidi ya Mageuzi(Evolution)

Wengine wanaweza kupinga kwamba ushuhuda wa Maandiko kuhusu urejesho wa mwanadamu kwenye hali ya zamani haupatani na mafundisho ya sayansi na falsafa, ambayo, kwa sababu inayoonekana kuwa ya kweli, yanatuelekeza kwenye akili bora zaidi ya karne hii ya ishirini, na kudai huu ni ushahidi wa mwisho kwamba mwanadamu wa asili ni lazima awe alikuwa na upungufu mkubwa wa akili, ambayo wanadai ni matokeo ya maendeleo (**mageuzi**). Kutoka kwa mtazamo huu, urejesho kwenye hali ya zamani ungekuwa jambo lisilotamanika kabisa, na hakika ungekuwa kinyume cha baraka.

Kwa mtazamo wa kwanza, hoja kama hiyo inaonekana kuwa ya kweli, na wengi wanaonekana kuwa na mwelekeo wa kuikubali kama ukweli bila uchunguzi wa makini, wakisema, kama mhubiri mmoja maarufu wa Brooklyn,

> *"Kama Adamu alianguka, basi anguko lake lilikuwa la kwenda juu, na kadiri tunavyoanguka zaidi na kwa kasi kutoka katika hali yake ya asili ndivyo inavyokuwa bora kwetu na kwa wote wanaohusika."*

Hivyo, falsafa, hata ikiwa madhabahuni, inalifanya Neno la Mungu liwe batili, na ikifaa, kutushawishi kwamba mitume walikuwa wapumbavu walipotangaza kwamba kifo na kila taabu vilikuja kwa uasi wa mtu wa kwanza, na kwamba haya

yangeweza kuondolewa na mwanadamu kurejeshwa kwenye upendeleo wa kimungu na uzima kwa njia ya fidia pekee. (**Warumi 5:10, 12, 17-19, 21; 8:19-22; Matendo 3:19-21; Ufunuo 21:3-5**) Lakini tusihitimishe kwa haraka kwamba falsafa hii haiwezi kushindwa; kwa maana kama tungelazimika kuyatupilia mbali mafundisho ya mitume kuhusu asili ya dhambi na mauti, na ya urejesho kwenye ukamilifu wa asili, tunapaswa, kwa uaminifu, kuukataa ushuhuda wao kabisa na juu ya kila somo, kama usioongozwa na roho na hivyo usiokuwa na uzito maalum au mamlaka. Basi, kwa kuzingatia ukweli, hebu tuchunguze kwa ufupi mtazamo huu unaozidi kuwa maarufu na tuone jinsi falsafa yake ilivyo ya kina.

Anasema mtetezi na mwakilishi wa nadharia hii:

> *"Mwanzoni, mwanadamu alikuwa katika hatua ya maisha ambapo **asili yake ya mwili** ilitawala, na mwili pekee ndio uliokuwa ukimuongoza. Kisha, akakua polepole kutoka hali moja hadi nyingine mpaka sasa, ambapo mwanadamu wa kawaida amefikia hali ambayo tunaweza kusema anaanza kuongozwa na akili. Hivyo basi, kipindi hiki kinaweza kuchukuliwa na kuitwa **Enzi ya Akili**. Akili ndiyo inayosukuma shughuli kuu za siku hizi. Akili inashika hatamu za serikali; na vitu vya asili kama ardhi, hewa na maji vinawekwa chini ya utawala wake. Mwanadamu anaanza kudhibiti nguvu zote za asili, na polepole lakini kwa hakika anapata uwezo juu ya ulimwengu wa asili. Uwezo huu unatoa ushahidi kwamba mwishowe ataweza kusema, kwa maneno ya Alexander Selkirk, "Mimi ni mfalme wa kila kitu ninachokiona."*

Ukweli ni kwamba nadharia inaonekana kuwa na mantiki kwa mtazamo wa kwanza haupaswi kutuongoza kuikubali kwa haraka, na kujaribu kuipotosha Biblia ili ipatane nayo. Kwa njia elfu moja tumeithibitisha Biblia, na tunajua bila shaka yoyote kwamba ina hekima ipitayo ya kibinadamu inayofanya kauli zake zisiwe na makosa. Tunapaswa kukumbuka, pia, kwamba ingawa utafiti wa kisayansi unapaswa kupongezwa, na mapendekezo yake kuzingatiwa, bado hitimisho zake si kamilifu hata kidogo. Na ni ajabu gani kwamba imethibitisha nadharia zake kuwa za uongo mara elfu moja, tunapokumbuka kwamba

mwanasayansi wa kweli ni mwanafunzi tu anayejaribu, chini ya hali nyingi zisizofaa, na akipambana na matatizo karibu yasiyoweza kushindwa, kujifunza kutoka katika Kitabu kikuu cha Maumbile historia na hatima ya mwanadamu na makao yake.

Basi, hatutaki kupinga wala kuzuia uchunguzi wa kisayansi; lakini katika kusikia mapendekezo kutoka kwa wanafunzi wa Kitabu cha Maumbile, hebu tulinganishe kwa makini makisio yao, ambayo mara nyingi yamethibitika kuwa na makosa kwa sehemu au kabisa, na Kitabu cha Ufunuo wa Mungu, na kuthibitisha au kukanusha mafundisho ya wanasayansi kwa *"sheria na ushuhuda. Kama hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwao hamna asubuhi."* (**Isaya 8:20**) Ujuzi sahihi wa vitabu vyote viwili utathibitisha kuwa vinapatana; lakini hadi tuwe na ujuzi huo, Ufunuo wa Mungu lazima uwe na kipaumbele, na lazima uwe kiwango miongoni mwa watoto wa Mungu, ambacho kwa hicho matokeo yanayodhaniwa ya wanadamu wenzetu wenye kukosea yatahukumiwa.

Lakini tukiwa tunashikilia kanuni hii, hebu tuone kama hakuna suluhisho lingine la kimantiki la kuongezeka kwa maarifa, ujuzi na nguvu za mwanadamu isipokuwa nadharia ya Mageuzi—kwamba ingawa mwanadamu mwanzoni alitokana na kiumbe wa daraja la chini sana, sasa amefikia Zama za Ubora au "Zama za Ubongo." Labda mwishowe tutagundua kwamba uvumbuzi na huduma za kisasa, elimu ya jumla na usambazaji mpana na ongezeko la maarifa, havitokani na uwezo mkubwa zaidi wa ubongo, bali na mazingira mazuri zaidi ya kutumia akili. Kwamba uwezo wa ubongo leo ni mkubwa kuliko katika zama zilizopita, **tukataa**; huku tukikubali kwa hiari kwamba, kutokana na mazingira yenye faida, matumizi ya uwezo wa akili walio nao watu leo ni ya jumla zaidi kuliko wakati mwingine wowote uliopita, na hivyo huleta maonyesho makubwa zaidi. Katika masomo ya uchoraji na uchongaji, je, wanafunzi wa "Zama hizi za Ubongo" hawawarudii mabingwa wakuu wa zamani? Je, kwa kufanya hivyo hawakubali kuwepo kwa nguvu ya akili na

ubunifu wa asili pamoja na ustadi wa kazi unaostahili kuigwa? Je, "Zama hizi za Ubongo" za sasa hazitegemei kwa kiasi kikubwa miundo ya asili ya zama zilizopita kwa ajili ya usanifu wake wa majengo? Je, wasemaji na wataalamu wa mantiki wa "Zama hizi za Ubongo" hawajifunzi na kuiga mbinu na mihutasari ya kimantiki ya Plato, Aristotle, Demosthenes na wengine wa zamani? Je, wazungumzaji wengi wa umma wa leo wasingetamani kuwa na ulimi wa Demosthenes au Apolo, na zaidi sana uwezo wa wazi wa kufikiri wa Mtume Paulo?

Tukirudi nyuma zaidi: ingawa tunaweza kurejelea uwezo wa kuhutubia wa manabii kadhaa, na picha tukufu za kishairi zilizotawanyika katika Zaburi, tunawaelekeza wanafalsafa hawa wa "Zama za Ubongo" kwenye hekima na mantiki, na vilevile kwenye hisia nzuri za kiadili, za Ayubu na wafariji wake. Na tuseme nini kuhusu Musa, *"aliyekuwa amesoma hekima yote ya Wamisri"*? Sheria zilizotolewa kupitia yeye zimekuwa msingi wa sheria za mataifa yote yaliyostaarabika, na bado zinatambuliwa kama mfano halisi wa hekima ya ajabu. Kufukuliwa kwa miji ya kale iliyozikwa kunafunua maarifa ya sanaa na sayansi katika zama zilizopita ambayo yanawashangaza baadhi ya wanafalsafa wa hii inayoitwa "Zama za Ubongo." Mbinu za kale za kutia maiti dawa isioze, kulainisha shaba, kutengeneza kioo nyumbufu na chuma cha Dameski, ni miongoni mwa mafanikio ya zamani za kale ambayo ubongo wa zama za sasa, pamoja na faida zake zote, hauwezi kuyaelewa wala kuyaiga.

Tukirudi nyuma miaka elfu nne hadi wakati wa Ibrahimu, tunakuta Piramidi Kuu la Misri—kitu cha ajabu na cha kustaajabisha kwa wanasayansi wasomi zaidi wa leo. Ujenzi wake unapatana kikamilifu na mafanikio ya juu zaidi ya "Zama hizi za Ubongo" katika sayansi ya Hisabati na Astronomia. Linafundisha, kwa uhakika, kweli ambazo leo zinaweza tu kukadiriwa kwa kutumia vyombo vya kisasa. Mafundisho yake ni ya wazi na ya kuvutia kiasi kwamba baadhi ya wanaastronomia wakuu duniani wamelitamka bila kusita kuwa ni la asili ya

kimungu. Na hata kama wanamageuzi wa "Zama zetu za Ubongo" wangekubali kwamba lina mpangilio wa kimungu, na kwamba hekima yake inapita ya kibinadamu, bado lazima wakubali kwamba ni la ujenzi wa kibinadamu. Na ukweli kwamba katika siku hizo za kale kundi lolote la watu lilikuwa na uwezo wa kiakili wa kutekeleza mpangilio wa kimungu kama huo ambao ni watu wachache sana leo wangeweza kuufanya wakiwa na kielelezo mbele yao, na wakiwa na vifaa vyote vya kisasa vya kisayansi, unathibitisha kwamba "Zama zetu za Ubongo" zinakuza majivuno zaidi kuliko hali halisi na ukweli unavyoruhusu.

Ikiwa, basi, tumethibitisha kwamba uwezo wa kiakili wa leo si mkubwa kuliko wa zama zilizopita, na pengine ni mdogo, tutaelezeaje ongezeko la maarifa ya jumla, uvumbuzi wa kisasa, n.k.? Tunaamini tutaweza kuonyesha hili kwa mantiki na kwa kupatana na Maandiko. Uvumbuzi na ugunduzi ambao sasa unathibitika kuwa wa thamani kubwa, na unaochukuliwa kuwa uthibitisho kwamba hizi ni "Zama za Ubongo," kwa kweli ni vya kisasa sana—karibu vyote vimekuja ndani ya karne iliyopita, na miongoni mwa muhimu zaidi ni vile vya miaka sitini iliyopita; kwa mfano, matumizi ya mvuke na umeme—katika telegrafu, reli na meli za mvuke, na katika mitambo ya viwanda mbalimbali. Ikiwa, basi, hizi ni dalili za kuongezeka kwa nguvu za ubongo, "Zama za Ubongo" lazima ziwe ndio zinaanza, na hitimisho la kimantiki ni kwamba karne nyingine itashuhudia kila aina ya miujiza kama tukio la kila siku; na kwa kiwango hicho cha ongezeko, ingeishia wapi?

Lakini hebu tuangalie tena: Je, watu wote ni wavumbuzi? Ni wachache mno ambao uvumbuzi wao ni wa manufaa na wa vitendo, ukilinganisha na idadi ya watu wanaothamini na kutumia uvumbuzi wanapowekewa mkononi! Wala hatusemi kwa dharau kuhusu kundi hilo muhimu na linaloheshimiwa sana la watumishi wa umma tunaposema kwamba idadi ndogo kati yao ni watu wenye nguvu kubwa za ubongo. Baadhi ya watu wenye

akili zaidi duniani, na wenye uwezo mkubwa wa kufikiri, si wavumbuzi wa mitambo. Na baadhi ya wavumbuzi ni wazito kiakili kiasi kwamba wote hushangaa jinsi walivyojikwaa kwenye ugunduzi walioufanya. Kanuni kuu (umeme, nguvu ya mvuke, n.k.), ambazo watu wengi kwa miaka mingi huzifanyia kazi, kuzitumia na kuziboresha, mara kwa mara, kwa ujumla ziligunduliwa kwa kile kinachoonekana kuwa ni ajali tupu, bila matumizi ya nguvu kubwa za ubongo, na bila kutafutwa sana.

Kwa mtazamo wa kibinadamu tunaweza kuelezea uvumbuzi wa sasa hivi: Uvumbuzi wa uchapishaji, mnamo mwaka 1440 BK, unaweza kuchukuliwa kuwa ndio mwanzo. Pamoja na uchapishaji wa vitabu, kulikuja na kumbukumbu za mawazo na ugunduzi wa watu wenye kufikiri na wachunguzi, ambazo, bila uvumbuzi huu, zisingewahi kujulikana kwa waliowafuata. Pamoja na vitabu, kulikuja na elimu ya jumla zaidi na, hatimaye, shule za kawaida. Shule na vyuo vikuu haviongezi uwezo wa kibinadamu, lakini vinafanya mazoezi ya akili yawe ya kawaida zaidi, na hivyo kusaidia kukuza uwezo ambao tayari upo. Kadiri maarifa yanavyozidi kuenea na vitabu kuwa vingi, vizazi vinavyomiliki vitu hivi vina faida iliyo dhahiri kuliko vizazi vya awali; si tu kwa sababu sasa kuna wafikiriaji elfu moja kwa kila mmoja wa zamani, wa kunoana na kuchocheana kwa mapendekezo, bali pia kwa sababu kila kizazi cha baadaye, kupitia vitabu, kinamiliki uzoefu uliojumuishwa wa wakati uliopita pamoja na ule wa kwake mwenyewe. Elimu na shauku inayostahili sifa inayoambatana nayo, uthubutu wa kazi, na hamu ya kupata sifa na mafanikio, vikisaidiwa na kumbukumbu na maelezo ya uvumbuzi katika magazeti ya kila siku, vimechochea na kutia nuru nguvu za utambuzi za mwanadamu, na kumfanya kila mmoja awe macho kugundua au kuvumbua, ikiwezekana, kitu fulani kwa ajili ya wema na ustawi wa jamii. Hivyo, tunapendekeza kwamba uvumbuzi wa kisasa, ukitazamwa kwa mtazamo wa kibinadamu pekee, haufundishi kuwepo kwa ongezeko la uwezo wa ubongo, bali utambuzi ulionolewa kutokana na sababu za kiasili

Na sasa tunakuja kwenye Maandiko kuona yanachofundisha juu ya somo hili; kwa maana ingawa tunaamini, kama ilivyopendekezwa hapo juu, kwamba uvumbuzi na ongezeko la maarifa, n.k., miongoni mwa wanadamu ni matokeo ya sababu za **asili**, bado tunaamini kwamba sababu hizi zote za asili zilipangwa na kuamriwa na Yehova Mungu zamani, na kwamba kwa wakati ufaao zimetimia—kwa majaliwa yake yanayoongoza, ambavyo kwayo *"hutenda vitu vyote kwa shauri la mapenzi yake."* (**Waefeso 1:11**) Kulingana na mpango uliofunuliwa katika Neno lake, Mungu alikusudia kuruhusu dhambi na taabu vitawale isivyo haki na kuukandamiza ulimwengu kwa miaka elfu sita, na kisha katika milenia ya saba kurejesha vitu vyote, na kuung'oa uovu—kuuuharibu na matokeo yake kupitia Yesu Kristo, ambaye alimchagua tangu zamani kufanya kazi hii. Kwa hiyo, miaka elfu sita ya utawala wa uovu ilipoanza kukaribia mwisho, Mungu aliruhusu mazingira yapendelee ugunduzi, katika kujifunza Kitabu chake cha Ufunuo na Kitabu chake cha Maumbile(asili), na pia katika maandalizi ya vifaa vya kimakanika na kikemia vyenye manufaa katika kubariki na kuinua wanadamu wakati wa Zama za Milenia, zinazokaribia kuanzishwa sasa.

> *Kwamba huu ulikuwa mpango wa Mungu inaonyeshwa wazi na kauli ya kinabii: "Lakini wewe, Danielii, yafunge maneno haya, ukakitie muhuri kitabu, hata **wakati wa mwisho**; [ndipo] wengi wataenda mbio huko na huko, na **MAARIFA** [si uwezo] yataongezeka," "wala wabaya hawataelewa [mpango na njia ya Mungu]; bali walio na hekima ndio watakaoelewa"; "na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwako tangu lilipoanza kuwako taifa hata wakati uo huo."* **—Danieli 12:1, 4, 10**

Kwa wengine inaweza kuonekana ajabu kwamba Mungu hakupanga ili uvumbuzi na baraka za sasa zimfikie mwanadamu mapema zaidi ili kupunguza laana. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba mpango wa Mungu umekuwa ni kuwapa wanadamu uthamini kamili wa laana, ili baraka itakapowajia wote wawe wameamua milele juu ya kutokuwa na faida kwa dhambi. Zaidi ya hayo, Mungu aliona mbele na ametabiri kile ambacho ulimwengu bado haujakitambua, yaani, kwamba baraka zake bora

kabisa zingeongoza na kuzaa maovu makubwa zaidi kama zingetolewa kwa wale ambao mioyo yao haipatani na sheria za haki za ulimwengu. Mwishowe itaonekana kwamba kuruhusu kwa Mungu kwa sasa ongezeko la baraka ni somo la vitendo juu ya jambo hili, ambalo linaweza kutumika kama mfano wa kanuni hii kwa milele yote—kwa malaika na pia kwa wanadamu watakaorejeshwa. Jinsi hili linavyoweza kuwa, tunadokeza tu:

Kwanza: Maadamu wanadamu wapo katika hali yao ya sasa ya anguko na upotovu, ni wazi kwamba bila sheria imara na serikali yenye nguvu ya kusimamia, tamaa za ubinafsi zitaendelea kuwa na nguvu juu ya watu wengi. Tukizingatia pia tofauti za uwezo alizonazo kila mtu, matokeo ya uvumbuzi wa mashine za kurahisisha kazi hayawezi kuwa tofauti: mwishowe matajiri watazidi kuwa matajiri, na maskini watazidi kuwa maskini. Hii ni kwa sababu mwelekeo wa sasa unaelekea kwenye **mfumo wa biashara ya wachache** na watu kujilimbikizia mali, jambo ambalo linawapa faida zaidi wale ambao tangu mwanzo walikuwa na uwezo na fursa nzuri.

Pili: Hata kama ingewezekana kutunga sheria ya kugawanya utajiri uliopo na ongezeko lake la kila siku kwa usawa kwa watu wote—jambo ambalo haliwezekani—bado, bila mwanadamu kuwa mkamilifu au kuwepo kwa serikali isiyo ya kibinadamu inayosimamia mambo, matokeo yake yangekuwa mabaya zaidi kuliko hali ya sasa. Kama faida za mashine zinazorahisisha kazi na vifaa vyote vya kisasa zingegawanywa kwa usawa, punde si punde matokeo yake yangekuwa ni kupungua sana kwa saa za kazi na kuongezeka sana kwa muda wa mapumziko.

Ukosefu wa shughuli za kufanya ni jambo lenye madhara makubwa kwa wanadamu walioanguka dhambini. Kama isingekuwa lazima kwa mwanadamu kufanya kazi na kutoka jasho, uharibifu wa jamii ya wanadamu ungekuwa wa haraka zaidi. *Uzembe ni mama wa maovu;* na ni hakika kwamba uharibifu wa akili, maadili na mwili ungefuata. Hapa ndipo tunaona hekima na wema wa Mungu kwa kuzuia baraka hizi mpaka wakati ufaao

ulipofika, ili ziwe kama maandalizi ya Utawala wa Milenia wa baraka. Chini ya usimamizi wa serikali isiyo ya kibinadamu ya Ufalme wa Mungu, si tu kwamba baraka zote zitagawanywa kwa usawa, bali hata ule muda wa mapumziko utapangwa na kuongozwa na serikali hiyo ili matokeo yake yawe ni kuleta fadhila njema na kuelekeza watu kwenye ukamilifu wa akili, maadili na mwili. Kuongezeka kwa uvumbuzi na baraka nyingine za maarifa kinachotokea sasa katika hii "siku ya maandalizi" kumeruhusiwa kuja kwa njia inayoonekana ya kawaida kiasi kwamba watu wanajisifu kuwa ni kwa sababu hii ni "Enzi ya Akili." Lakini, kwa kiasi kikubwa, matokeo ya mambo haya yataruhusiwa kuwa tofauti sana na matarajio ya wanafalsafa hawa wenye hekima, na bila shaka yatawavunja moyo. Ni ongezeko hili la baraka hizi ambalo tayari linaanza kuuletea ulimwengu wakati wa taabu, ambao utakuwa wa namna ambayo haijawahi kutokea tangu lilipokuwapo taifa.

Nabii Danieli, kama alivyonukuliwa hapo juu, anaunganisha pamoja ongezeko la maarifa na wakati wa taabu. Maarifa husababisha taabu, kwa sababu ya upotovu wa jamii ya wanadamu. Ongezeko la maarifa halijaipa tu ulimwengu mashine na huduma za ajabu za kuokoa nguvu kazi, bali pia limepelekea ongezeko la ustadi wa kitabibu ambapo maelfu ya maisha yanarefushwa, na limewaangazia wanadamu kiasi kwamba uchinjaji wa binadamu, yaani vita, unapungua umaarufu, na hivyo, maelfu wengine pia wanaepushwa ili waongeze zaidi jamii ya wanadamu, ambayo inaongezeka kwa kasi zaidi leo, pengine, kuliko kipindi kingine chochote cha historia.

Hivyo, wakati wanadamu wanapoongezeka kwa kasi, uhitaji wa nguvu zao za kazi unazidi kupungua kulingana na hilo; na wanafalsafa wa 'Zama za Akili' wana tatizo mbele yao la jinsi ya kutoa ajira na riziki kwa tabaka hili kubwa na linaloongezeka kwa kasi, ambalo huduma zake, zikiwa kwa sehemu kubwa zimechukuliwa na mashine, zinaweza kuachwa, lakini ambalo mahitaji na matakwa yake hayana mipaka. Lazima wanafalsafa

hawa wakiri mwishowe kwamba, suluhisho la tatizo hili liko nje ya uwezo wa akili zao..

Ubinafsi utaendelea kuwatawala matajiri, ambao wanashikilia nguvu na fursa, na utawapofusha wasione mantiki na haki; wakati ubinafsi kama huo, ukichanganyika na silika ya **kujihifadhi** na ujuzi ulioongezeka wa haki zao, utawapa ujasiri wengine na kuwawasha wengine moto miongoni mwa matabaka ya maskini, na matokeo ya **baraka** hizi, kwa muda, yatakuwa ya kutisha—wakati wa taabu, kweli, ambao haujawahi kutokea tangu lilipoanza kuwako taifa—na hii, ni kwa sababu mwanadamu katika hali ya upotovu hawezi kutumia vizuri baraka hizi bila kuongozwa na kusimamiwa. Hadi utawala wa Milenia utakapokuwa umeiandika upya sheria ya Mungu katika moyo wa mwanadamu uliorejeshwa ndipo watu watakapokuwa na uwezo wa kutumia uhuru kamili bila madhara au hatari.

Siku ya taabu itaisha kwa wakati ufaao, wakati yeye aliyesema na Bahari ya Galilaya iliyochafuka, vivyo hivyo, kwa mamlaka, ataamuru bahari inayochafuka ya tamaa za kibinadamu, akisema, "*Nyamaza! Utulie*!" Mfalme wa Amani "atakaposimama" katika mamlaka, utulivu mkuu utakuwa ndio matokeo. Ndipo elementi zinazochafuka na kugongana zitatambua mamlaka ya "Masihi wa Yehova," *"na utukufu wa Bwana utafunuliwa, na wote wenye mwili watauona pamoja"*; na katika utawala wa Kristo utakaoanza hivyo *"jamaa zote za dunia zitabarikiwa."*

Ndipo watu wataona kwamba kile walichokihusisha na mageuzi au maendeleo ya asili na ujanja wa "Zama za Ubongo" kilikuwa, badala yake, ni *"umeme wa Yehova"* (**Zaburi 77:18**) katika "siku ya maandalizi yake" kwa ajili ya kubarikiwa kwa wanadamu.

Lakini kwa sasa ni watakatifu pekee wanaoweza kuona, na ni wenye hekima ya kimbingu pekee wanaoweza kuelewa hili; kwa maana *"Siri ya Bwana iko kwao wamchao; Naye atawajulisha agano lake."* (**Zaburi 25:14**) Shukrani ziwe kwa Mungu, kwamba ingawa maarifa ya jumla yameongezeka, amepanga pia kwamba

watoto wake hawahitaji *"kupuuzwa na kutokuwa na matunda katika kumjua Bwana"* na katika kuthamini mipango yake. Na kwa uthamini huu wa Neno na mipango yake tunawezeshwa kutambua na kupinga falsafa za ubatili na mapokeo ya upumbavu ya wanadamu yanayopingana na Neno la Mungu.

Simulizi ya Biblia kuhusu uumbaji wa mwanadamu ni kwamba Mungu alimwumba akiwa mkamilifu na mnyoofu, sura yake ya kidunia; lakini mwanadamu alijitafutia mbinu nyingi na kujichafua mwenyewe. (**Mwanzo 1:27; Warumi 5:12; Mhubiri 7:29**) Kwa kuwa wote walikuwa wenye dhambi, jamii ya wanadamu haikuweza kujisaidia, na hakuna yeyote aliyeweza kwa njia yoyote kumkomboa ndugu yake au kumpa Mungu fidia kwa ajili yake. (**Zaburi 49:7, 15**) kwamba Mungu katika huruma na upendo alikuwa amefanya mpango kwa ajili ya hili; kwamba, kutokana na hayo, Mwana wa Mungu alifanyika mwanadamu, na kutoa bei ya fidia ya mwanadamu; kwamba, kama thawabu kwa dhabihu hii, na ili kukamilisha ile kazi kuu ya upatanisho, alikwezwa sana, hata kufikia asili ya uungu; na kwamba kwa wakati wake atatimiza urejesho wa jamii hiyo kwenye ukamilifu wa awali na kwenye kila baraka iliyomilikiwa wakati huo.

Mambo haya yanafundishwa waziwazi katika Maandiko, tangu mwanzo hadi mwisho, na yako katika upinzani wa moja kwa moja na nadharia ya Mageuzi; au, tuseme, hayo 'maneno matupu ya sayansi, iitwayo hivyo kwa uongo,' yako katika mgongano mkali na usiopatanishika na Neno la Mungu.

"Bado mawingu ya ghadhabu yanatanda angani mwa dunia, Na kisasi cha Mungu chaning'inia kizito juu ya nafsi yake; Lakini atainuka—japo kwanza arudiwe na Mungu— Kisha abatizwe katika utukufu na uzuri.

"Naam, Dunia, utainuka; msaada wa Baba yako Utaponya jeraha ambalo mkono wake wa kurudi ulilifanya; Utahukumu utawala katili wa dhalimu mwenye kiburi, Na kuvunja pingu zake, na kutupa kamba zake mbali.

"Ndipo kwenye udongo wako uoto usiosinyaa utachipuka; Paazeni sauti, enyi milima, na enyi mabonde, imbeni! Miamba yenu yenye kiu haitakunja tena uso kwa huzuni, Kuwa dhihaka ya asiyeamini, na zarau ya wapagani.

"Mchanga wa joto kali utatoa mavuno mara kumi, Na Edeni mpya itapamba shamba la miiba. Hata sasa tunaona, ikipunga kwa upana juu ya nchi, Malaika mwenye nguvu akiinua fimbo yake ya dhahabu,

"Akaribisha maono angavu ya nguvu inayoshuka, Ahesabu kila lango na kupima kila mnara; Na kukemea mihuri inayochelewa ambayo bado inazuia Simba wako, Yuda, asianze utawala wake uliokusudiwa."

– Heber

SOMO LA X

ASILI ZA KIROHO NA ZA KIBINADAMU ZIMETENGANISHWA NA NI TOFAUTI

DHANA POTOFU ZA KAWAIDA—ASILI ZA KIDUNIA AU KIBINADAMU NA ZA MBINGUNI AU KIROHO—UTUKUFU WA KIDUNIA NA UTUKUFU WA MBINGUNI—USHUHUDA WA BIBLIA KUHUSU VIUMBE WA ROHO—HALI YA KUFA NA HALI YA KUTOKUFA—JE, VIUMBE WENYE HALI YA KUFA WANAWEZA KUWA NA UZIMA WA MILELE?—HAKI KATIKA UTOAJI WA HISANI—KANUNI INAYODHANIWA YACHUNGUZWA—AINA MBALIMBALI KATIKA UKAMILIFU—HAKI ZA ENZI KUU YA MUNGU—MAANDALIZI YA MUNGU KWA MWANADAMU NI FUNGU LA KURIDHISHA—UCHAGUZI WA MWILI WA KRISTO—JINSI MABADILIKO YA ASILI YAO YANAVYOFANYIKA.

KUSHINDWA kuona kwamba mpango wa Mungu kwa wanadamu kwa ujumla unakusudia urejesho kwenye hali yao ya zamani—ukamilifu wa kibinadamu uliopotea Edeni—na kwamba Kanisa la Kikristo, kama la kipekee katika mpango huu mkuu, litapata mabadiliko ya asili kutoka ya kibinadamu kwenda ya kiroho, watu wa Kikristo kwa ujumla wamedhania kwamba hakuna atakayeokolewa isipokuwa wale wanaofikia asili ya kiroho. Hata hivyo, Maandiko, huku yakitoa ahadi za uzima, baraka na urejesho kwa jamaa zote za dunia, yanatoa na kuahidi mabadiliko ya kwenda kwenye asili ya kiroho kwa Kanisa lililochaguliwa wakati wa Zama za Injili pekee; na hakuna kifungu hata kimoja kinachoweza kupatikana kinachounga mkono matumaini kama hayo kwa wengine wowote.

Ikiwa umati wa wanadamu utaokolewa kutoka katika uharibifu, udhaifu, maumivu, taabu na mauti yote yanayotokana na dhambi, na kurejeshwa kwenye hali ya ukamilifu wa kibinadamu iliyofurahiwa kabla ya anguko, watakuwa wameokolewa kweli na kikamilifu kutoka katika anguko hilo, sawa na wale ambao, chini ya "wito mkuu" maalum wa Zama za Injili, wanakuwa *"washiriki wa asili ya uungu."*

Kushindwa kuelewa vizuri maana ya mwanadamu mkamilifu, uelewa potofu wa maneno *mwenye kufa* na *asiyekufa*, na mawazo yasiyo sahihi kuhusu haki, yote kwa pamoja yamechangia kosa

hili, na yamefanya maandiko mengi ambayo vinginevyo yangeeleweka kwa urahisi yaonekane ya fumbo. Ni mtazamo wa kawaida, ingawa hauna uthibitisho wa andiko hata moja, kwamba mwanadamu mkamilifu hajawahi kuwepo duniani; kwamba yote yanayoonekana kwa mwanadamu duniani ni sehemu tu ya mwanadamu aliyeendelezwa kiasi, na kwamba ili kufikia ukamilifu ni lazima awe wa kiroho. Mtazamo huu unaleta mkanganyiko katika Maandiko badala ya kuleta upatano na uzuri unaotokana na *"kulitumia kwa halali neno la kweli."*

Maandiko yanafundisha kwamba kumekuwepo na wanadamu wawili tu wakamilifu—Adamu na Yesu. Adamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu: yaani, akiwa na nguvu za akili zinazofanana za kufikiri, kumbukumbu, hukumu na utashi, na sifa za kiadili za haki, ukarimu, upendo n.k. Akiwa *"wa dunia, wa udongo,"* alikuwa sura ya kidunia ya kiumbe wa kiroho, akiwa na sifa za aina moja, ingawa zinatofautiana sana kwa kiwango, upana na upeo. Mwanadamu ni mfano wa Mungu kiasi kwamba Mungu anaweza kumwambia hata mwanadamu aliyeanguka, *"Haya, **njoni, tusemezane**."*

Kama vile Yehova alivyo mtawala juu ya vitu vyote, ndivyo mwanadamu alivyofanywa kuwa mtawala juu ya vitu vyote vya kidunia—*"Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama..."* (**Mwanzo 1:26**) Musa anatuambia (**Mwanzo 1:31**) kwamba Mungu alimtambua mwanadamu **aliyemuumba**—si tu kuanza kumuumba, bali kumkamilisha—na Mungu alimwona kiumbe wake kuwa *"mwema sana,"* yaani, mkamilifu; kwa maana machoni pa Mungu hakuna kitu chini ya ukamilifu kinachoitwa **mwema sana**, kwa viumbe vyake wenye akili.

Ukamilifu wa mwanadamu, kama alivyoumbwa, unaelezwa katika **Zaburi 8:5-8**:

> *"Umemfanya mdogo punde kuliko malaika; Umemvika taji ya utukufu na heshima; Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; Umevitia*

vitu vyote chini ya miguu yake. Kondoo na ng'ombe wote pia, Naam, na wanyama wa porini; Ndege wa angani, na samaki wa baharini."

Imependekezwa na wengine wanaotaka kuifanya Biblia ipatane na nadharia ya mageuzi, kwamba kauli, *"mdogo punde,"* katika **Waebrania 2:7**, inaweza kueleweka kumaanisha mdogo kwa **muda mfupi**, na si mdogo kwa **daraja** kuliko malaika. Hata hivyo, hakuna mamlaka wala sababu ya tafsiri kama hiyo. Hii ni nukuu kutoka Zaburi 8:5, na ulinganisho wa kina wa maandiko ya Kiebrania na Kigiriki hauwezi kuacha shaka yoyote juu ya maana yake. Wazo, lililoelezwa wazi, ni mdogo kwa daraja kidogo kuliko malaika.

Daudi, katika zaburi hiyo, anazungumzia mwanadamu katika hali yake ya asili, na kinabii anadokeza kwamba Mungu hajauacha mpango wake wa asili wa kumfanya mwanadamu awe kwa mfano wake na awe mfalme wa dunia, na kwamba **atamkumbuka**, atamkomboa na kumrejesha tena katika hali hiyo hiyo. Mtume (**Waebrania 2:7**) anasisitiza ukweli huohuo—kwamba kusudi la asili la Mungu halijaachwa; kwamba mwanadamu, aliyekuwa mkuu na mkamilifu mwanzoni, mfalme wa dunia, atakumbukwa, atajiliwa, na kurejeshwa. Kisha anaongeza, Bado hatuoni urejesho huu ulioahidiwa, lakini tunaiona hatua ya kwanza anayoichukua Mungu kuelekea kuutekeleza. Tunamwona Yesu amevikwa utukufu na heshima hii ya uanadamu mkamilifu, ili yeye, kama fidia au mbadala anayefaa, aweze kwa fadhili ya Mungu kuonja mauti kwa ajili ya kila mtu, na hivyo kuandaa njia ya kumrejesha mwanadamu kwa yote yaliyopotea. Rotherham, mmoja wa watafsiri waangalifu sana, anatafsiri kifungu hiki kama ifuatavyo:

*"Mtu ni nini, hata umkumbuke; Au mwana wa Adamu, hata umjilie? Umemfanya **mdogo punde kuliko wajumbe**; Kwa utukufu na heshima umemvika taji, Nawe umemweka juu ya kazi za mikono yako."*

Wala isidhaniwe kwamba mdogo kwa daraja kidogo inamaanisha mkamilifu kidogo. Kiumbe anaweza kuwa mkamilifu, lakini

awe katika kiwango cha chini cha uwepo kuliko mwingine; kwa mfano, farasi mkamilifu atakuwa chini kuliko mwanadamu mkamilifu, n.k. Kuna asili mbalimbali, zenye uhai na zisizo na uhai. Ili kutoa mfano, tunapanga jedwali lifuatalo:

Madaraja ya Viumbe wa Kiroho wa Mbinguni	Madaraja ya Viumbe wa Kidunia au Wanyama	Madaraja katika Ufalme wa Mimea	Madaraja katika Ufalme wa Madini
Uungu/Divine	Mwanadamu	Miti	Dhahabu
------	Wanyama Wakubwa	Vichaka	Fedha
------	Ndege	Nyasi	Shaba
Kimalaika/angelic	Samaki	Mosi	Chuma

Kila moja ya madini yaliyotajwa inaweza kuwa safi, lakini dhahabu inashika nafasi ya juu zaidi. Ingawa kila aina ya mimea ingefikishwa kwenye ukamilifu, bado zingetofautiana katika asili na daraja. Vivyo hivyo kwa wanyama: kama kila spishi ingefikishwa kwenye ukamilifu, bado kungekuwa na utofauti; **kwa maana kuikamilisha asili hakubadili asili hiyo.*** Madaraja ya viumbe wa kiroho, pia, ingawa ni wakamilifu, yanahusiana kama ya juu na ya chini katika asili au aina. Asili ya uungu ndiyo ya juu zaidi na bora kuliko asili zote za kiroho. Kristo alipofufuka alifanywa *"bora zaidi"* kuliko malaika wakamilifu kama vile asili

* *Neno **asili** wakati mwingine hutumika kwa maana isiyo rasmi, kwa mfano, inaposemwa kwamba mbwa ana tabia ya ukali, au farasi ana tabia ya upole, au ni mwenye tabia mbaya. Lakini katika kutumia neno hivi, linamaanisha tu hali ya kiumbe anayeelezewa ikilinganishwa na wengine, na, kwa maana halisi, haihusiani na **asili** yenyewe.*

ya uungu ilivyo bora kuliko asili ya kimalaika. —**Waebrania 1:3-5**

Angalia kwa makini kwamba ingawa makundi yaliyotajwa katika jedwali hapo juu ni tofauti na yametengana, bado ulinganisho unaweza kufanywa kati yao, hivi: Daraja la juu zaidi la madini liko chini, au **chini kidogo**, kuliko daraja la chini zaidi la mimea, kwa sababu katika mimea kuna uhai. Hivyo daraja la juu zaidi la mimea liko **chini kidogo** kuliko daraja la chini zaidi la uhai wa wanyama, kwa sababu uhai wa wanyama, hata katika viwango vyake vya chini kabisa, una akili ya kutosha kuwa na ufahamu wa kuwepo. Vivyo hivyo mwanadamu, ingawa ndiye wa juu zaidi wa viumbe wa kidunia au wanyama, yuko *"chini kidogo kuliko malaika,"* kwa sababu malaika ni viumbe wa kiroho au wa mbinguni.

Kuna tofauti ya ajabu kati ya mwanadamu tunavyomwona sasa, akiwa ameshushwa hadhi na dhambi, na mwanadamu mkamilifu ambaye Mungu alimfanya kwa mfano wake. Dhambi imebadilisha polepole sura yake, na pia tabia yake. Vizazi vilivyoongezeka, kwa ujinga, uasherati na upotovu wa jumla, vimeifisha na kuiharibu sana jamii ya wanadamu kiasi kwamba katika idadi kubwa ya watu mfano wa Mungu umekaribia kufutika kabisa. Sifa za kiadili na kiakili zimedumazwa; na silika za kinyama, zilizokuzwa isivyofaa, hazisawazishwi tena na zile za juu. Mwanadamu amepoteza nguvu za kimwili kiasi kwamba, pamoja na msaada wote wa sayansi ya tiba, wastani wa urefu wa maisha yake sasa ni takriban miaka thelathini, ilhali mwanzoni aliishi miaka mia tisa thelathini chini ya adhabu ileile. Lakini ingawa ametiwa unajisi na kushushwa hadhi na dhambi na adhabu yake, yaani kifo, kinachofanya kazi ndani yake, mwanadamu atarejeshwa kwenye ukamilifu wake wa asili wa akili na mwili, na kwenye utukufu, heshima na mamlaka, Kipindi cha/kupitia utawala wa Milenia wa Kristo. Vitu vitakavyorejeshwa kupitia Kristo ni vile vilivyopotea kupitia kosa la Adamu. (**Warumi 5:18, 19**) Mwanadamu hakupoteza

paradiso ya mbinguni bali ya kidunia. Chini ya adhabu ya kifo, hakupoteza uwepo wa kiroho bali wa kibinadamu; na yote yaliyopotea yalinunuliwa tena na Mkombozi wake, aliyetangaza kwamba alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea. **—Luka 19:10**

Pamoja na hayo yaliyo hapo juu, tuna uthibitisho kwamba mwanadamu mkamilifu si kiumbe wa **kiroho**. Tunaambiwa kwamba Bwana wetu, kabla ya kuacha utukufu wake na kuwa mwanadamu, alikuwa *"katika mfano wa Mungu"*—mfano wa kiroho, kiumbe wa kiroho; lakini kwa kuwa ili awe fidia kwa ajili ya wanadamu ilibidi awe mwanadamu, wa asili ileile kama ya mwenye dhambi ambaye angekuwa mbadala wake katika kifo, ilikuwa ni lazima asili yake ibadilishwe. Na Paulo anatuambia kwamba hakutwaa asili ya malaika, hatua moja chini ya yake, bali alishuka hatua mbili na kutwaa asili ya wanadamu—akawa mwanadamu; *"alifanyika mwili."* **—Waebrania 2:16; Wafilipi 2:7, 8; Yohana 1:14**

Angalia kwamba hili halifundishi tu kwamba asili ya kimalaika siyo aina pekee ya viumbe wa kiroho, bali kwamba ni asili ya chini kuliko ile ya Bwana wetu kabla ya kuwa mwanadamu; na wakati huo hakuwa juu kama alivyo sasa, kwa maana *"Mungu alimwadhimisha mno,"* kwa sababu ya utii wake katika kuwa fidia ya hiari ya mwanadamu. (**Wafilipi 2:8, 9**) Sasa yeye ni wa daraja la juu zaidi la viumbe wa kiroho, mshiriki wa asili ya uungu (ya Yehova).

Lakini si tu kwamba tunapata uthibitisho kwamba asili za kimungu, za kimalaika na za kibinadamu zimetengana na ni tofauti, bali hii inathibitisha kwamba kuwa mwanadamu mkamilifu si kuwa malaika, kama vile ambavyo ukamilifu wa asili ya kimalaika haumaanishi kwamba malaika ni wa kimungu na sawa na Yehova; kwa maana Yesu **hakutwaa asili ya malaika**, bali asili tofauti—**asili ya wanadamu**; si asili isiyo kamilifu ya kibinadamu kama tulivyo nayo sasa, bali asili **kamilifu** ya kibinadamu. Alikuwa **mwanadamu**; si kiumbe aliyepotoka na

karibu kufa kama walivyo wanadamu sasa, bali mwanadamu katika nguvu kamili ya ukamilifu.

Tena, Yesu ni lazima awe alikuwa mwanadamu mkamilifu la sivyo asingeweza kuishika sheria kamilifu, ambayo ndiyo kipimo kamili cha uwezo wa **mwanadamu mkamilifu**. Na ni lazima awe alikuwa mwanadamu mkamilifu la sivyo asingeweza kutoa fidia (bei sawasawa—**1 Timotheo 2:6**) kwa ajili ya uhai uliopotezwa wa mwanadamu mkamilifu Adamu; "*Kwa maana kwa kuwa mauti ililetwa na **mtu**, vivyo hivyo na kiyama ya wafu ililetwa na **mtu**.*" (**1 Wakorintho 15:21**) Kama angekuwa na kiwango kidogo tu cha kutokamilika, ingethibitisha kwamba alikuwa chini ya hukumu, na kwa hiyo asingeweza kuwa dhabihu inayokubalika; wala asingeweza kuishika kikamilifu sheria ya Mungu. Mwanadamu mkamilifu alijaribiwa, akashindwa, na akahukumiwa; na ni mwanadamu mkamilifu pekee ndiye angeweza kutoa **bei sawasawa** kama Mkombozi.

Sasa tuna swali mbele yetu kwa uwazi katika namna nyingine, yaani: Ikiwa Yesu alipokuwa katika mwili alikuwa mwanadamu mkamilifu, kama Maandiko yanavyoonyesha, je, hilo halithibitishi kwamba mwanadamu mkamilifu ni kiumbe wa kibinadamu, wa kimwili—si malaika, bali chini kidogo kuliko malaika? Hitimisho la kimantiki halina shaka; na kwa kuongezea, tuna kauli iliyoongozwa na roho ya Mtunga-zaburi (**Zaburi 8:5-8**) na rejea ya Paulo kwayo katika **Waebrania 2:7-9**.

Wala Yesu hakuwa mchanganyiko wa asili hizi mbili, ya kibinadamu na ya kiroho. Kuchanganya asili mbili hakuzalishi mojawapo, bali kitu kisicho kamili, cha chotara, ambacho ni cha kuchukiza kwa mpango wa kimungu. Yesu alipokuwa katika mwili alikuwa kiumbe mkamilifu wa kibinadamu; kabla ya wakati huo alikuwa kiumbe mkamilifu wa kiroho; na tangu ufufuo wake yeye ni kiumbe mkamilifu wa kiroho wa daraja la juu zaidi au la kimungu. Haikuwa hadi wakati wa kujiweka kwake wakfu hata mauti, kama ilivyoonyeshwa kwa mfano katika ubatizo wake—akiwa na umri wa miaka thelathini (utu uzima, kulingana

na Sheria, na kwa hiyo wakati sahihi wa kujiweka wakfu kama **mwanadamu**)—ndipo alipopokea arabuni ya urithi wake wa asili ya uungu. (**Mathayo 3:16, 17**) Asili ya kibinadamu ilibidi **iwekwe wakfu kwa ajili ya mauti** kabla ya yeye kupokea hata **dhamana** ya asili ya uungu. Na haikuwa mpaka wakfu huo ulipotekelezwa kihalisi na alipokuwa ameitolea dhabihu asili ya kibinadamu, hata mauti, ndipo Bwana wetu Yesu alipokuwa mshiriki kamili wa asili ya uungu. Baada ya kuwa mwanadamu alitii hata mauti; **kwa hiyo**, Mungu alimwadhimisha mno na kumpandisha kwenye asili ya uungu. (**Wafilipi 2:8, 9**) Ikiwa andiko hili ni kweli, inafuata kwamba hakuinuliwa kwenye asili ya uungu mpaka asili ya kibinadamu ilipotolewa dhabihu kihalisi—ikiwa imekufa.

Hivyo tunaona kwamba ndani ya Yesu hakukuwa na mchanganyiko wa asili, bali mara mbili alipata uzoefu wa mabadiliko ya asili; kwanza, kutoka ya kiroho kwenda ya kibinadamu; baadaye, kutoka ya kibinadamu kwenda daraja la juu zaidi la asili ya kiroho, yaani, ya kimungu; na katika kila kisa, moja iliachwa kwa ajili ya nyingine.

Katika mfano huu mkuu wa uanadamu mkamilifu, uliosimama bila dosari mbele ya ulimwengu hadi ulipotolewa dhabihu kwa ajili ya ukombozi wa ulimwengu, tunaona ukamilifu ambao jamii yetu ilianguka kutoka kwake katika Adamu, na ambao itarejeshwa kwake. Katika kuwa fidia ya mwanadamu, Bwana wetu Yesu alitoa **sawa na** kile ambacho mwanadamu alipoteza; na kwa hiyo wanadamu wote wanaweza kupokea tena, kupitia imani katika Kristo, na utii kwa matakwa yake, si asili ya kiroho, bali asili tukufu, kamilifu ya **kibinadamu**—"kile kilichopotea."

Uwezo na nguvu kamilifu za kiumbe mkamilifu wa kibinadamu zinaweza kutumika bila kikomo, na juu ya mambo mapya na mbalimbali yenye kuvutia, na maarifa na ujuzi vinaweza kuongezeka sana; lakini hakuna ongezeko kama hilo la maarifa au nguvu litakaloleta mabadiliko ya asili, au kuifanya iwe zaidi ya kamilifu. Itakuwa tu ni kupanuka na kukuza kwa nguvu

kamilifu za asili ya kibinadamu. Ongezeko la maarifa na ujuzi bila shaka litakuwa fursa iliyobarikiwa ya mwanadamu kwa milele yote; bado atakuwa mwanadamu, na atakuwa anajifunza tu kutumia kikamilifu zaidi nguvu za asili ya kibinadamu alizonazo tayari. Zaidi ya mipaka yake mipana hawezi kutumaini, wala hatatamani, kusonga mbele, tamaa zake zikiwa na kikomo kulingana na upeo wa nguvu zake.

Wakati Yesu akiwa mwanadamu alikuwa kielelezo cha asili kamilifu ya kibinadamu, ambayo umati wa wanadamu utarejeshwa kwake, tangu ufufuo wake yeye ndiye kielelezo cha asili tukufu ya kimungu ambayo Kanisa linaloshinda, wakati wa ufufuo, litashiriki pamoja naye.

Kwa sababu zama za sasa zimetolewa hasa kwa ajili ya maendeleo ya kundi hili linalopewa **mabadiliko** ya asili, na kwa sababu nyaraka za mitume zimetolewa kwa ajili ya maelekezo ya "kundi dogo" hili, isidhaniwe kwamba mipango ya Mungu inaishia na ukamilifu wa kundi hili teule. Wala, kwa upande mwingine, hatupaswi kwenda kwenye upande mwingine uliokithiri, na kudhani kwamba ahadi maalum za asili ya uungu, miili ya kiroho, n.k., zilizotolewa kwa hawa, ndio kusudi la Mungu kwa wanadamu wote. Kwa hawa ndizo *"ahadi zilizo kuu mno, za thamani,"* zilizo juu ya ahadi nyingine za thamani zilizotolewa kwa wanadamu wote. Ili kulitumia kwa halali Neno la kweli, tunapaswa kutambua kwamba Maandiko yanatambua ukamilifu wa asili ya uungu katika "kundi dogo," na ukamilifu wa asili ya kibinadamu katika ulimwengu uliorejeshwa, kama mambo mawili tofauti.

Hebu sasa tuchunguze kwa undani zaidi, Viumbe wa kiroho ni nini? wana nguvu gani? na wanaongozwa na sheria gani? Wengi wanaonekana kufikiri, kwa sababu hawaelewi asili ya kiumbe wa kiroho, kwamba ni lazima iwe ni hadithi ya kubuni tu, na juu ya somo hili ushirikina mwingi umeenea. Lakini Paulo haonekani kuwa na wazo kama hilo. Ingawa anadokeza kwamba mwanadamu hawezi kuielewa asili ya juu, ya kiroho (**1**

Wakorintho 2:14), bado anasema waziwazi, kana kwamba ni kwa ajili ya kujilinda dhidi ya mawazo yoyote ya kubuni au ya kishirikina, kwamba kuna mwili wa kiroho, na pia mwili wa asili (wa kibinadamu), wa mbinguni na pia wa duniani, na utukufu wa duniani na pia wa mbinguni. Utukufu wa duniani, kama tulivyoona, ulipotea kwa dhambi ya Adamu wa kwanza, na utarejeshwa kwa jamii ya wanadamu na Bwana Yesu na Bibi-arusi wake (Kristo, Kichwa na mwili) wakati wa utawala wa Milenia. Utukufu wa mbinguni bado hauonekani isipokuwa kama unavyofunuliwa kwa jicho la imani na Roho kupitia Neno. Utukufu huu ni tofauti na umetengana. **—1 Wakorintho 15:38-49** Tunajua kwa kiasi fulani mwili wa asili, wa kidunia, ulivyo, kwa maana sasa tuna miili kama hiyo, ingawa tunaweza tu kukadiria utukufu wa ukamilifu wake. Ni nyama, damu na mifupa; kwa maana *"kilichozaliwa kwa mwili ni mwili."* Na kwa kuwa kuna aina mbili tofauti za miili, tunajua kwamba ule wa kiroho, uwe wowote ule, haujaundwa kwa nyama, damu na mifupa: ni wa mbinguni, wa kiroho—*"Na kilichozaliwa kwa Roho ni roho."* Lakini mwili wa kiroho ni nini, hatujui, kwa maana *"haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini... tutafanana naye."* **—Yohana 3:6; 1 Yohana 3:2**

mikopo (madeni) na mawazo—ambao sasa mwelekeo wa kinyume unaanza kutokea polepole.

Katika miaka michache iliyopita, zimezalishwa kwa wingi zana za kilimo za kila aina zinazomwezesha mtu mmoja kufanya kazi sawa na watu watano walivyoweza kufanya zamani. Hii ina athari maradufu: kwanza, ekari nyingi mara tatu zinalimwa, zikitoa ajira kwa wafanyakazi watatu kati ya watano, hivyo kuwaacha wawili bila kazi ili washindanie kazi nyingine; pili, wale watatu waliobaki wanaweza, kwa kutumia mitambo, kuzalisha mazao mengi kama watu kumi na tano wangefanya bila hiyo. Mabadiliko yaleyale au makubwa zaidi yanafanywa katika idara nyingine kwa njia zinazofanana; kwa mfano, katika utengenezaji wa chuma na chuma cha pua. Ukuaji wake umekuwa mkubwa sana kiasi kwamba idadi ya waajiriwa imeongezeka sana, licha ya ukweli kwamba mitambo imemwezesha mtu mmoja kwa sasa kufanya kazi sawa na watu kumi na wawili walivyofanya zamani. Moja ya matokeo itakuwa kwamba hivi karibuni sana uwezo wa viwanda hivi vikubwa utazidi mahitaji makubwa ya sasa, na mahitaji hayo, badala ya kuendelea kuongezeka, huenda yakapungua; kwani ulimwengu unajazwa kwa kasi na reli kuliko mahitaji ya sasa, na matengenezo ya kila mwaka ya reli hizi huenda yakatoshelezwa na chini ya nusu ya idadi ya sasa ya viwanda.

Hivyo tunakutana na hali ya kipekee ambapo kuna uzalishaji kupita kiasi, unaosababisha ukosefu wa shughuli mara kwa mara kwa mitaji na wafanyakazi, huku wakati huohuo wengine wakikosa ajira ambayo ingewawezesha kupata mahitaji na anasa na hivyo kwa kiasi fulani kuponya tatizo la uzalishaji kupita kiasi. Na mwelekeo wa uzalishaji kupita kiasi na ukosefu wa ajira unaongezeka, na unahitaji tiba ya aina fulani ambayo madaktari wa jamii wanaitafuta, lakini ambayo mgonjwa hataitumia.

Wakati, kwa hiyo (anaendelea mfanyakazi), tunatambua kwamba upatikanaji unapoanza kuzidi mahitaji, ushindani unapunguza sana faida ya mitaji na mitambo, na kote ulimwenguni

unawatesa matajiri kwa kupunguza faida zao, na katika baadhi ya matukio kuwasababishia hasara halisi badala ya faida, bado tunaamini kwamba tabaka lililofaidika zaidi na "mlipuko" na mfumuko wa bei linapaswa kuteseka zaidi katika mwelekeo wa kinyume, badala ya umati kuteseka kutokana nao. Kwa lengo hili, na kwa sababu hizi, wafanyakazi wanachukua hatua kupata matokeo yafuatayo—kwa sheria ikiwezekana, au kwa nguvu na uvunjaji wa sheria katika nchi ambazo, kwa sababu yoyote ile, sauti ya umati haisikilizwi, na maslahi ya umma hayalindwi:

Inapendekezwa kwamba masaa ya kazi yapunguzwe kulingana na ustadi au ugumu wa kazi, bila kupunguza mshahara, ili kuajiri idadi kubwa zaidi ya watu bila kuongeza bidhaa, na hivyo kusawazisha uzalishaji kupita kiasi unaokuja kwa kuwapa watu wengi zaidi uwezo wa kununua. Inapendekezwa kurekebisha na kuweka kikomo cha riba ya pesa kwa kiwango cha chini sana kuliko viwango vya sasa, na hivyo kulazimisha upole wa wakopeshaji kwa wakopaji au tabaka la maskini, la sivyo mitaji yao itakaa bila kazi au kuingia kutu.

Inapendekezwa kwamba reli ziwe mali ya watu, zikiendeshwa na watumishi wao, maafisa wa serikali, au sheria izuie uhuru wao, tozo, n.k., na kulazimisha uendeshaji wao kwa namna ya kuwahudumia umma vizuri zaidi. Kama ilivyo sasa, reli zilizojengwa wakati wa mfumuko wa bei, badala ya kupunguza mitaji yao ili kuendana na upungufu wa jumla wa thamani unaoonekana katika kila idara nyingine ya biashara, zimezidisha mitaji yao ya hisa iliyokuwa mikubwa mara mbili au tatu (kwa kawaida huitwa kuongeza thamani ya hisa kiujanja), bila thamani halisi kuongezwa.

Hivyo inakuwa kwamba mifumo mikubwa ya reli inajitahidi kulipa riba na gawio juu ya hisa na madeni ya dhamana ambayo kwa wastani ni makubwa mara nne kuliko gharama halisi ya kujenga reli hizi zikiwa mpya leo. Matokeo yake, umma unateseka. Wakulima wanatozwa nauli kubwa kwa mizigo, na wakati mwingine wanaona ni faida kuchoma nafaka zao kama kuni; na

hivyo gharama ya chakula kwa watu inakuwa kubwa zaidi bila kuwa na faida kwa mkulima. Inapendekezwa kurekebisha jambo hili, ili reli zilipe wanahisa wao takriban asilimia nne ya thamani yao halisi ya sasa, na si asilimia nne hadi nane, ya thamani yao iliyoongezwa mara tatu au nne, kama nyingi zinavyofanya sasa, kwa kuzuia ushindani kupitia makubaliano ya pamoja.

Tunajua vizuri, anasema fundi, kwamba machoni pa wale wanaomiliki hisa za reli zenye thamani iliyoongezwa kiujanja, na hisa nyingine, upungufu huu wa faida kwenye mitaji yao iliyowekezwa utaonekana kuwa wa kutisha, na utakuwa kama kung'oa meno, na watahisi kwamba haki zao (?) za kutumia leseni walizopewa na watu, ili kuwakamua faida kubwa, kulingana na thamani za kubuni, zinakiukwa vibaya sana, na kwamba watapinga kwa nguvu zao zote. Lakini tunahisi kwamba wanapaswa kushukuru kwamba umma una huruma sana, na kwamba hawatakiwi kurudisha mamilioni ya dola ambayo tayari yamepatikana kwa njia hii.

Tunahisi kwamba wakati umefika kwa umati wa watu kushiriki kwa usawa zaidi baraka za siku hii ya baraka, na ili kufanya hivi ni muhimu kutunga sheria ili mashirika yote yenye tamaa, yaliyonona kwa pesa na mamlaka kutoka kwa umma, yazuiwe, na kulazimishwa na sheria kuhudumia umma kwa bei nafuu. Hakuna njia nyingine ambayo baraka hizi za Mungu zinaweza kupatikana kwa umma.

Kwa hiyo, ingawa mashirika makubwa, yanayowakilisha mitaji, kwa kiasi kikubwa ni baraka na faida, tunaona kila siku kwamba yamevuka kiwango cha manufaa na yanakuwa mabwana wa watu, na yasipodhibitiwa, hivi karibuni yatawarudisha wafanyakazi kwenye umaskini na utumwa. Mashirika, yaliyoundwa na idadi ya watu wote wakiwa matajiri kwa kiasi fulani, yanakaribia haraka kuchukua nafasi ileile kwa umma wa Amerika kama Mabwana wa Uingereza na Ulaya yote wanavyochukua kwa umati huko, isipokuwa tu kwamba mashirika yana nguvu zaidi.

Ili kutimiza madhumuni yetu, wafanyakazi wa ujira wanaendelea kusema, tunahitaji umoja. Lazima tuwe na ushirikiano wa umati la sivyo hatuwezi kamwe kutimiza chochote dhidi ya mamlaka na ushawishi mkubwa kiasi hicho. Na ingawa tumejipanga katika vyama vya wafanyakazi, n.k., isieleweke kwamba lengo letu ni uvurugaji au dhuluma kwa tabaka lolote. Sisi, umati wa watu, tunataka tu kulinda haki zetu, na za watoto wetu, kwa kuweka mipaka inayofaa kwa wale ambao utajiri na mamlaka yao vinginevyo vingeweza kutuponda—utajiri na mamlaka ambayo, yakitumiwa na kudhibitiwa ipasavyo, yanaweza kuwa baraka ya jumla zaidi kwa wote. Kwa neno moja, wanamalizia, tungetekeleza ile kanuni ya dhahabu—"**Watendee wengine yale unayotaka wakutendee wewe.**"

Ingekuwa furaha kwa pande zote zinazohusika kama njia hizo za kiasi na za busara zingefanikiwa; kama matajiri wangeridhika na mali zao za sasa na kushirikiana na umati mkubwa wa watu katika uboreshaji wa jumla na wa kudumu wa hali ya matabaka yote; kama wafanyakazi wangeridhika na madai yanayofaa; kama kanuni ya dhahabu ya upendo na haki ingeweza kutekelezwa.

Lakini watu katika hali yao ya sasa hawataizingatia kanuni hii bila kulazimishwa. Ingawa kuna baadhi miongoni mwa mafundi wa ulimwengu ambao wangekuwa na kiasi na haki katika mawazo yao, wengi si hivyo, bali watakuwa na msimamo mkali, wasio wa haki na wenye kiburi katika mawazo na madai yao, kupita kiasi. Kila ridhaa kutoka kwa wenye mitaji itaongeza tu madai na mawazo hayo; na wote wenye uzoefu wanajua kwamba kiburi na utawala wa maskini wasio na elimu ni mkali mara dufu.

Na vivyo hivyo miongoni mwa matajiri—wengine wana huruma kamili kwa tabaka la wafanyakazi, na wangefurahi kutenda kulingana na huruma yao kwa kufanya mipango ambayo polepole ingeleta mageuzi yanayohitajika; lakini wao ni wachache sana na hawana nguvu kabisa katika uendeshaji wa

mashirika na kwa kiasi kikubwa katika biashara zao za kibinafsi. Kama ni wafanyabiashara au wazalishaji, hawawezi kupunguza masaa ya kazi au kuongeza mishahara ya waajiriwa wao; kwani washindani wao wangeuza bidhaa kwa bei ya chini kuliko wao, na maafa ya kifedha kwao wenyewe, wadai wao na waajiriwa wao yangefuata.

Hivyo tunaona sababu ya asili ya taabu kubwa ya hii "**Siku ya Yehova.**" Ubinafsi, na upofu kwa kila kitu isipokuwa maslahi yao wenyewe, utatawala wengi kwa pande zote mbili za suala hili.

Wafanyakazi watajipanga na kuunganisha maslahi yao, lakini ubinafsi utaharibu umoja huo; na kila mmoja, akisukumwa hasa na kanuni hiyo, atapanga njama na kula njama katika mwelekeo huo. Wengi, wasio na elimu na wenye kiburi, watapata udhibiti, na tabaka bora litakuwa halina nguvu ya kuzuia kile ambacho akili zao zilikipanga.

Wenye mitaji watasadiki kwamba kadiri wanavyolegeza kamba ndivyo watakavyodaiwa zaidi, na hivi karibuni wataamua kupinga madai yote. Maasi yatatokea; na katika hofu na wasiwasi wa jumla mitaji itaondolewa kwenye miradi ya umma na ya kibinafsi, na kudorora kwa biashara na mshtuko wa kifedha utafuata. Maelfu ya watu watakaopoteza ajira kwa njia hii hatimaye watakata tamaa. Ndipo sheria na utaratibu vitaondolewa—milima itamezwa katika bahari hiyo yenye dhoruba. Hivyo dunia ya kijamii itayeyuka, na mbingu za kiserikali (kanisa na serikali) zitatoweka; na wote wenye kiburi, na wote watendao uovu, watakuwa kama mabua. Ndipo mashujaa watalia kwa uchungu, matajiri wataomboleza, na hofu na dhiki vitakuwa juu ya umati wote.

Hata sasa, watu wenye busara, wanaoona mbali, wanajikuta mioyo yao inawazimia wanapotazamia mambo hayo yajayo ulimwenguni, kama vile Bwana wetu alivyotabiri. (*Luka 21:26*) Maandiko yanatuonyesha kwamba katika mpasuko huu wa

jumla, kanisa la jina tu (linalojumuisha madhehebu yote) litavutiwa polepole zaidi na zaidi upande wa serikali na matajiri, litapoteza ushawishi wake mwingi juu ya watu, na hatimaye litaanguka pamoja na serikali. Hivyo mbingu [utawala wa kidini], zikiwaka moto, zitatoweka kwa mshindo mkuu.

Taabu yote hii itauandaa tu ulimwengu kutambua kwamba ingawa wanadamu wanaweza kupanga vizuri na kwa busara kiasi gani, mipango yao yote itathibitika kuwa bure maadamu ujinga na ubinafsi viko madarakani na vina udhibiti. Itawasadikisha wote kwamba njia pekee inayowezekana ya kurekebisha tatizo ni kwa kuanzishwa kwa serikali imara na ya haki, ambayo itayatiisha matabaka yote, na kutekeleza kanuni za haki, hadi polepole mioyo ya jiwe ya wanadamu, chini ya mvuto unaofaa, itakapopisha sura ya asili ya Mungu. Na hili ndilo hasa Mungu ameahidi kutimiza kwa wote, kupitia Utawala wa Milenia wa Kristo, ambao Yehova anauanzisha kwa adhabu na masomo ya siku hii ya taabu. *Ezekieli. 11:19; 36:25,36; Yeremia. 31:29-34; Sefania. 3:9; Zabui. 46:8-10*

Ingawa siku hii ya taabu inakuja kama matokeo ya asili na yasiyoepukika ya hali ya mwanadamu ya kuanguka na ya ubinafsi, na ilionwa kikamilifu na kutangazwa na Bwana, aliyeona kwamba sheria na maagizo yake yatapuuzwa na wote isipokuwa wachache hadi uzoefu na ulazima vitakapolazimisha utii, bado wote wanaotambua hali ya mambo ijayo wanapaswa kujiweka wenyewe na mambo yao katika utaratibu unaofaa.

Hivyo tunawaambia wote walio wanyenyekevu—wanyenyekevu wa ulimwengu, pamoja na mwili wa Kristo: "*Mtafuteni Bwana, enyi nyote mlio wanyenyekevu wa dunia, ninyi mliozitenda hukumu zake[mapenzi yake]; itafuteni haki, utafuteni unyenyekevu; huenda mtafichwa katika siku ya hasira ya Bwana.*" (*Sefania. 2:3*)

Hakuna atakayeepuka kabisa taabu hiyo, lakini wale wanaotafuta haki na kufurahia unyenyekevu watakuwa na faida nyingi

kuliko wengine. Namna yao ya maisha, tabia zao za kufikiri na kutenda, pamoja na huruma yao kwa lililo sahihi, ambayo itawawezesha kuelewa hali ya mambo, na pia kuthamini maelezo ya Biblia kuhusu taabu hii na matokeo yake, yote yatashirikiana kuwafanya wateseke kidogo kuliko wengine—hasa kutokana na hofu na wasiwasi unaosumbua.

Mwenendo wa matukio katika Siku hii ya Bwana utakuwa wa udanganyifu sana kwa wale wasio na ufahamu wa Kimaandiko. Itakuja ghafla, kama moto uteketezao makapi (*Sefania. 2:2*), ikilinganishwa na zama ndefu zilizopita na utendaji wake wa polepole; lakini si ghafla kama umeme kutoka angani, kama wengine wanavyotarajia kimakosa wakidhani kwamba mambo yote yaliyoandikwa kuhusu Siku ya Bwana yatatimizwa katika siku ya saa ishirini na nne.

Itakuja kama "mwivi usiku," kwa maana kwamba ujio wake utakuwa wa siri na usiotambuliwa na ulimwengu kwa ujumla. Taabu ya siku hii itakuja kwa mishtuko. Itakuwa ni mfululizo wa mitikisiko ya mara kwa mara na mikali zaidi kadiri siku inavyokaribia, hadi ule wa mwisho. Mtume anaonyesha hivyo anaposema—"kama utungu umjiavyo mwenye mimba." (*1 Wathesalonike. 5:2,3*) Nafuu itakuja tu na kuzaliwa kwa UTARATIBU MPYA wa mambo—mbingu mpya (utawala wa kiroho wa Kristo) na nchi mpya (jamii iliyopangwa upya) ambayo ndani yake kuna haki (*2 Petro. 3:10,13*)—ambamo haki na upendo, badala ya nguvu na ubinafsi, vitakuwa sheria.

Kila mara maumivu haya ya uchungu wa enzi mpya yanapoikumba jamii ya sasa, nguvu na ujasiri wake vitaonekana kuwa vichache zaidi, na maumivu kuwa makali zaidi. Yote ambayo madaktari wa jamii (wanauchumi wa kisiasa) wanaweza kufanya ili kuleta nafuu itakuwa ni kusaidia, na kuelekeza kwa busara mwendo wa kuzaliwa huko kusikoepukika—kuandaa njia polepole kwa ajili ya tukio hilo. Hawawezi kulizuia hata kama wangetaka; kwa maana Mungu amepanga kwamba litatokea. Hata hivyo, wengi wa madaktari wa jamii watakuwa

wajinga kabisa kuhusu ugonjwa halisi na mahitaji na uharaka wa hali hiyo. Hawa watachukua hatua za kukandamiza; na kila mshtuko wa taabu unapopita, watatumia fursa hiyo kuimarisha vifaa vya kuzuia, na hivyo wataongeza maumivu; na ingawa hawatachelewesha kuzaliwa kwa muda mrefu, utendaji wao mbaya utaharakisha kifo cha mgonjwa wao; kwani utaratibu wa zamani wa mambo utakufa katika uchungu wa kuuzaa ule mpya.

Tukiweka kando mfano huu wenye nguvu uliopendekezwa na Mtume, na kusema waziwazi: Juhudi za umati za kujiokoa kutoka kwenye mtego wa Mitaji na mitambo zitakuwa changa; mipango na maandalizi yatakuwa hayajakamilika na hayatatosha, kila mara wanapojaribu kulazimisha njia yao na kuvunja vifungo na mipaka ya "upatikanaji na mahitaji" ambayo inakuwa midogo sana kwao. Kila jaribio lisilofanikiwa litaongeza imani ya Mitaji katika uwezo wake wa kuweka utaratibu mpya wa mambo ndani ya mipaka yake ya sasa, hadi mwishowe nguvu ya sasa ya kuzuia ya mashirika na serikali itakapofikia kikomo chake cha juu, kamba ya mfumo wa jamii itakatika, sheria na utaratibu vitatoweka, na uvurugaji ulioenea utaleta yote ambayo manabii wametabiri kuhusu taabu "ambayo haijatokea namna yake tangu lilipoanza kuwako taifa"—na, asante Mungu kwa uhakikisho ulioongezwa—"wala haitakuwako kamwe" baadaye.

Ukombozi wa Israeli kutoka Misri na kutoka kwa mapigo yaliyowapata Wamisri unaonekana kuonyesha ukombozi ujao wa ulimwengu, mikononi mwa aliye mkuu kuliko Musa, ambaye alikuwa mfano wake. Utakuwa ni ukombozi kutoka kwa Shetani na kila chombo alichobuni kwa ajili ya utumwa wa mwanadamu kwa dhambi na makosa. Na kama vile mapigo juu ya Misri yalivyokuwa na athari ya kuufanya moyo kuwa mgumu mara tu yalipoondolewa, vivyo hivyo nafuu ya muda kutoka kwa maumivu ya Siku hii ya Bwana itakuwa na mwelekeo wa kuwafanya wengine kuwa wagumu, nao watawaambia maskini, kama Wamisri walivyomwambia Israeli, "**Ninyi ni wavivu,"** na

kwa hiyo hamridhiki! na pengine, kama wao, watajaribu kuongeza mzigo. (*Kutoka. 5:4-23*)

Lakini mwishowe watu kama hao watatamani, kama alivyofanya Farao usiku wa manane wa pigo lake la mwisho, kwamba wangelikuwa wametenda kwa upole na busara zaidi zamani sana. (*Kutoka. 12:30-33*) Ili kuonyesha zaidi kufanana huko, kumbuka kwamba taabu za Siku hii ya Bwana zinaitwa "**bakuli saba za ghadhabu,"** au "mapigo saba ya mwisho," na kwamba si mpaka pigo la mwisho ndipo tetemeko kuu la nchi (mapinduzi) linatokea, ambalo katika hilo kila mlima (ufalme) utatoweka. *Ufunuo. 16:17-20*

Wazo lingine kuhusiana na Siku hii ya Taabu ni kwamba imekuja kwa wakati wake hasa—wakati ufaao wa Mungu. Katika kitabu kinachofuata cha kazi hii, ushahidi unatolewa kutoka kwa ushuhuda wa Sheria na Manabii wa Agano la Kale, pamoja na kutoka kwa Yesu na manabii wa kitume wa Agano Jipya, unaoonyesha wazi na bila shaka kwamba Siku hii ya Taabu imewekwa kimkakati mwanzoni mwa utawala mtukufu wa Milenia wa Masihi. Ni maandalizi haya ya lazima kwa ajili ya kazi ijayo ya urejesho katika zama ya Milenia ndiyo yanayosababisha taabu hiyo.

Katika kipindi cha mpito cha miaka elfu sita ya uovu, na hadi wakati uliopangwa wa kuanzishwa kwa serikali ya haki na yenye nguvu ya Kristo, ingekuwa ni madhara dhahiri kwa wanadamu walioanguka kama wangepewa muda mwingi wa uvivu, kupitia maendeleo ya mapema ya mitambo ya sasa inayopunguza kazi, au vinginevyo. Uzoefu umeleta methali isemayo "**Uvivu ni mama wa uovu**," hivyo kuthibitisha hekima ya amri ya Mungu, "*kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi*." Kama mipango yote ya Mungu, huu ni wa fadhili na hekima, na kwa manufaa ya mwisho ya viumbe vyake. Taabu ya Siku ya Bwana, ambayo tayari tunaiona ikikusanyika, inathibitisha hekima ya mpango wa Mungu; kwani, kama tulivyoona, inatokea kama matokeo ya uzalishaji kupita kiasi

unaosababishwa na mitambo inayopunguza kazi, na kutoweza kwa pande mbalimbali za jamii kujirekebisha kulingana na hali mpya, kwa sababu ya ubinafsi kwa upande wa kila mmoja.

Hoja isiyopingika, inayothibitisha kwamba huu ni wakati ufaao wa Mungu wa kuanzisha utaratibu mpya wa mambo, ni kwamba anainua pazia la ujinga na kuleta polepole nuru ya akili na uvumbuzi kwa wanadamu, kama ilivyotabiriwa, wakati ilipotabiriwa, na kwa matokeo yaliyotabiriwa. (*Danieli. 12:4,1*) Kama maarifa yangekuja mapema, taabu ingekuja mapema; na ingawa jamii ingeweza kujipanga upya baada ya dhoruba na kuyeyuka kwake, isingekuwa nchi mpya [mpangilio wa kijamii] ambamo haki ingetawala na kukaa, bali nchi mpya au mpangilio ambao ndani yake dhambi na uovu vingeongezeka zaidi kuliko sasa. Mgawanyo sawa wa manufaa ya mitambo inayopunguza kazi hatimaye ungeleta masaa mafupi zaidi na zaidi ya kazi; na hivyo, akiwa ameondolewa kinga ya asili, mwanadamu aliyeanguka, akiwa na ladha zake zilizopotoka, asingetumia uhuru na wakati wake kwa maendeleo ya kiakili, kimaadili na kimwili, bali, kama historia ya zamani inavyothibitisha, mwelekeo ungekuwa kuelekea uasherati na uovu.

Kuinuliwa kwa sehemu kwa pazia hilo sasa kunaandaa maelfu ya huduma kwa wanadamu, na hivyo kunatoa, tangu mwanzo wa enzi ya urejesho, muda wa elimu na maendeleo ya kimaadili na kimwili, pamoja na maandalizi ya kulisha na kuvisha makundi ambayo yataamshwa kutoka kaburini mara kwa mara. Na zaidi ya hayo, inaweka wakati wa taabu mahali ambapo utakuwa na manufaa kwa wanadamu, kwa kuwa utawapa somo la kutoweza kwao kujitawala, mwanzoni kabisa mwa Milenia, wakati, kwa agizo la Bwana, yeye aliyewakomboa wote anapaswa kuanza kuwabariki kwa utawala imara wa fimbo ya chuma, na kwa maarifa kamili na msaada ambao kwayo wanaweza kurejeshwa kwenye ukamilifu wa asili na uzima wa milele.

Wajibu na Fursa ya Watakatifu

Swali muhimu linajitokeza kuhusu wajibu wa watakatifu wakati wa taabu hii, na msimamo wao unaofaa kuelekea pande mbili zinazopingana ambazo sasa zinajitokeza. Kwamba baadhi ya watakatifu bado watakuwa katika mwili angalau kwa sehemu ya wakati huu wa kuteketeza inaonekana inawezekana. Hata hivyo, msimamo wao ndani yake utatofautiana na wa wengine, si sana kwa sababu watahifadhiwa kimuujiza (ingawa imeahidiwa wazi kwamba mkate na maji yao vitakuwa vya hakika), bali kwa ukweli kwamba, wakiwa wamefundishwa kutoka kwa Neno la Mungu, hawatahisi wasiwasi uleule na hofu isiyo na matumaini itakayouenea ulimwengu. Watatambua taabu hiyo kama maandalizi, kulingana na mpango wa Mungu, kwa ajili ya kuubariki ulimwengu wote, nao watatiwa moyo na kufarijiwa katika yote hayo. Hili limeelezwa kwa nguvu katika *Zaburi. 91; Isaya. 33:2-14,15-24*.

Hivyo, wakifarijiwa na kubarikiwa na uhakikisho wa kimungu, wajibu wa kwanza wa watakatifu ni kuuacha ulimwengu uone kwamba katikati ya taabu na kutoridhika kote kulikoenea, na hata wanaposhiriki katika taabu na kuteseka chini yake, wao wana matumaini, wachangamfu na daima wanafurahi kwa kutazamia matokeo matukufu yaliyotabiriwa katika Neno la Mungu.

Mtume ameandika kwamba **"Utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa";** na ingawa hili daima limekuwa kweli, litakuwa na nguvu maradufu katika Siku hii ya Bwana, wakati kutoridhika ndio ugonjwa mkuu miongoni mwa matabaka yote ya kidunia. Kwa hawa, watakatifu wanapaswa kuwa tofauti dhahiri. Hakujawahi kuwa na wakati ambapo kutoridhika kumeenea hivi; na bado hakujawahi kuwa na wakati ambapo wanadamu wamefurahia fadhila na baraka nyingi kiasi hiki.

Popote tunapotazama, iwe katika majumba ya kifahari ya matajiri, yaliyojaa huduma na fahari ambavyo Sulemani katika utukufu wake wote hakujua karibu chochote kuvihusu, au iwe

tunatazama katika nyumba ya starehe ya mfanyakazi mwangalifu na mwenye kiasi, pamoja na ushahidi wake wa uzuri, faraja, sanaa na anasa, tunaona kwamba kwa kila njia sasa panazidi kila kipindi kingine tangu kuumbwa, mara nyingi zaidi; na bado watu hawana furaha na hawajaridhika. **Ukweli ni kwamba tamaa za moyo wa ubinafsi, uliopotoka, hazina mipaka**. Ubinafsi umewatawala wote kiasi kwamba, tunapotazama, tunaona ulimwengu wote ukisukuma na kuendesha na kunyakua utajiri kwa wazimu. Wachache tu ndio wanaofanikiwa, waliobaki wana wivu na wamechoka kwa sababu wao si wenye bahati, na wote hawajaridhika na wana huzuni—zaidi kuliko wakati mwingine wowote uliopita.

Lakini mtakatifu hapaswi kushiriki katika mapambano hayo. Nadhiri yake ya wakfu ilikuwa kwamba angejitahidi na kunyakua na kukimbilia tuzo ya juu zaidi, ya mbinguni, na hivyo ameachishwa na tamaa za kidunia, na hafanyi kazi kwa ajili ya mambo ya kidunia, isipokuwa kujipatia vitu vya heshima na vya lazima; kwani anazingatia mwendo na mfano wa Bwana na mitume.

Kwa hiyo wao wana **kuridhika pamoja na utauwa**, si kwa sababu hawana malengo, bali kwa sababu malengo yao yameelekezwa mbinguni na yamemezwa katika jitihada za kujiwekea hazina mbinguni na kuwa matajiri kwa Mungu; kwa mtazamo huu, na kwa ujuzi wao wa mipango ya Mungu iliyofunuliwa katika Neno lake, wanaridhika na chochote cha kidunia ambacho Mungu anaweza kuwapa. Hawa wanaweza kuimba kwa furaha:

Nimeridhika, na hali yoyote niliyonayo,

Maana ni mkono wa Mungu unaoniongoza.

Lakini ole! Si watoto wote wa Mungu walio katika msimamo huu. Wengi wameanguka katika kutoridhika kulikoenea ulimwenguni, na wanajinyima furaha za maisha kwa sababu wameacha nyayo za Bwana na wanaungana na ulimwengu—

wakitafuta mambo ya kidunia wawe wanayapata au la, wakishiriki katika kutoridhika kwa ulimwengu, na kushindwa kupata kule kuridhika na amani ambayo ulimwengu hauwezi kuitoa wala kuiondoa.

Kwa hiyo, tunawahimiza watakatifu waache mapambano ya tamaa na majivuno na kutoridhika kwake, na wajitahidi kupata utajiri wa juu zaidi na amani inayotolewa nao. Tungependa kuwakumbusha maneno ya Mtume:

> *"Walakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa. Kwa maana hatukuja na kitu duniani, tena hatuwezi kutoka na kitu; ila tukiwa na chakula[cha lazima] na nguo tutaridhika na vitu hivyo.Lakini hao watakao kuwa na mali[matajiri] huanguka katika majaribu na tanzi, na tamaa nyingi zisizo na maana, zenye kudhuru, ziwatosazo wanadamu katika upotevu na uharibifu. Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha[iwe kwa matajiri au maskini]; ambayo wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na Imani, na kujichoma kwa maumivu mengi. Bali wewe, mtu wa Mungu, uyakimbie mambo hayo; ukafuate haki, utauwa, imani, upendo, saburi, upole. Piga vita vile vizuri vya imani; shika uzima ule wa milele ulioitiwa, ukaungama maungamo mazuri mbele ya mashahidi wengi."* ***1 Timotheo. 6:6-12***

Ikiwa mfano wa watakatifu ni wa kuridhika na matarajio ya furaha, na unyenyekevu wa uchangamfu kwa majaribu ya sasa kwa matumaini ya hakika ya wakati mzuri ujao, mifano kama hiyo hai ni masomo muhimu kwa ulimwengu. Na pamoja na mfano huo, ushauri wa watakatifu kwa wale wanaowazunguka unapaswa kupatana na imani yao. Unapaswa kuwa kama marhamu na zeri ya uponyaji. Fursa inapaswa kutumiwa kuwaelekeza ulimwengu kwenye wakati mzuri ujao, kuwahubiria Ufalme wa Mungu unaokuja, na kuonyesha sababu halisi ya taabu za sasa, na tiba pekee. *Luka 3:14; Waebrania. 13:5; Wafilipi. 4:11*

Ulimwengu maskini unaugua, si tu chini ya magonjwa yake halisi, bali pia chini ya yale ya kuwazia, na hasa chini ya kutoridhika kutokana na ubinafsi, kiburi na tamaa vinavyowasumbua na kuwahangaisha wanadamu kwa sababu hawawezi

kuvitosheleza kikamilifu. Hivyo, ingawa tunaweza kuona pande zote mbili za suala hili, tuwashauri wale walio tayari kusikia waridhike na walivyo navyo, na wasubiri kwa uvumilivu hadi Mungu kwa wakati na njia yake awape baraka nyingi ambazo upendo na hekima yake imewaandalia.

Kwa kuchunguza na kuchochea majeraha na maovu ya kweli au ya kuwazia, tutawadhuru wale ambao tunapaswa kuwasaidia na kuwabariki, hivyo kueneza kutoridhika kwao, na kwa hiyo taabu yao. Lakini kwa kutimiza utume wetu, tukihubiri habari njema za fidia iliyotolewa kwa WOTE, na baraka zitakazokuja kwa WOTE, tutakuwa watangazaji wa kweli wa ufalme—mabalozi wake wa amani. Hivyo imeandikwa, "*Jinsi ilivyo mizuri juu ya milima [falme] miguu yake [washiriki wa mwisho wa mwili wa Kristo] aletaye habari njema, yeye atangazaye amani, aletaye habari njema ya mambo mema.*" *Isaya. 52:7*

Taabu za "Siku hii ya Yehova" zitatoa fursa ya kuhubiri habari njema za mema yajayo, fursa ambayo haipatikani mara nyingi, na heri wale watakaofuata nyayo za Bwana, na kuwa Wasamaria wema wanaofunga majeraha na kumimina mafuta na divai ya faraja na uchangamfu. Uhakikisho unaotolewa kwa watu kama hao ni kwamba kazi yao si bure; kwani hukumu za Bwana zikiwapo duniani, wenyeji wa ulimwengu watajifunza haki. *Isaya. 26:9*

Huruma ya watoto wa Bwana, kama ile ya Baba yao wa mbinguni, lazima iwe kwa kiasi kikubwa inapatana na viumbe vinavyougua, vinavyojitahidi kupata ukombozi wowote kutoka utumwani; ingawa wanapaswa, kama yeye, kuwakumbuka na kuwaonea huruma wale wa matabaka yanayopingana ambao tamaa zao ni kuwa wa haki na wakarimu, lakini juhudi zao zinazuiwa na kuhujumiwa, si tu na udhaifu wa asili yao ya kuanguka, bali pia na mazingira yao maishani, na uhusiano wao na utegemezi wao kwa wengine. Lakini watoto wa Bwana hawapaswi kuwa na huruma na tamaa na juhudi za kiburi, zisizoshibishwa za tabaka lolote. Matamshi yao yanapaswa

kuwa ya utulivu na kiasi, na daima yawe ya amani pale ambapo kanuni haiko hatarini. Wanapaswa kukumbuka kwamba hii ni vita ya Bwana, na kwamba kwa upande wa siasa au masuala ya kijamii, hawana suluhisho la kweli isipokuwa lile lililotabiriwa katika Neno la Mungu. Hivyo, wajibu wa waliojiweka wakfu ni, kwanza kabisa, kuona kwamba hawazuii njia ya gari la Yehova, na kisha '**kusimama imara na kuuona wokovu wa Mungu,**' kwa maana ya kutambua kwamba si sehemu ya kazi yao kushiriki katika pambano hilo, bali kwamba ni kazi ya Bwana, kupitia vyombo vingine. Bila kujali mambo hayo yote, wanapaswa kukaza mwendo katika utume wao wenyewe, wakitangaza ufalme wa mbinguni uliokaribia kama ndiyo tiba pekee kwa tabaka zote, **na tumaini lao pekee**.

SOMO LA XVI
MAWAZO YA HITIMISHO

WAJIBU WETU KWA ILE KWELI—GHARAMA YAKE, THAMANI YAKE, NA FAIDA YAKE

KATIKA masomo yaliyotangulia, tumeona jinsi nuru ya asili na nuru ya ufunuo (Maandiko) zinavyodhihirisha wazi kwamba Mungu mwenye akili, hekima, uweza wote, na haki ndiye Muumbaji wa vitu vyote, na kwamba Yeye ndiye Bwana mkuu na halali wa wote. Tumejifunza kuwa viumbe vyote, vyenye uhai na visivyo na uhai, viko chini ya mamlaka yake; na kwamba Biblia ni ufunuo wa tabia na mipango yake kwa kiwango alichopenda kuwafunulia wanadamu. Kutoka katika Biblia, tumejifunza kwamba ingawa kwa sasa uovu unaonekana kutawala miongoni mwa baadhi ya viumbe vyake, hali hiyo ipo kwa muda maalum na kwa kiwango maalum, na ni kwa ruhusa yake kwa ajili ya makusudi ya hekima aliyonayo. Pia tumejifunza kwamba ingawa sasa giza linaifunika dunia, na giza nene linawafunika watu, nuru ya Mungu itakapofika wakati ufaao itaondoa giza lote, na dunia yote itajazwa na utukufu wake.

Tumeona kwamba mpango wake mkuu umehitaji zama nyingi kukamilika hadi sasa, na bado kutahitajika zama nyingine ili kuukamilisha kikamilifu. Na kwamba katika zama zote za giza zilizopita, wakati ambapo ilionekana kana kwamba Mungu amewasahau viumbe vyake, mpango wake wa baraka zao za wakati ujao umekuwa ukiendelea kimyakimya lakini kwa ukuu, ingawa katika zama hizo zote siri za mpango wake zilifichwa kwa hekima mbali na wanadamu. Tumeona pia kwamba ile siku au zama ambayo sasa inakaribia kupambazuka duniani, itakuwa ni siku ya hukumu au jaribio la ulimwengu, na kwamba maandalizi yote yaliyotangulia yalikuwa na lengo la kuwapa wanadamu wote kwa ujumla fursa nzuri iwezekanavyo, wakati ambapo kila mmoja binafsi atasimamishwa kwenye jaribio la uzima wa milele.

Kipindi hicho kirefu cha miaka elfu sita kimeongeza sana idadi ya wanadamu, na mapigo pamoja na mateso yao chini ya utawala wa uovu vimewapa uzoefu ambao utakuwa wa faida kubwa kwao watakapoletwa hukumuni. Na ingawa jamii ya wanadamu kwa ujumla imeruhusiwa kuteseka kwa miaka elfu sita, lakini kama mtu mmoja mmoja, kila mmoja amekamilisha safari yake ya maisha katika miaka michache tu.

Tumeona kwamba wakati jamii ya wanadamu ilipokuwa inapitia nidhamu hii muhimu, Mungu alimtuma Mwana wake kwa wakati ufaao ili kuwakomboa. Na ingawa umati wa wanadamu haukumtambua Mkombozi katika hali yake ya unyenyekevu, na hawakuamini kwamba Masihi wa Bwana angekuja kuwaokoa kwa njia *hiyo*, bado Mungu amekuwa, katika zama hizi zilizopita, akichagua makundi mawili kutoka miongoni mwa wale ambao mioyo yao ilimwelekea Yeye na waliozi-amini ahadi zake, ili wapokee heshima za ufalme wake—heshima za kushiriki katika utekelezaji wa mpango wa Mungu. Tumeona kwamba haya makundi mawili teule yataunda sehemu mbili za Ufalme wa Mungu. Na kutoka kwa manabii, tunajifunza kwamba Ufalme huu utaimarishwa duniani hivi karibuni. Chini ya utawala wake wa hekima na haki, familia zote za dunia zitabarikiwa kwa fursa nzuri isiyo na kifani ya kujithibitisha kuwa zinastahili uzima wa milele. Kama matokeo ya ukombozi wao kupitia damu ya thamani ya Kristo, barabara kuu ya utakatifu itajengwa. Waliokombolewa na Bwana (wanadamu wote—Waebrania 2:9) watapata fursa ya kutembea katika njia hiyo. Itakuwa ni njia ya wazi kwa wote, iliyofanywa rahisi kwa ajili ya kila mtu anayetamani kwa dhati kuwa msafi na mtakatifu. Mawe yote ya kukwaza yataondolewa, na mitego yote, vishawishi na mashimo vitaondolewa. Na watakuwa wenye heri wale wote watakaoitumia njia hiyo kupanda kuelekea ukamilifu na uzima wa milele.

Ni dhahiri kwamba hukumu hii, au utawala huu, hauwezi kuanza mpaka Kristo, ambaye Yehova amemchagua kuwa Jaji au

Mtawala wa ulimwengu, atakapokuja tena—si katika unyenyekevu tena, bali katika nguvu na utukufu mwingi; si kuja kuukomboa ulimwengu tena, bali kuuhukumu [kuutawala] ulimwengu kwa haki. Kwa hali yoyote, shauri haliwezi kuendelea mpaka jaji ameketi katika kiti chake cha hukumu na mahakama imefunguliwa kwa wakati uliopangwa, ingawa kabla ya wakati huo kunaweza kuwa na kazi kubwa ya maandalizi. Ndipo Mfalme ataketi katika kiti chake cha enzi cha utukufu, na mbele yake yatakusanywa mataifa yote, naye atawahukumu katika zama hiyo kulingana na matendo yao, akiwafungulia vitabu vya Maandiko na kuijaza dunia kwa kumjua Bwana. Na kwa mwenendo wao chini ya fadhila na msaada wote huo, ataamua ni nani miongoni mwao anayestahili uzima wa milele katika zama za utukufu na furaha zitakazofuata. —*Mathayo 25:31; Ufunuo 20:11-13*

Hivyo, tumeona kwamba kuja kwa Kristo mara ya pili, ili kuusimamisha ufalme wake duniani, ni tukio ambalo watu wa aina zote wanaweza kuwa na tumaini ndani yake, tukio ambalo, likieleweka kikamilifu, litaleta furaha na shangwe katika mioyo yote. Ni siku ambayo "kundi dogo" la Bwana la watakatifu waliojiweka wakfu lina sababu kubwa zaidi ya kushangilia. Ni siku ya furaha ambayo Kanisa, lililochumbiwa kama bikira, linakuwa Bibi-arusi, mke wa Mwana-Kondoo, kwa shangwe; anapotoka nyikani akiwa ameuegemea mkono wa Mpenzi wake, na kuingia katika urithi wake mtukufu.

Ni siku ambayo Kanisa la kweli, likiwa limetukuzwa pamoja na Kichwa chake, litavikwa mamlaka na nguvu za Mungu, na litaanza kazi kubwa kwa ajili ya ulimwengu, ambayo matokeo yake yatakuwa ni urejesho kamili wa vitu vyote. Na itakuwa ni siku ya furaha kwa ulimwengu wakati yule adui mkuu atakapofungwa, pingu zilizowafunga wanadamu kwa miaka elfu sita zitakapovunjwa, na kumjua Bwana kutakapoijaza dunia yote kama maji yaifunikavyo bahari.

Kuyajua mambo haya, ni uthibitisho kwamba yapo karibu, naam, mlangoni, kunapaswa kuwa na ushawishi wenye nguvu juu ya wote, lakini hasa juu ya watoto wa Mungu waliojiweka wakfu, wanaokitafuta kile cheo cha hali ya Uungu. Tunawasihi watu hao kwamba, wanapoinua vichwa vyao na kufurahi wakijua kwamba ukombozi wao unakaribia, waweke kando kila mzigo na kizuizi, na wapige mbio kwa saburi katika shindano waliloanzisha. Acha kujitazama wewe mwenyewe na udhaifu wako usioweza kuepukika, ukijua kwamba udhaifu wote huo umefunikwa kikamilifu na kustahili kupitia fidia iliyotolewa na Kristo Yesu Bwana wetu, na kwamba dhabihu zako na kujikana kwako vinakubalika kwa Mungu kupitia Mkombozi na Bwana wetu—na kwa njia hiyo pekee. Tukumbuke kwamba nguvu ya kutosha ambayo Mungu ametuahidi, na ambayo kwa kuitumia tunaweza kuwa "washindi," inapatikana katika Neno lake.

Ni nguvu inayotokana na *kujua* tabia na mipango yake, na masharti ambayo kwayo tunaweza kushiriki. Petro analieleza hivi, akisema,

> *"Neema na iwe kwenu na amani iongezwe katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu. Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa." —2 Petro 1:2-4*

Lakini, ili kupata maarifa na nguvu hizi, ambazo Mungu amekusudia kumpatia kila mkimbiaji katika shindano la kuwania tuzo ya mbinguni, hakika kutajaribu unyoofu wa ahadi zako za kujiweka wakfu. Umeweka wakfu wakati wako wote na vipawa vyako vyote kwa Bwana; sasa swali ni je, unatoa kiasi gani? Je, bado uko tayari, kulingana na agano lako la wakfu, kuacha yote?—kuacha mipango na mbinu zako mwenyewe, na nadharia zako na za wengine, ili kuukubali mpango wa Mungu, njia yake, na wakati wake wa kufanya kazi yake kuu? Je, uko tayari kufanya hivi kwa gharama ya kuwapoteza marafiki wa

kidunia na kuvunja mahusiano ya kijamii? Na je, uko tayari kuacha kutumia muda kwa ajili ya mambo mengine ili uchunguze kweli hizi tukufu ambazo huichangamsha mioyo ya waliojiweka wakfu kweli, ukijua kwa hakika kwamba itakugharimu kujikana huku? Ikiwa si kila kitu kimewekwa wakfu, au kama hukumaanisha kwa dhati ulipomtolea Bwana kila kitu, basi utaona ni hasara kutumia muda na jitihada zinazohitajika kulichunguza Neno lake kama vile unavyotafuta hazina iliyofichwa, ili upate nguvu unazohitaji kwa ajili ya majaribu yote ya imani yanayohusiana na wakati huu wa sasa (mapambazuko ya Milenia) kuliko nyakati nyingine zote.

Lakini usifikiri kwamba kujitoa huko kutaishia tu katika kutoa muda na nguvu kwa ajili ya funzo hili; la hasha. Unyoofu wa dhabihu yako ya kujikana utajaribiwa kikamilifu, na utathibitisha kama unastahili au hustahili kuwa mshiriki wa lile "**kundi dogo**," yaani, Kanisa linaloshinda, ambalo litapokea heshima za ufalme. Ukiweka bidii katika kulichunguza Neno la Mungu, na kuzipokea kweli zake katika moyo mwema, mnyoofu, na uliowekwa wakfu, kutazaliwa ndani yako upendo mkuu kwa Mungu na mpango wake, na shauku kubwa ya kutangaza habari njema, kuhubiri injili, kiasi kwamba hilo litakuwa ndilo jambo kuu la maisha yako tangu hapo; na hili halitakutenga tu na ulimwengu na Wakristo wengi wa jina tu *kiroho*, bali litaongoza kwenye kujitenga nao kabisa. Watakuona wa ajabu na watakutenga na kundi lao, nawe utadharauliwa na kuhesabiwa mpumbavu kwa ajili ya Kristo; kwa sababu hawakutujua sisi, kama vile wasivyomjua Bwana. —*2 Wakorintho 4:8-10; Luka 6:22; 1 Yohana 3:1; 1 Wakorintho 3:18*

Je, uko tayari kuendelea kumjua Bwana kupitia hali nzuri na hata mbaya? Uko tayari kuacha yote, na kumfuata popote anapokuongoza kupitia Neno lake?—bila kujali matakwa ya marafiki, na pia tamaa zako mwenyewe? Inatumainiwa kwamba wengi waliojiweka wakfu wanaosoma kitabu hiki watachochewa na bidii mpya na ari ya kiroho kupitia kuuelewa vizuri zaidi

mpango wa Mungu, kiasi cha kuweza kusema, "**Kwa neema ya Mungu, nitaendelea mbele ili nimjue na nimtumikie Bwana, haijalishi gharama itakuwa nini**." Kama wale Waberoya waungwana (*Matendo 17:11*), watu kama hao na wajiweke wakfu kuchunguza kwa bidii ili kuthibitisha yale yaliyoelezwa katika kurasa zilizotangulia. Thibitisha, si kwa kutumia mapokeo na mapokeo ya imani za wanadamu zinazopingana, bali kwa kutumia kiwango pekee kilicho sahihi na kilichoidhinishwa na Mungu—Neno la Mungu mwenyewe. Ni ili kurahisisha uchunguzi huo ndiyo maana tumenukuu maandiko mengi sana.

Haitakuwa na maana kujaribu kupatanisha mpango wa Mungu ulioelezwa humu na mawazo mengi uliyokuwa nayo awali na uliyodhani ni ya Kimaandiko, lakini hukuyathibitisha. Utaona kwamba mpango wa Mungu umekamilika na unapatana wenyewe katika kila sehemu, na kwamba unapatana kikamilifu na tabia ambayo Maandiko yanamwelezea Muumba wake mkuu. Ni onyesho la ajabu la hekima, haki, upendo, na nguvu. Unabeba wenyewe uthibitisho wa kuwa na mpangilio unaopita uwezo wa kibinadamu, ukiwa juu ya uwezo wa mwanadamu kuubuni, na karibu kupita uwezo wa mwanadamu kuuelewa.

Bila shaka, maswali yatazuka kuhusu mambo mbalimbali yatakayohitaji ufumbuzi kulingana na mpango uliowasilishwa humu. Funzo la Biblia la makini na la kufikiri litatatua mengi ya maswali hayo mara moja; na kwa yote, tunaweza kusema kwa ujasiri, Hakuna swali unaloweza kuuliza litakalokosa jibu la kutosha, linalopatana kikamilifu na maoni yaliyowasilishwa humu. Machapisho yajayo yatafafanua sehemu mbalimbali za mpango huu mmoja, yakifunua katika kila hatua jinsi mambo yanavyoendana kikamilifu—jambo ambalo ni kweli pekee inayoweza kujivunia. Na ijulikane kwamba hakuna mfumo mwingine wowote wa theolojia unaodai, au uliowahi kujaribu, kupatanisha ndani yake *kila* andiko la Biblia; lakini sisi tunadai hivyo kabisa kwa maoni haya. Kuendana huku si tu na Biblia, bali na tabia ya Mungu na busara takatifu, bila shaka umekwisha

kuvuta usikivu wa msomaji mnyoofu, na kumjaza na kicho, pamoja na tumaini na uhakika. Ni jambo la ajabu kweli, lakini ndivyo hasa tunavyopaswa kutarajia kutoka kwa ILE KWELI, na kutoka kwa mpango wa Mungu wenye hekima na fadhili zisizo na kikomo.

Na wakati Biblia inapofunguka kwa njia hii kutoka katika mtazamo huu, na kufunua mambo ya ajabu (*Zaburi 119:18*), nuru ya siku ya leo inapomulika kanuni mbalimbali za imani na mapokeo ya wanadamu, inayaathiri kwa njia tofauti kabisa. Zinatambulika hata na waumini wake kuwa hazina ukamilifu na zimepotoshwa, na hivyo zinaanza kupuuzwa kwa kiasi fulani; na ingawa watu bado wanazikiri, ni nadra sana kuzifafanua, kwa sababu ya aibu. Na aibu inayoambatana na mapokeo ya imani za kibinadamu inaenea hadi kwenye Biblia, ambayo inadaiwa kimakosa kuwa ndiyo huunga mkono upotoshaji huu wa fikra kana kwamba umetoka kwa Mungu. Hii ndiyo sababu wasomi wengi wanaojiita wa kisasa wanajisikia huru kuanza kuzikana sehemu mbalimbali za Biblia ambazo hazipatani na maoni yao.

Basi, tazama jinsi majaliwa ya Mungu yanavyoshangaza, ambapo kwa wakati huu hasa anawafunulia watoto wake mpango huu mtukufu na wenye kuendana—mpango ambao haukanushi hata sehemu moja, bali unapatanisha kila sehemu na kila neno la Neno lake.

Wakati ufaao unapofika, Kweli inakuwa *chakula kigumu* kwa ajili ya nyumba ya imani, ili wapate kukua kwayo. (*Mathayo 24:45*) Yeyote anayekutana na kweli, na kutambua asili yake, anakuwa na wajibu kwa ajili ya hiyo kweli. Ni lazima aipokee na kuitendea kazi, au aikatae na kuidharau. Kuipuuzia hakuondoi wajibu. Tukiipokea sisi wenyewe, tunakuwa na wajibu *KUIHUSU* pia, kwa sababu ni kwa ajili ya WOTE wa nyumba ya imani; na kila mmoja anayeipokea anakuwa na deni kwake, na, ikiwa yeye ni shahidi mwaminifu, ni lazima awagawie washiriki wengine wa familia ya Mungu.

Nuru yenu na iangaze! Ikiwa itageuka kuwa giza tena, giza hilo litakuwa kuu mno. Inueni nuru! Inueni bendera kwa ajili ya watu!

UFUMAJI WA KIMUNGU

"Tazama Mfuma wa ajabu akikaa
Juu mbinguni – na kitanzi chake chini.
Vipande vya kanyagio hushuka na kupanda.
Huchukua, kama mtandao, zama za giza za ulimwengu,
Huchukua, kama uzi, wafalme na wenye hekima.
Huchukua wakuu na wahudumu wao,
Huchukua hali zote na hatua zote.
Viti vya enzi ni vipande kwenye kifyonza chake.
Majeshi huwafanya vikimbie na kutawanyika –
Mtandao huingia ndani ya uzi lazima:
Mataifa hupanda na kushuka!
Kwa mapenzi ya Mfuma, ndivyo huenda!

Kwa utulivu tazama Mfuma wa ajabu
Akitupa kifyonza chake huku na huko;
Katikati ya kelele na vurugu kali,
Mfuma anaonekana kujua vyema
Kila mwendo na msukosuko,
Kila muungano na machafuko,
Ni nini kitadhihirika katika matokeo makuu!

Ajabu ya utukufu! Ni ufumaji wa namna gani!
Kwa walio wazito wa kuelewa, hauaminiki.
Zama za kubuni hazijui jambo kama hili.
Ni imani pekee iwezayo kuona siri,
Jinsi, katika kumbi za historia,
Ambako nyayo za wenye hekima hupita,
Zulia la ajabu hulala kwa uzuri mkuu!
Laini na nyororo, na daima likienea,
Kana kwamba limetengenezwa kwa miguu ya malaika –
Mizunguko iliyochongwa ikigusanagusa daima:
Kila umbo lina miundo yake,
Maumbo ang'avu zaidi na vivuli laini zaidi,
Kila kimoja kikiangazwa – ni kitendawili gani!
Kutoka msalaba unaopamba katikati.

"Ni msemo – wengine huukataa –
Kwamba nuru yake yote ni ya kuakisiwa;
Kwamba mistari ya zulia hutolewa
Na Jua linalong'aa mbinguni!
Inaaminiwa – na wote wanaoamini –
Kwamba Mungu Mkuu mwenyewe ndiye anayefuma,
Akifichua fumbo la giza la ulimwengu,
Katika nuru ya imani na historia;
Na kadiri mtandao na uzi vinavyopungua,
Hufika mwisho mkuu na wenye utukufu,
Pale zinapoanza Zama za Dhahabu,
Zilizotabiriwa tangu zamani na waonaji na wenye hekima."